**5 FEBRUARI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

__________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

___________

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Saba – Tarehe 5 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali.

Na. 108

**Kuwatambua Vijana Wenye Ujuzi**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatambua Vijana wenye ujuzi ambao hawatambuliki rasmi ili kuwaendeleza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuwatambua vijana wenye ujuzi ambao hautambuliki kwa kuweka mipango ifuatayo:-

(i) Kuboresha mazingira ya kisera ili kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za maendeleo na kuweza kujitegemea kupitia Sera ya Maendeleo ya Vijana (2007) ambayo imefanyiwa marekebisho ikiwa ni Tolea la Mwaka 2024, na Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008;

(ii) Kurasimisha na kutambua ujuzi wa vijana uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu;

(iii) Kubuni na kutekeleza programu maalum kupitia sekta zinazozalisha ajira kwa wingi kama vile Sekta ya Kilimo kupitia programu ya Jenga Kesho Iliyobora, ujasiriamali, na madini kupitia Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow*;

(iv) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa ngazi za Stashahada na Shahada kupitia maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023;

(v) Kujenga miundombinu ya Kimkakati inayochochea uchumi ambayo inakuza ujuzi na inachangia kuzalisha ajira mfano ujenzi wa Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere na barabara ya mwendokasi ya *SGR*;

(vi) Kubuni na kutekeleza programu ya kukuza ujuzi ambayo inalenga kukuza ujuzi kwa nguvu kazi ya Taifa, mfano mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi waliopo kazini na wajasiriamali; na

(vii) Kuweka msisitizo kwenye matumizi ya *TEHAMA* katika kuzalisha fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Latifa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana wengi ambao wamepata ujuzi usio rasmi Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini Serikali bado haiwatambui. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kushirikiana na Wizara hii ya Vijana pamoja na Wizara yetu ya

Elimu, ili kuwasaidia vijana hawa kuingia katika mfumo rasmi ikiwemo angalau kupata vyeti ili waweze kujisaidia katika ajira? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Latifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwenyewe alivyokutana na vijana pale Mwanza, ikiwa ni kundi la kwanza baada ya kuingia katika nafasi ya Urais. Alipokea changamoto nyingi sana, lakini alieleza mikakati na mipango mingi ambayo ililenga kukusudia kuwanyanyua vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa ilikuwa hii ya vijana wengi kuwa na ujuzi, lakini haujarasimishwa. Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais na vilevile maelekezo ya utekelezaji ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba tuanzishe programu maalum ambayo inaitwa *recognition of prior learning*, tulifanya hivyo kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na *VETA*. Hadi sasa zaidi ya vijana 686 kwa kupitia programu ya *Building Better Tomorrow* walirasimishiwa ujuzi na wanapata vyeti kwa ajili ya kutambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, vijana 500 wamepata vyeti kwa maana ya kutambuliwa ujuzi wao ambao wamepata mafunzo ya ziada pamoja na vijana 234 ambao nao walirasimishiwa ujuzi wao wa unenepeshaji wa mifugo kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini vivyo hivyo, katika programu yote kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 tayari vijana zaidi ya 20,334 wameweza kurasimishiwa ujuzi kwa kupata mafunzo kwenye kada mbalimbali zikiwemo Ufundi, Useremala, Ushonaji, Uashi na pia kwenye programu nyingine za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewatumia vijana hawa kupitia halmashauri katika utaratibu wa *force account,* ambapo wametumika katika kufanya ujenzi. Hata wale waliofanya kwenye miradi mikubwa ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameikamilisha, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na ule Mradi wa *SGR* walijifunza kupitia ujenzi na sasa tunawarasimishia ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi yao wanajiandaa kuendelea na masomo katika vyuo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha ujuzi wao na tutawatumia katika kazi za *maintenance*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Koka.

Na. 109

**Hatma ya Shirika la Elimu Kibaha**

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, nini hatma ya Shirika la Elimu Kibaha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Elimu Kibaha lilianzishwa mwaka 1963 kwa lengo la kuondoa umaskini, ujinga na maradhi ambapo ilisababisha kuanzisha huduma za elimu, afya na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tarehe 15 Disemba, 2023, Serikali ilitangaza kuvunja Shirika la Elimu Kibaha ambapo Hospitali ya Tumbi, Kibaha ilitangazwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta namna bora ya kuratibu taasisi zilizo chini ya shirika hilo ili kutoathiri lengo kuu la kuanzishwa kwake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Shirika hili lina ukubwa wa takribani hekari 3,400 na lengo lake kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kuondoa ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kama Serikali imeamua kuangalia upya na kulivunja ili kubaini namna bora kuendesha shirika hili, je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuleta mkakati huo ili tukawashirikishe wananchi wa Kibaha Mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Manispaa ya Mji wa Kibaha iliomba rasmi angalau hekari 1,500 ili ziendelezwe na kuondoa lile eneo ambalo linaonekana ni pori, likiambatana na Barabara ya Dar es Salaam – Morogoro. Je, ni lini Serikali itatenga eneo hili kwa ajili ya manispaa, ikiwa ni pamoja na mkakati wa kufufua shirika hili ili liweze kuleta tija ya kuondoa umaskini, maradhi na ujinga kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake lenye nia ya kutaka kuwasemea wapiga kura wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali yake mawili kwa pamoja. Ni kweli Serikali ilitangaza kuvunja Shirika hili la Elimu la Kibaha. Hata hivyo, Serikali imefanya mapitio ya maamuzi yake na kuamua kwamba, kutokana na sababu za kihistoria, sababu kubwa kabisa na lengo la kuondoa umaskini, ujinga na

maradhi, shirika hili litaendelea kuwepo badala ya kuvunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika muktadha huo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu maeneo ya shirika hili ambayo bado hayajaendelezwa na yanatengeneza mwonekano wa pori katika Manispaa ya Kibaha, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafanya uwekezaji katika Shirika hili la Elimu la Kibaha, ili kuondoa na hadha hiyo ya kuonekana kuna mapori, kutokana na shirika hili kutokuendelezwa na kuwa na eneo kubwa lenye pori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba shirika litaendelezwa na Kibaha watapata mazingira mazuri kabisa ya mwonekano kwenye shirika hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Na. 110

**Ukarabati wa Shule Chakavu – Vunjo**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, ni Shule zipi chakavu katika Jimbo la Vunjo zimewekwa kwenye Mpango wa kufanyiwa ukarabati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilifanya tathmini ya mahitaji na hali ya miundombinu ya shule zote za msingi zikiwemo shule za Jimbo la Vunjo. Aidha, kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2023/2024, Serikali

imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ukarabati, ambapo shilingi bilioni 70.39 zimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa shule 793 zikijumuisha shilingi bilioni 1.58 zilizokarabati shule za msingi 15 na shule za sekondari tatu zilizopo katika Jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa shule chakavu zikiwemo shule za Jimbo la Vunjo kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli Jimbo la Vunjo lina shule nyingi chakavu na mazingira yake yanatishia na ni hatarishi kwa wanafunzi. Kuna Shule kama Yamu, kule Kirua Vunjo Kusini, Lekura, Mamba Kusini, Maande, Mamba Kaskazini, Lotima, Makuyuni, Lole, Mwika Kaskazini, Maua, Kilema Kaskazini, Nduoni, Kirua Vunjo, Uria, Kahe Magharibi, Mangaria, pamoja na Mawanda na Makunduchi, kule Kirua Vunjo Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza; ninaomba Serikali itupe uhakika kwamba, katika mwaka huu unaokuja basi hizi zitaingizwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ninaomba Waziri akubali kutembelea angalau baadhi ya hizi shule ili aone mazingira yaliyopo. Tafadhali, tafadhali! Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atutembelee ili awape watu uhakika kwamba kweli anafahamu mazingira ya kule Vunjo kwenye Shule za Msingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei kwa kuuliza maswali haya ya msingi kabisa kwa lengo la kutetea wananchi wake kwenye Sekta ya Elimu katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Bajeti 2023/2024 Serikali ilileta jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Njiapanda, lakini katika Mwaka wa Bajeti 2024/2025, Serikali inaleta fedha kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Kahe; Miruneni, Horia, na Rua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ushauri wake wa kwamba niweze kutembelea katika jimbo lake kuona miundombinu ya shule hizi chakavu anazozitaja, nimeupokea na nitaweka kwenye ratiba ili niweze kufika nijionee mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa shule hizi chakavu na zikiwemo nyingine nyingi ambazo zipo kwenye jimbo lako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Hai, tuna shule 77 ambazo ni chakavu sana, kwa sababu shule zetu zimejengwa kuanzia mwaka 1952 na kuendelea. Nimeshawasilisha andiko maalum TAMISEMI la kuomba fedha za kufanya ukarabati, Shule kama Kyuu, Lerai, Mroma, Lukani, Weruweru, Lyamungo, Laskika, Lambo-Estate, Nkwamakuu, Mkoraya, Tumona, Gezaulole, Nkokashu, Kwa Sangire na nyingine ziko 77 ni chakavu sana. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha ya kufanya marekebisho na matengenezo ya shule hizi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kwa kweli amekuwa akipaza sauti yake kwa

ajili ya wananchi wake wa Hai ili waweze kupata miundombinu iliyo bora katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, maombi yao rasmi tuliyapata, tumeyapokea, tunayachakata na nimhakikishie kwamba Serikali italeta fedha ili iweze kuzifikia shule hizo katika jimbo lako kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, uchakavu wa shule za msingi katika Jimbo la Kibaha ni mkubwa na tulishaleta maombi maalumu kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati wa Shule ya Ngwale, Dutumi, Maghindu, pamoja na Kipangege. Ni lini Serikali itatutengea pesa na kutupatia ili tuweze kuzifanyia ukarabati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake makini sana linalolenga kuwasemea wananchi wake kuona wanapata mazingira mazuri ya wanafunzi kusomea, kwa maana ya kuboresha Sekta ya Elimu katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya tathmini ya hali ya miundombinu ya elimu kwa maana ya elimu ya msingi na sekondari mwaka 2022/2023 na ikabaini kwamba katika miundombinu asilimia 5.3 ni mazingira au miundombinu ambayo inahitaji kubomolewa na kujengwa upya kwa maana ipo katika hali mbaya kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna asilimia 24.4 ambazo zinahitaji ukarabati mkubwa, kuna asilimia 44.1 ya miundombinu katika Sekta hii ya Elimu ambayo inahitaji ukarabati

mdogo na 26.2% ya miundombinu katika Sekta ya Elimu ambayo ipo katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa wakati huu Serikali inajitahidi sana na inafanya uwekezaji wa kipaumbele kwenye miundombinu inayokabiliwa na hali mbaya sana, inayohitaji kubomolewa na kujengwa upya, pamoja na ile inayohitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, maombi yao tumeyapokea, tunayachakata na lengo la Serikali ni kufikia maeneo mengi yenye uhitaji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafika ili iweze kuleta fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu chakavu katika jimbo lako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris.

Na. 111

**Hitaji la Vituo vya Afya Kata ya Singisa na Bwakila Juu**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya Kata ya Singisa na Bwakila Juu katika Jimbo la Morogoro Kusini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za Kimkakati kote nchini, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasanga na Mkulazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ambavyo vimeanza kutoa huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* na majengo kwa ajili ya huduma za upasuaji wa dharura kwa akinamama wajawazito ambapo ujenzi wake upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Singisa ina jumla ya wananchi 14,812, vijiji saba na zahanati moja, hivyo Serikali itafanya tathmini ya Kata hiyo ikiwa inakidhi vigezo vya kata ya kimkakati na mpango wa ujenzi wa kituo cha afya utaandaliwa. Aidha, Kata ya Bwakila juu ina jumla wananchi 6,776, vijiji vitatu na zahanati mbili hivyo haikidhi vigezo vya kuwa na kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha zahanati zilizopo katika Kata ya Bwakila Juu ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Inno.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ninataka nijue, swali la kwanza; ni idadi ya watu wangapi ambacho ndicho kigezo cha kuwa na kituo cha afya, wakati sera tuliyokuwa nayo nyuma ilikuwa inazungumzia suala la kila kata kuwa na kituo cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kata ya Singisa katika mazingira iliyopo inaonekana kwamba inaweza kukidhi vigezo. Je, katika vile vituo vya afya ambavyo tuliahidiwa kila Mbunge hapa Bungeni, je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kupeleka kituo cha afya hicho katika Kata ya Singisa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ujenzi wa vituo vya afya unazingatia vigezo kadhaa, moja ya kigezo ni idadi ya wananchi katika eneo husika na kiwango cha chini cha wananchi ambao wanaweza wakafikiriwa kujengewa kituo cha afya ni wananchi wasiopungua 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na idadi ya wananchi kuna vigezo vingine kama umbali kutoka kituo cha jirani zaidi cha huduma, lakini na hali ya kijiografia ya eneo husika. Kwa hiyo, kwa

Kata ya Singisa kwa idadi hii ya wananchi tunaamini hii ni sensa ya 2022 walikuwa 14,000 na zaidi wanaweza wakawa wameshafika 15,000. Kwa hiyo, tutafanya tathmini ya kuona uwezekano wa kujenga kituo cha afya katika Kata hii ya Singisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la vituo vya afya kwa kila jimbo. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikwishatoa maelekezo kwa ajili ya kujenga vituo vya afya kila jimbo katika majimbo yote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge ikiwa kipaumbele cha jimbo lake ni kituo cha afya katika Kata ya Singisa, sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI tulishaomba wawasilishe mapendekezo ya kata hizo na ikiwa uliwasilisha pendekezo la kata hii tutahakikisha fedha ikipatikana inakwenda kujenga kituo cha afya katika kata ambayo umeipendekeza. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Kwenye Jimbo la Igunga, Kata ya Kining'inila Serikali ilikuwa imetuahidi kutujengea kituo cha afya kupitia hiyo Programu ya Fedha za *World Bank* kwa ajili ya kuwahudumia Wananchi wa Kata ya Kining'inila, Mwamashimba, Mwamakona, Mbutu na Isakamaliwa. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huu wa kituo hicho cha afya? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa vituo vya afya kupitia Benki ya Dunia kwa maana ya Mradi wa *TMCHIP* na ni kweli kwamba Jimbo la Igunga lina kata ambayo imeingizwa kwenye huu mpango pamoja na majimbo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imeshaanza utekelezaji wa awamu ya kwanza katika vituo vyote ambavyo vimewekwa kwenye mpango huo. Hivi karibuni tutakwenda kwenye mpango awamu ya pili ambapo vituo vingine vyote na zahanati ambazo zimeainishwa zitapelekewa fedha kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kata yako hiyo ipo na ni kipaumbele na ipo kwenye mradi huu. Tutahakikisha fedha inakwenda kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Vita Kawawa; kwa niaba yake, Mheshimiwa Raymond.

Na. 112

**Hitaji la Kituo cha Mabasi – Namtumbo**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Kisasa cha Mabasi - Namtumbo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhitaji wa kituo cha mabasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ili kuboresha huduma za usafiri. Aidha, Halmashauri imefanya tathmini ya ujenzi wa stendi hiyo na kuanza hatua za awali za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kazi zilizofanyika ni pamoja na kutenga eneo lenye ukubwa wa ekari 3.18 lililopo

eneo la Muungano Namtumbo Mjini na kupata hati miliki ya eneo hilo; kuchonga barabara ya kuingia na kutoka; ujenzi wa baadhi ya miundombinu ya awali ambayo ni jengo dogo la abiria, choo cha abiria na mabanda ya biashara ndogondogo. Kazi hizo zimegharimu jumla ya shilingi milioni 34.7

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri imekamilisha andiko la mradi huo ikiwa ni pamoja na kukamilisha michoro, ramani na makadirio ya gharama. Mradi huo unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 3.5 na hatua inayofuata ni uwasilishaji wa andiko hilo kwa ajili ya upembuzi na kupata fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yametupa mwanga. Swali la kwanza; kwa kuwa kutokuwepo kwa stendi hiyo kunasababisha watu wengi sana kupata ajali za pikipiki, bodaboda na bajaji wakati wakiunganisha kwenye vituo vidogovidogo. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka zoezi hilo kufanyika kwa haraka zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa hali iliyopo Namtumbo inafanana kabisa na hali iliyopo Moshi Manispaa, ni lini stendi ya Ngagamfumuni itakamilika? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ina idadi kubwa ya wananchi wapatao 271,000 na haina stendi kubwa ya mabasi kwa maana ya stendi ya wilaya. Serikali imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba halmashauri zetu zinakuwa na stendi za kisasa ili kutoa huduma bora zaidi za usafiri kwa wananchi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari Serikali imetoa

maelekezo kwa Halmashauri ya Namtumbo na wamekwishaandaa andiko na wameshatenga eneo kazi inayobaki sasa ni kufanya tathmni ya andiko hilo na fedha itatafutwa kwa ajili ya kujenga stendi hiyo ili wananchi waweze kupata huduma hiyo nzuri ya usafiri kama ilivyo dhamira ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusiana na stendi katika Manispaa ya Moshi, tunatambua kwamba Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi lakini kuna changamoto zilijitokeza kati ya manispaa na mkandarasi; Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Manispaa ya Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro tunaendelea kutatua ule mkwamo ili ujenzi wa stendi uweze kuendelea na wananchi wa Manispaa ya Moshi wapate stendi iliyo bora zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Ninataka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga stendi nzuri na ya kisasa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ileje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba halmashauri zetu ambazo zina idadi kubwa ya wananchi zinakuwa na stendi bora kabisa kwa ajili ya huduma za usafiri. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni moja ya halmashauri ambazo zitawekwa kwenye mpango huo na kupewa kipaumbele ili stendi hiyo iweze kujengwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Chaurembo jiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi kubwa ya mkoa katika eneo la *TACRI* pale Vwawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Hasunga ameuliza swali hili mara kadhaa na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Songwe, lakini ninaomba niwahakikishie tu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali sikivu sana na tayari tumeshaweka mpango kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Songwe na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi ya mabasi katika eneo la Vwawa katika Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, haina stendi ya mabasi yaendayo Kusini, je, Serikali haioni ipo haja kwa sasa kutumia ile stendi ya mwendokasi kama stendi ya mabasi yaendayo kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa stendi ya mwendokasi una madhumuni mahsusi kwa ajili ya kupunguza msongamano wa mabasi katika Jiji la Dar es Salaam na kwa hivyo ni vema sana tusimame kwenye mpango wa matumizi wa stendi ile ya Mwendokasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua sana kwamba Manispaa ya Temeke haina stendi kubwa na hasa ya Mikoa ya Kusini. Ninafahamu kulikuwa na mpango wa kujenga eneo lile linalopakana na Temeke pamoja na Mkuranga kuna eneo kubwa

liliainishwa kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi yanayokwenda Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kufanya tathmini na kuandaa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa stendi katika Manispaa ya Temeke, lakini pia stendi kwa ajili ya mabasi yanayokwenda kusini mwa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Nancy Hassan, kwa niaba.

Na. 113

**Mafunzo kwa Watumishi wa Umma**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma ili kuendana na kasi ya maendeleo na kuongeza ufanisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha watumishi wa umma wanaendelezwa katika taaluma zao ili kuendana na kasi ya maendeleo na kuongeza ufanisi, waajiri wote wanapaswa kuainisha mahitaji ya mafunzo, kuandaa mipango ya mafunzo na kutenga bajeti kila mwaka na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na waajiri kutenga fedha za mafunzo kwa watumishi wa umma, Serikali pia imekuwa ikipokea fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kutoka maeneo mbalimbali ya kimkakati kwa kuzingatia vipaumbele vya Kitaifa kutoka kwa wadau mbalimbali wa Maendeleo wakiwemo

Korea, China, India, Indonesia, Japan, Singapore, Misri, Malaysia, Thailand na Bangladesh ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 zaidi ya watumishi 1,278 walinufaika na fursa hizo. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; katika miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeajiri takribani watumishi 140,000. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inatoa mafunzo elekezi ya awali kwa watumishi wapya ambao wanaajiriwa katika utumishi wa umma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba taasisi zinapanga bajeti ya mafunzo kwa watumishi kazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Simon kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia mambo ya watumishi hasa wa Jimbo lake la Busega. Nikianza na suala la mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya, ni kweli Serikali kwa kipindi hiki cha miaka minne imeweza kuajiri watumishi takribani 140,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mwaka 2011 Serikali ilitoa waraka kwa taasisi zote za umma kuhakikisha watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wanapewa mafunzo elekezi ndani ya miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia Bunge hili Tukufu kukumbusha waajiri wote, wanapowapokea waajiriwa kwa mara ya kwanza wahakikishe wanawapa mafunzo hayo elekezi ili waweze kujua taratibu, misingi ya utumishi wa umma, kanuni na

sheria na pia utendaji bora katika utumishi wa umma. Hii imeelezwa wazi kwamba wale wanaoajiriwa Serikali Kuu na mashirika ya umma watapewa mafunzo na Chuo chetu cha Utumishi wa Umma; wale wanaoajiriwa kwa maana ya Serikali za Mitaa jukumu hilo kimepewa Chuo cha Serikali za Mitaa pale Hombolo; na wale wanaoajiriwa kwa kada za sheria watatakiwa kupata mafunzo elekezi na Chuo cha Uongozi wa Mahakama kwa maana ya Lushoto. Ninashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, anataka kujua juu ya bajeti, tayari Serikali tulishatoa waraka kwa maana Ofisi ya Rais, Utumishi, kuhakikisha waajiri wote kwa mwaka huu wa fedha wanatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya mafunzo na mwishoni mwa mwaka huu wa fedha tutafanya tathmini tuone utekelezaji wa jambo hilo kwa kuwa ni muhimu katika ufanisi wa watumishi wetu wa umma, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Tayari.

**NAIBU SPIKA:** Ameshauliza, *okay*. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Oscar Ishengoma.

Na. 114

**Posho ya Mazingira Magumu kwa Watumishi Mikoa ya Pembezoni**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa posho ya mazingira magumu wafanyakazi hasa walimu wanaopangiwa kazi mikoa ya pembezoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za kuishi walimu hususan walimu wa umma na watumishi wa kada za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, ukarabati wa miundombinu ya barabara; kuboresha huduma za jamii kama vile, elimu, afya, maji, nishati ya umeme na mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, huduma hizi zinawanufaisha watumishi wa umma wote pamoja na wanaofanya kazi katika mikoa ya pembezoni. Hata hivyo, Serikali haijatoa mwongozo mahsusi wa kulipa posho ya mazingira magumu kwa watumishi wa kada ya ualimu na watumishi wengine wa umma wanaopangiwa vituo vya kazi katika mikoa ya pembezoni kutokana na changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Wilaya ya Muleba ina kata tano ambazo ziko katikati ya Ziwa Victoria ambako huduma nyingi za Serikali hazijafika. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutupatia angalau *ambulance* kwa ajili ya kuharakisha usafiri hasa walimu na wafanyakazi wengine wanapopata matatizo ya afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kuna taasisi za Serikali ambazo zinatoa motisha kwa wafanyakazi wake; je, Serikali haioni haja ya kuharakisha huo mwongozo ambao imeusema hapa kwa ajili ya kuwaboreshea maisha wafanyakazi

hasa walimu na manesi ambao wako pembezoni kabisa mwa nchi ambako hakuna umeme na nyumba za kuishi ili waweze kutumikia Serikali kwa moyo wao wote? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; nimpongeze kwa namna anavyowasemea wananchi wake wa Jimbo la Muleba Kusini. Suala la kwanza, ameongelea juu ya *ambulance*. Nimhakikishie Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuboresha huduma za afya katika maeneo yote nchini na hivi karibuni Mheshimiwa Rais alitoa *ambulance* nchi nzima, na anaendelea kufanya hivyo kutokana na mazingira mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kikoyo jambo la kupeleka *ambulance* katika kata hiyo yenye changamoto tutawasiliana na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuona namna ya kupeleka *ambulance* katika eneo hilo na hiyo ndiyo nia ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la motisha kwa watumishi hili ni jambo la jumla. Mheshimiwa Rais alionesha nia ya dhati na hata juzi alipokuwa anazindua Sera ya Elimu ya 2014, Toleo la Mwaka 2023 amesema wazi tunaenda kupitia upya maslahi hasa maslahi ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie pia, suala hili la motisha ni kati ya mambo ambayo tunayapa kipaumbele kama Serikali na kutokana na hali ya uchumi na upatikanaji wa fedha nikuhakikishie jambo hili tutalitekeleza na hasa kwa watumishi wako wa Jimbo la Muleba Kusini.  Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Taska.

Na. 115

**Fomula ya Malipo ya Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa Wastaafu waliokuwa Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaodai *formula* haikufuatwa wakati wanalipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhakiki uliofanyika, ilibainika kuwa, wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaoidai Serikali kutokana na dosari ya ukokotozi wa fomula wanadai shilingi bilioni 1.3 ambapo shilingi bilioni 1.17 kwa wastaafu walio hai 146 na shilingi milioni 151.1 kwa wastaafu 21 waliofariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhakiki, tumewasilisha orodha ya madeni kwa Wizara ya Fedha ili yalipwe pindi pesa zitakapopatikana. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa wafanyakazi hawa wamekuwa wakiidai Serikali toka mwaka 1977

na wengi wao wamefariki bila kupata mafao yao. Je, Serikali haioni haja ya kuharakisha mchakato wa kuwalipa wafanyakazi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanadai kwamba Serikali iliwalipa pesa pungufu kinyume na kikokotoo ambacho kilitolewa na *Liquidator*. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukaa nao mezani ili kuangalia madai yao ambayo wanadai na walitakiwa walipwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee kujibu maswali ya maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna wafanyakazi ambao wamedai kwa muda mrefu na wengine wamefariki, lakini msingi wa swali hili ulikuwa ni kufuatilia na kuweza kujua yale mapungufu ya wafanyakazi ambao walikuwa chini ya *TTCL* kabla na baada ya kubinafsishwa na wengine ambao walipeleka kesi Mahakamani (Kesi Namba 69 ya Mwaka 2005) na wengine ambao walikuwa wafanyakazi wa *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, sisi kupitia Ofisi ya Mtunza Hazina tumeweza kuhakiki madeni hayo na tumegundua kweli, kulikuwa na madeni ambayo yamekosewa kutokana na ukokotoaji, ambayo yalifanya waweze kupata upungufu wa fedha walizokuwa wakilipwa kila mwezi. Tumefuatilia na tumeweza kuhakiki madeni hayo na Ofisi ya *TR* ilivyoweza kugundua, imekuja na *figure* hii ya *1.3 billion* ambayo sasa tumeipeleka Wizara ya Fedha, ili waweze kuandaa mkakati wa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna wafanyakazi wengine ambao kwa kweli, Serikali bado inaendelea kuhakiki

(Kwa wale wafanyakazi wengine wa kampuni nyingine ambazo zilikuwa chini ya *East Africa* na Wafanyakazi wa *East Africa* kwa ujumla). Tutakapogundua kwamba, kweli kuna watu wanadai fedha hizo, Serikali chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, itawalipa wale wote ambao wanadai madeni hayo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nina mwaka wa kumi katika Bunge hili na swali hili limekuwa likiulizwa mara kwa mara. Je, Serikali haioni sasa, ina wajibu wa kufanya haraka iwezekanavyo ili watu hawa waweze kulipwa fedha zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna watu wanadai fedha kwa muda mrefu na wakati mwingine inakuwa ni vigumu kupata vielelezo. Hata hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inakwenda kulipa madeni yale yote ambayo yatakuwa yamekwisha kuhakikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Tunza Malapo.

Na. 116

**Tathmini ya Zoezi la Upandaji Miti Nchini**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, Serikali imefanya Tathmini ya kujua ni Miti mingapi inayopandwa inatunzwa na kukua ili kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imekuwa ikifanya tathmini ya upandaji miti kwa kila mwaka ili kukabiliana na uharibifu wa ardhi, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na kupambana dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 – 2023/2024 tathmini imebainisha kuwa, jumla ya miti milioni 866.7 ilipandwa ambapo kati ya miti hiyo, miti milioni 686.24 ilistawi, sawa na 82.3%. Aidha, katika msimu wa mwaka 2024/2025, Serikali inaendelea kufanya tathmini, ili kubaini idadi ya miti iliyopandwa na iliyostawi kwa maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi na Sekta binafsi kuendelea kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali nchini, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutunza mazingira. Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninaomba kutoa wito kwa jamii nzima ya Watanzania kutumia mvua zinazonyesha kipindi hiki kwa kupanda miti katika maeneo yetu mbalimbali. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu hayo ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nataka kujua mkakati wa Serikali ni upi ili kuhakikisha miti yote inayopandwa inatunzwa na kukua ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, kwani inatumia pesa nyingi na muda mwingi wa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nataka kujua kuna mkakati gani wa kuwashirikisha wanafunzi hasa wa shule za msingi kuwa na tabia ya kupanda na kutunza miti katika mazingira yanayowazunguka, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto ya Watanzania wengi kupanda miti na hatimaye inakuwa haipati ufuatiliaji. Hata hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, tumechukua hatua mbalimbali; moja ni kwamba, tunao maafisa wetu, viungo, katika mikoa na halmashauri zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopanda miti tunakuwa tunawapa maelekezo waifuatilie. Vilevile, tunao utaratibu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa baadhi ya barabara na baadhi ya maeneo huwa tuna utamaduni wa kumwagilia maji na kufuatilia miti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo na madhumuni ni kwamba, kama tumepanda miti milioni moja, tuhakikishe ile miti inakua na inafikia lengo la kutunza mazingira, lakini kupitia ziara zetu za mara kwa mara katika maeneo tofauti na kupitia matukio tofauti, huwa tunapanda miti na kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu wanafunzi, wakati ule Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, alipokuwa Makamu wa Rais alianzisha kampeni mbalimbali za utunzaji wa mazingira. Alianzisha kampeni ya kutunza vyanzo vya maji, *clean cooking* na kampeni maalum ya kusoma na mti, ambapo Serikali ilikuwa inawataka wanafunzi wote wa shule za sekondari, msingi, vyuo na vyuo vikuu, wahakikishe kuwa

wanapanda miti wakati wapo vyuoni na shuleni, lengo na madhumuni ni miti hii iweze kukua kwa muda uliokusudiwa. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha inaviongezea nguvu vikundi vinavyojishughulisha na upandaji miti kandokando ya bahari ili kurudisha uoto wa asili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto kubwa ya baadhi ya watu kukata miti iliyopo pembezoni mwa kandokando ya Bahari hasa miti ya mikoko na mwisho wa siku wanaharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, zipo jitihada ambazo tumezifanya; kwanza, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi, ili kuwaeleza umuhimu wa uwepo wa mikoko. Sasa hivi kumekuwa kuna changamoto kubwa, maji ya bahari kuingia kwenye makazi, kuingia kwenye vipando vya wananchi visivyostahimili maji ya chumvi. Hii yote ni kwa sababu, mikoko imekatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuendelea kutoa mikoko bure ili iendelee kupandwa kwenye yale maeneo ya bahari, lakini zaidi kuendelea kutoa miradi. Pia, miongoni mwa miradi inayotolewa katika Ofisi ya Makamu wa Rais ni pamoja na upandaji wa miti pembezoni mwa bahari, hasa miche ya mikoko. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

Na. 117

**Kuunganisha Umeme kwa Gharama Nafuu Maeneo ya Pembezoni, Tanga Mjini**

**MHE. UMMY A. MWALIMU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaunganishia umeme wa gharama nafuu wananchi wa maeneo ya pembezoni yenye sifa za Vijiji, Tanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurahisisha upatikanaji wa huduma ya umeme wa bei nafuu kwa maeneo ya pembezoni mwa Jimbo la Tanga Mjini, Serikali kupitia *REA,* inaendelea kutekeleza Mradi wa *Peri-Urban III* ambapo Mkandarasi aitwaye *OK Electrical* anaendelea na zoezi la kuunga wateja kwa baadhi ya mitaa kwa gharama ya shilingi 27,000 ambapo mpaka sasa jumla ya wateja 1,302 wameshaunganishiwa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, maeneo yaliyosalia yapo kwenye mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 vya kila Mbunge, ambapo Jimbo la Tanga Mjini litapelekewa umeme kwenye mitaa 15. Serikali inaendelea kuwahimiza wananchi kuunganisha umeme wakati ambapo ujenzi wa miradi unaendelea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ummy.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, kata 10 kati ya kata 27 za Halmashauri ya Jiji la Tanga zina mitaa yenye sifa za vijiji, kama vijiji vya Muheza, Handeni, Mkinga, Pangani na Korogwe Vijijini.

Kwa nini mitaa hii yote isiingizwe katika utaratibu wa wananchi kupata umeme wa *REA* wa shilingi 27,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa, Wakuu wa Nchi wamepitisha Azimio la Nishati Safi la Dar es Salaam chini ya uenyeji wa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa nini Serikali isianzishe programu maalum ya kuwawezesha wananchi kuunganisha umeme wa mkopo halafu walipe kidogo kidogo, kupitia matumizi ya kila siku ya umeme? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kuhusiana na Mitaa ya Tanga Mjini ambayo Mheshimiwa amesema iunganishwe na *REA* kwa sababu, ina sifa za vijiji. Ndiyo maana Serikali tunatekeleza miradi ya *Peri-Urban* kwenye maeneo haya, ili kurahisisha kuwafikia wateja wengi zaidi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa sasa hivi ndiyo maana tumepeleka umeme katika vitongoji 15, lakini miradi ya *Peri-Urban* inaendelea, ili wananchi waweze kuunganisha umeme kwa gharama nafuu. Jambo la kuendelea kuwasisitiza, ni kwamba, wakati miradi inaendelea, basi wananchi waweze kuunganisha umeme, ili kuepuka kadhia pale ambapo miradi inaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la pili la wananchi kuunganisha umeme na kulipa kidogo kidogo. Ninapokea wazo la Mheshimiwa Mbunge na tutaendelea kulichakata ili kuona namna ya kulifanyia kazi kwa sababu, huko nyuma tayari *TANESCO* walijaribu kufanya hivyo, baadaye wakawapatia *Akiba Commercial Bank* kufanya hivyo, lakini marejesho hayakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuchakata kuona namna ambayo tunaendelea kulifanyia kazi ili wananchi

waendelee kupata huduma. Kwa hiyo, ni wazo zuri, tutaendelea kulichakata. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganishia umeme wananchi wa Kijiji cha Magugu, Jimbo la Babati Vijijini, kwa bei ya shilingi 27,000 badala ya 321,000?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Maeneo ambayo ni Vijiji-Miji ambayo ina *center* ndogo, gharama yake ya kuunganishwa umeme ni shilingi 321,000. Ndiyo maana tunapeleka Miradi ya Vitongoji, kwa ajili ya kuwafikishia wananchi huduma ili wakati wanaunganisha gharama ipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha tutaongeza vijiji hamsini kwa jimbo ambalo ameuliza Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, niendelee kuwasisitiza wananchi, wakati miradi inaendelea waweze kuunganisha umeme ili kuweza kukwepa kadhia hii wakati miradi inaisha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mitaa ya Masemele, Kilabela, Bujingwa, Nyanguku, Butingo na Koronto, ilikuwa katika ile mitaa 15 iliyokuwa inawekewa umeme wa *REA*. Hata hivyo, baadaye mitaa hii imeondolewa kwa sababu, iko mbali na *line* kubwa. Je, ni lini sasa mitaa hii itasogezewa *line* kubwa, ili na wao waweze kupata umeme kama ambavyo wanapata wengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Miradi ambayo sasahivi tunakwenda kwenye vitongoji ni miradi ambayo ni jazilizi, lakini inajumuisha kujenga miundombinu kwenye maeneo ambayo yamepitiwa tu na *line* kubwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika miradi tunayoianza (kama hii ya vitongoji takribani 9,000 tutakayoianza kwa mwaka huu wa fedha), basi na mitaa hiyo tutaona namna ya kuiangalia ili na yenyewe iweze kunufaika na huduma hii. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Rehema Juma.

Na. 118

**Maeneo ya Hifadhi Yaliyokosa Sifa Kutumika kwa Shughuli za Kibinadamu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuruhusu maeneo ya hifadhi yaliyokosa sifa yatumike kwa matumizi ya kilimo na makazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia maelekezo ya Serikali imefuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,962 kwa Tangazo la Serikali Na. 427/2020 yaliyokosa sifa na kurejeshwa kwa wananchi, kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara imefuta hifadhi za misitu saba zenye ukubwa wa ekari 46,715 kwa Tangazo la Serikali Na. 544/2020 zilizokosa sifa na kurejeshwa kwa wananchi, kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo makazi na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine Wizara imetekeleza uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa kumega takriban ekari 973,380.906 kutoka katika maeneo ya hifadhi za Taifa, mapori ya akiba, mapori tengefu na hifadhi za misitu, kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Vijiji vya Mwanduti, Kipendamoyo Mashariki, Kasandalala, Imagi, Usinga na Kakoko vina *GN* ya Serikali na vimesajiliwa. Hata hivyo, mpaka dakika hii vinasemekana na vinaonekana viko kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ukweli ni kwamba, vijiji hivi vimeshakosa hadhi kuwa kwenye hifadhi kwa sababu, hakuna wanyama, misitu wala hakuna vyanzo vya maji kama mito na maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wananchi wetu wanaendelea kuishi kwa tabu sana katika maeneo haya, wanasumbuliwa sana na watu wa maliasili na wanaishi maisha ya taabu ya kuhangaika. Je, pamoja na hayo majibu uliyosema, ni kwa nini Serikali haioni haja ya kuendelea kufanya upanuzi wa maeneo hayo na kuvirasimisha hivi vijiji viwe ni makazi ya wananchi na wafanye shughuli za kibinadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana nami kwenda jimboni kwangu ili akajionee hali halisi ya hivi vijiji na ashuhudie haya ninayoyaongea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja ni maeneo ambayo yapo chini ya Wakala wa Usimamizi wa

Huduma za Misitu Tanzania. Maeneo haya ni ardhi oevu, ambayo ni bakuli la kukinga maji ambayo yanaingia Mto Malagarasi na hatimaye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni muhimu sana kwa ikolojia ya eneo lile na uhifadhi katika nchi yetu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira wakati Serikali inaangalia jinsi ambavyo kwanza itarejesha yale ambayo yamepoteza hadhi kurejeshewa hadhi yake na pale itakapoonekana kuna uhitaji wa kuyamega maeneo hayo, basi mchakato wa kawaida ndani ya Serikali utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, niko tayari kuongozana naye kwenda kwenye maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Hifadhi ya Wamimbiki ina mgogoro wa muda mrefu wa mipaka na vijiji vitano ambavyo ni Kanga, Kaole, Kunke, Muhumbilo na Kidudwe. Pia, kwa kuwa, Mheshimiwa Rais kupitia timu ya Mawaziri nane ameridhia kutoa hekta 7,500. Je, Wizara ya Maliasili mko tayari kushirikiana na Wizara ya Ardhi kwenda kupima na kuwapa wananchi haya maeneo na kuondoa huu mgogoro? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya jambo hili na timu ya kushughulikia jambo hili chini ya uongozi wa mkoa, iko uwandani na inaendelea na kazi. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira, ndani ya muda mfupi jambo hili litakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Tamina Abbas.

Na. 119

**Kampeni ya SMAUJATA Nchini**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo wa Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) imeleta matokeo gani tangu kuzinduliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Kampeni Huru ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania yaani SMAUJATA, Tarehe 16 Juni, 2022, kampeni imeweza kuhamasisha wananchi 10,714 kutoka Tanzania Bara na 191 kutoka Zanzibar kujiunga na Kampeni hiyo kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Desemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kampeni imeongeza hamasa ya jamii ya kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kupitia wana SMAUJATA na watendaji wengine, hivyo kusababisha jumla ya matukio 2,533 ya ukatili wa kijinsia na watoto katika mikoa yote kubainika na kuwasilishwa katika mamlaka za usimamizi wa sheria, kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni ya SMAUJATA imeongeza uelewa wa jamii kuhusu vitendo vya ukatili kwa kuwa, uongozi wa kampeni ya SMAUJATA upo kuanzia ngazi ya huduma za msingi mpaka Taifa. Aidha, kampeni hii imepunguza pengo la upungufu wa wataalam wanaotakiwa kutoa elimu ya ukatili katika jamii, hasa ikizingatiwa kuwa, kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii ikilinganishwa na mahitaji halisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tamima.

**MHE. TAMIMA HAJI ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili. Swali la kwanza; je, kampeni hii ni ya muda mrefu au ni endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali za Mikoa na Wilaya zinashiriki vipi katika kampeni hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tamina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kampeni hii ina muda wa miaka mitatu. Vilevile, kampeni hii ya SMAUJATA imeungwa na Wizara ya Mambo ya Ndani na wamejisajili kama *NGO*. Pia, inafanya kazi katika taasisi zote za Serikali kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Serikali, Mikoa pamoja na Wilaya zinashirikiana vema kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na ukatili na utekelezaji mbalimbali wa kupinga ukatili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Matiko.

Na. 120

**Kuboresha Barabara kwa Kuweka Sehemu za Waenda kwa Miguu na Pikipiki Nchini**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isiboreshe barabara zote nchini kwa kuongeza barabara za waenda kwa miguu na pikipiki?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahakikisha kuwa barabara zote mpya zinazojengwa kwa kiwango cha lami zinahusisha ujenzi wa njia za waenda kwa miguu katika maeneo ya majiji, miji na maeneo yaliyojengeka. Kwa barabara ambazo zilijengwa bila kuweka njia za waenda kwa miguu maboresho yamekuwa yanafanyika kwa kujenga njia za waenda kwa miguu kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Majibu ya Serikali kwa kweli yanasikitisha sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; tumeendelea kupoteza Watanzania waenda kwa miguu na waendesha pikipiki hata jana tu tulishuhudia ajali mbaya sana hapo Meriwa na raia wawili wakafariki. Nataka kujua Serikali imejipanga vipi, mathalani unapokuwa unaenda Dar es Salaam waendesha pikipiki wale wanaobeba mkaa, wanabeba mkaa mwingi inaziba hata *visibility* ambapo inapelekea ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajipanga vipi wakati wanaendelea na mkakati wa kujenga barabara hizo walizosema kuhakikisha kwamba Sheria ya Usalama Barabarani inatekelezeka na hawa watu wanaoendesha pikipiki wanafuata hizo sheria ili wasipoteze maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kumekuwepo na mwingiliano mkubwa hasa kwenye hizi *highway* zetu, ukiacha pikipiki utakutana na kondoo, utakutana na mbuzi, utakutana na mbwa, utakutana na wanyama wengine mbalimbali. Wizara hii inashirikiana vipi na Wizara nyingine kama za Mifugo ili waweze kuhakikisha kwamba hawa raia wenye mifugo hii wanahakikisha haingii barabarani na kusababisha ajali za hapa na pale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika jibu langu la msingi kwamba tunakiri kwamba barabara zilizojengwa zamani hazikuwa na hizo *facilities,* lakini barabara zote tunazozijenga sasa hivi kwenye miji, miji mikubwa hata miji inayokua sasa hivi tunazingatia kwamba hicho kinafanyika, tunayo mifano ya hizo barabara nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwa mfano Dodoma hapa ukienda kwenye barabara ya *outer ringroad* utakuta hizo *facilities* zote zipo lakini tuna mpango pia barabara zote zinazotoka katikati ya mji kwenda kuunga na hiyo *ringroad* tutahakikisha kwamba ziko kwenye *design* na zitajengwa. Tunayo barabara tunasema *inner ring* lakini kuna *median* kwa Dodoma hapa barabara zote hizo tutazingatia hicho unachokisema. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale wanaotumia tuna sheria pia ambazo zinamtaka kila anayetumia barabara hizi afuate sheria ambazo zipo zinatumika. Suala la waendesha pikipiki ambao wanavunja sheria vipo vyombo vingine ambavyo vinashughulika nao, ndiyo maana wanachukuliwa hatua kwa sababu sheria hizo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga na barabara ambazo tunajenga ukienda *BRT,* ukienda madaraja ya Tanzanite, Kigongo – Busisi, tunazo barabara tume-*design* Mwanza ambazo tutazijenga njia nne zote zimezingatia hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha msingi ni kwamba wote tunaotumia barabara, anayetumia chombo cha moto, lakini wale pia wanaotembea tume-*design* na tuna sheria inayosema mifugo ni marufuku kupita kwenye barabara. Kwa hiyo, anayepitisha mifugo ama amebeba mkaa kinyume cha taratibu

huyo anavunja sheria na sheria zipo ndiyo maana watu hao wanachukuliwa hatua. Kwa hiyo, tunashirikiana vizuri sana na vyombo vya usalama wenzetu wa Polisi ambao wapo na ndiyo maana zile sheria ndiyo zinazowafanya hawa watu wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nichukue nafasi hii kuwajulisha...

**NAIBU SPIKA:** Ameshakuelewa Mheshimiwa Waziri, umezungumza vizuri majibu yako sahihi pamoja na majibu raia wana haki ya kufuata sheria ambazo zimewekwa kwenye hii nchi, ahsante sana, Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Novemba ulikuwa umekaa kwenye hicho kiti, nikauliza swali la Barabara ya Tarime - Nyamongo ninavyozungumza barabara ile mkandarasi hayupo, njia ya pembezoni imeharibika, waenda kwa miguu hawapiti na magari hayapiti ni matusi kule Tarime. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa jambo hili? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba alichouliza swali la msingi hapa ni barabara ambazo zimetumika na kuwatengenezea waenda kwa miguu ama baiskeli njia tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalosema hii ni barabara za mchepuko za muda kwa maana ya *diversion* ambazo mkandarasi aliyepo anayejenga barabara hiyo ya Tarime kwenda Nyamongo anatakiwa ajenge *diversion* na ni wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama barabara hizo hazipitiki na kwa kuwa ni barabara ambazo zipo kwa ujenzi kwa sasa na zinatumika kwa muda nimweleze tu Meneja wa Mkoa wa

Mara ahakikishe kwamba huyo mkandarasi anatengeneza hizo barabara na wananchi wanapita bila kukwama. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Ngonyani.

Na. 121

**Fidia kwa Wananchi Ujenzi wa Barabara ya Lumecha – Londo - Mpepo Morogoro**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, lini wananchi wa vijiji vya pembezoni mwa barabara ya Lumecha – Londo – Mpepo Morogoro watalipwa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Lumecha – Londo – Kilosa kwa Mpepo. Sambamba na hilo, Serikali pia inatafuta fedha kwa ajili ya fidia kwa wananchi wote wanaostahili kulipwa fidia kwa Mujibu wa Sheria, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka 17 sasa tangu Serikali itwae maeneo ya pembezoni mwa barabara hiyo kwa wananchi na kwamba wananchi bado hawajapewa fidia. Je, Serikali imejipangaje kufanya mapitio upya ya tathmini ili watakapokwenda kulipwa walipwe pesa kulingana na thamani iliyopo sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Miundombinu bajeti iliyopita alisimama hapa na kusema kwamba barabara hii inakwenda kujengwa kwa mtindo wa *EPC+F* na kwamba barabara hii haijaanza kujengwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hii inaanza kujengwa badala ya hizi stori stori wanazotupa sasa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma tunazichoka? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kujibu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge). Sheria iko wazi ikiishapita miezi sita baada ya kufanya usanifu wananchi hawa wanastahili fidia na kama imepita miaka miwili tunatakiwa tufanye mapitio tena na kutafuta gharama za fidia kwa upya kabisa. Kwa hiyo, kama miaka ni 17 nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ili kuwalipa wananchi hao fidia maana yake zoezi hilo litarudiwa upya ili tuende na gharama ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge ambalo ni suala la ujenzi tofauti na fidia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nilishatoa majibu kwamba barabara zote zilizokuwa za *EPC+F* utaratibu umetengenezwa wa namna ya kuzitekeleza tofauti na mpango uliokuwepo. Kamati ilishaundwa na tayari taratibu zinafanyika ili barabara hii iweze kujengwa kwa utaratibu mwingine tofauti na wa *EPC+F*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri; je, ni lini sasa wananchi waliopisha Barabara ya Uyole - Songwe watalipwa fidia? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni barabara ya Jiji la Mbeya na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Wizara tulishakamilisha kila kitu na tunategemea muda wowote Wizara ya Fedha kupitia Hazina watatupatia fedha ili wananchi hawa ambao wamepisha huo ujenzi waweze kulipwa fidia zao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Bugene kwenda Itera kuja Songambele kupita Nkwenda, lakini pia kwenda Rwenkorongo, tumeambiwa kwamba ujenzi unaanza na kweli tumeona wakandarasi wameshaanza kujenga maeneo yao ya kukaa kabla ya kuanza, lakini hawa wananchi hawajalipwa fidia kwenye eneo ambako mradi unapita. Nataka kujua, ni lini hawa wananchi watalipwa fidia ili huu mradi uweze kuanza? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna mwananchi atakayeondolewa kabla hajalipwa fidia. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba sambamba na kuanza kujenga Serikali pia imeandaa fedha kwa ajili ya kuwalipa kabla hawajavunjiwa mali zao ama nyumba zao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya Haydom - Mbulu imeanza kujengwa; je, ni lini fidia italipwa kwa wananchi ambao wako katika maeneo ya Barabara ya Haydom - Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ilishakamilika na jedwali lilishapitishwa kwa maana ya uhakiki wote

ulishafanyika, tunachosubiri ni kupata fedha ili wananchi hawa waweze kulipwa kabla hatujaanza kuwaondoa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kamonga.

Na. 122

**Uwekezaji Mradi wa Liganga na Mchuchuma**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, baada ya Serikali kulipa eneo la Liganga na Mchuchuma lini uwekezaji unaanza?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha kulipa fidia ya eneo la Liganga na Mchuchuma ikiwa ni hatua muhimu ya utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Sichuan Hongda (Group) Company limited* ambaye ndiye alikuwa Mwekezaji wa mradi huo, ilitoa taarifa ya kwamba ipo katika hatua za mwisho za kuuza hisa zake katika Kampuni ya *Shudao Group* ya China.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hii ya Shudao *Group* ndiyo itakayotekeleza mradi huu muhimu baada ya taratibu za kuhamisha hisa kukamilika ndani ya miezi mitatu kuanzia Februari, 2025. Kwa hiyo, ni matarajio ya Serikali kuwa mradi huu utaanza kutekelezwa ndani ya mwaka wa fedha 2025/2026. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na niipongeze sana Serikali kwa kutatua mgogoro wa kimkataba kwa njia za kidiplomasia na leo tunasonga mbele.

pamoja na pongezi hizi nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; pale eneo la Liganga kuna mradi mdogo wa Maganga Matitu, kuna wananchi wachache walikuwa bado hawajalipwa fidia waliahidiwa hadi Januari hii watakuwa wamelipwa fidia. Je, ni lini fidia hizo zitalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo la pili; kule Nkomang'ombe kuna eneo dogo la makaa ya mawe Ketewaka nako kuna wananchi wachache walikuwa hawajalipwa fidia zao. Je, ni lini sasa Serikali hii iliyoweza kulipa bilioni 15 itawamalizia wananchi hawa ili waweze kufanya shughuli zao kwenye maeneo mengine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Kamonga kwa ufuatiliaji wa mradi huu na ni nimpe pongezi kwa sababu ameweka historia kati ya Wabunge ambao mradi huu sasa unatekelezwa ambao ulikuwa mradi wa kihistoria chini ya Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye anaweka naye historia kwa mradi huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna miradi hii mingine miwili ambayo inatekelezwa katika Jimbo la Ludewa ikiwemo huu wa Maganga Matitu ambao uko chini ya mwekezaji *Fujian Industry* Tanzania *Limited* ambaye kimsingi ndiye anatakiwa kulipa fidia na tayari tumeshakubaliana naye mpaka kufikia mwezi Machi awe amelipa fidia ambayo inafikia takribani bilioni 4.2. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ludewa katika eneo hili kwamba nao watalipwa fidia yao kama ambavyo tulipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kwenye eneo hili la Nkomang'ombe ambako kuna Mradi huo wa Ketewaka chini ya Mwekezaji *M.M. Steel* ambaye naye pia kama mwekezaji kutokana na makubaliano ya Serikali ndiye anayetakiwa kulipa

fidia. Tuko kwenye majadiliano naamini ndani ya mwaka huu wa fedha kwa maana ya mwaka 2024/2025 kufikia mwezi Juni atakuwa amelipa fidia ambayo inafikia takribani 2.1. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Awali ya yote na mimi naipongeza sana Serikali kwa hatua hii kubwa ambayo tumeisikia kwa mara ya kwanza ndani ya Bunge lako kwamba sasa mwekezaji atakayetekeleza mradi amepatikana na ndani ya miezi mitatu tutakuwa na huo uwekezaji.

Je, Serikali haioni haja ya kuwahusisha Watanzania kwenye uwekezaji huu mkubwa wa Liganga na Mchuchuma ili tutengeneze mabilionea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, lakini ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa sababu ndiye amekuwa pia anasimamia kuhakikisha mradi huu unakamilika na leo tunaona matunda haya chini ya Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja ya mikakati ya Serikali ni kuona namna gani Watanzania wazawa nao wanafaidika na mradi huu mkubwa wa kihistoria ambao ni wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkataba ule Serikali ina hisa kupitia Shirika la Maendeleo Tanzania *(NDC)* takribani 20% ambazo hizo ndiyo zitatumika kuwapa wazawa nafasi ya kushiriki aidha kwa kuuza hisa katika *Stock Exchange* au pia na wao

kuingia katika kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, watashiriki katika kutekeleza mradi huu muhimu kupitia hizo 20% ambazo zitaongezeka kadri tunavyokwenda kwa maana tumekubaliana ifike mpaka 49%. Kwa hiyo, Serikali ikinunua hizo hisa maana yake ni nafasi ya Watanzania kushiriki katika kutekeleza mradi huu muhimu wa kimkakati. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mwijage.

Na. 123

**Kutekeleza Miradi ya Maji – Muleba**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kutekeleza miradi ya maji katika Kata tano za Ziwani, Kata za Muleba Magharibi na Gwanseli – Kagoma?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Ziwa Wilayani Muleba lina jumla ya Kata tano za Goziba, Bumbire, Mazinga, Ikuza na Kerebe ambazo pamoja na kuwa ziwani zina tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kufanya usanifu wa kina wa miradi, *detailed design* na kutatua tatizo hilo. Aidha, Skimu ya Iroba, Kinagi, Goziba na Ikuza zinafanyiwa ukarabati katika mwaka huu wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa eneo la Muleba Magharibi lenye Kata za Kasharunga, Karambi, Kyebitembe, Mubunda, Burungura, Nyakatanga, Mushabago, Ngenge pamoja na Rutoro kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali itafanya upembuzi yakinifu wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria ili kuhudumia Kata hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia *program* za uchimbaji wa visima 900 Serikali tayari imechimba visima 14 na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma *(point source)* unaendelea. Utekelezaji wa kazi hizo unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2025 na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Gwanseli na Kagoma zinapata huduma ya maji kupitia Skimu ya Ilemela na Kagoma. Aidha, katika kuhakikisha Jimbo la Muleba Kaskazini linapata huduma ya maji ya uhakika, Serikali imekamilisha usanifu wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kwa ajili ya kuhudumia Kata sita za Gwanseli, Magata, Karutanga, Muleba, Bureza, Kikuku na Kagoma ambapo unatarajiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika eneo ambalo Serikali inaendelea kuchimba, wameshachimba 14 na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameanza kujenga vituo vya kutolea maji *point of service,* lakini kuna wadau *Christian Church of* Tanzania na Fimbo ya Musa *(The Orthodox)* wamechimba visima 16. Je, kwa nini sasa Serikali kwa usanifu mzuri na ujenzi ambao yenyewe inajenga visima vyake, isiwasaidie wadau hawa kusudi hii kazi nzuri ya Serikali ikaenea kwenye visima vyote?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika Mradi wa Kagoma Serikali imejenga tanki zuri nashukuru kwa hilo, lakini usambazaji wa maji haujafika katika Vijiji vya Nsisha, Kikuku na Bigaga. Ni lini Serikali sasa itapeleka neema hii nzuri kwenye vijiji hivyo kusudi watu wafaidi kazi ya Awamu ya Sita? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Charles Mwijage kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na Serikali ndani ya jimbo lake na kutambua Wizara ya Maji kuchimba visima 14 na *point sources* zinaendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali. Ni jukumu la Serikali na Sera yetu ya Maji kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wadau wote wanaotoa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika eneo ambalo wadau, iwe taasisi ya kidini, wananchi wenyewe wameweza kutoa huduma au wameweza kuchimba visima, lakini wameshindwa kuviendeleza, Serikali iko tayari kuendelea kushirikiana nao ili kuboresha visima hivyo ili viweze kutoa huduma ambayo inakusudiwa na wananchi, lakini maji yawe safi na salama kwa mujibu wa taratibu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza ni kuhusu Mradi wa Kagoma. Ni kweli Serikali tayari imewekeza fedha za kutosha katika ujenzi wa tenki lile. Katika bajeti ya mwaka uliopita tuliweza kujenga tenki lile, lakini hatukuwa na bajeti ya kujenga mtandao wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe katika Kamati yetu ya Maji na Mazingira, nimwombe, kupitia Bunge lako Tukufu, tutakapofikisha kwenye Kamati aweze kuwa sehemu ya kuhakikisha kwamba tunapitisha bajeti ambayo itatuwezesha kuongeza mtandao wa maji katika maeneo ya Vijiji vya Kikuku na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja ili wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jimbo la Mtwara Mjini bado linakabiliwa na upungufu wa maji. Je, ni lini Serikali itaamua kuyaleta maji kutoka Mto Ruvuma hadi katika Jimbo la Mtwara Mjini ili tuweze kupata maji kwa wingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mtenga kwa kazi kubwa anayoifanya pale Mtwara. Hakika amekuwa akitupatia ushirikiano mzuri sana na Serikali imeshaamua kuhakikisha kwamba tunakuwa na Gridi ya Taifa ya Maji kutoka kila *angle* ambapo tuna uwezo wa kupata chanzo cha maji cha uhakika na kwa sababu Mto Ruvuma ni chanzo cha uhakika, nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali tayari imekwishaamua na tumeshafanya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunatafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza mradi huo. Pesa zitakapopatikana Mheshimiwa Mbunge, mradi huo utaanza kutekelezwa kwa ajili ya wananchi wa Mtwara. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Jimbo la Bukoba Vijijini, Kata ya Lukoma, Kijiji cha Nsheshe, maji ni ya shida sana, napenda kujua ni lini Serikali itaenda kuwatua ndoo akinamama wa kijiji hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Oliver kwa kuendelea kuwapambania wananchi wa Kagera na kushirikiana na Wabunge wenzake wa majimbo. Vilevile, natambua changamoto ya eneo la Nsheshe ambalo amelitaja. Kwa kumbukumbu zangu kuna Mradi mmoja wa *World Vision* katika eneo lile unao-*serve* huduma ya maji pale katika eneo linaloitwa Karama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tumechimba visima ambavyo tunatarajia tukipata fedha tutafanya usanifu wa kwenda sasa kutengeneza mtandao wa maji ambao utaenda kuwafikia wananchi wote wa eneo husika. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan lengo lake kuu ni kumtua mama ndoo kichwani na kupata maji safi na salama, toshelevu na yenye gharama nafuu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari na Utamaduni, Mheshimiwa Shangazi.

Na. 124

**Fursa Zitakazopatikana kupitia Fainali za Mpira wa Miguu kwa Nchi za Afrika**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, fursa zipi zitapatikana kwa Mtanzania mmoja mmoja na vikundi kupitia Fainali za Mpira wa Miguu kwa Nchi za Afrika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa kushirikiana na Nchi za Kenya na Uganda imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya Mataifa ya Afrika Mwaka 2027 *(AFCON 2027);* ambapo kupitia mashindano haya fursa mbalimbali zitapatikana

zikiwemo ajira kupitia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo itakayotumika wakati wa mashindano hayo, uuzaji wa vifaa vya ujenzi, kuongezeka kwa mapato katika biashara mbalimbali kutokana na matumizi kwa wageni na wadau watakaoingia nchini kushuhudia mashindano, kuongezeka kwa mapato katika huduma za jamii kama vile hoteli, nyumba za kulala wageni, migahawa, usafirishaji na huduma nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, fainali hizi pia ni fursa kwa wachezaji wa Kitanzania kuonyesha vipaji vyao kwa mawakala wa vilabu vya kimataifa. Aidha, mashindano haya yatawezesha vikundi vya sanaa na utamaduni kujitangaza hivyo kutangaza utamaduni wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa sababu makundi ya kijamii aliyoyataja mengi bado hayajaunganishwa, kwa mfano eneo la usafirishaji, hapa tunazungumzia madereva wa tax, daladala na hata bodaboda. Je, Serikali ina andaa utaratibu gani ambao utatumika kuyashirikisha makundi haya ya jamii ili kufanikisha mashindano haya ya *AFCON* kwa kuzingatia diplomasia ya Uchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mashindano yenyewe haya ni ambayo yanahusisha mchezo wa mpira wa miguu na tunayo changamoto kubwa ya habari za mpira huwa zinapotoshwa potoshwa sana. Je, Serikali iko tayari sasa kuwapa mafunzo maalum na mahsusi Waandishi wa Habari za Michezo kwa ajili ya kuripoti mashindano haya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rashid Shangazi, mtu wa mpira kweli kweli, kwa

ufuatiliaji wake wa mara kwa mara kuhakikisha tunafanya vizuri wakati tukielekea kwenye uandaaji wa mashindano haya ya *AFCON* 2027 halikadhalika *CHAN* 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali iko tayari kukutana na makundi yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Na kwa kuonesha kwamba Serikali imedhamiria kweli kufanya hilo Januari 15 mwaka huu tulianza kwa kufanya kongamano na wadau wa michezo kuelekea *CHAN* 2024 na *AFCON* 2025 lililofanyika katika Hoteli ya Johari Rotana – Dar es Salaam na tuliongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Mashaka Biteko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kukutana na makundi mbalimbali na kukaa nayo kuyaelimisha, halikadhalika kuyatengenezea utaratibu ikiwemo utaratibu wa kuyatengenezea utambulisho maalum kama watoa huduma maalum wa mashindano haya ya *CHAN* 2024 na *AFCON* 2027. Makundi ninayoyataja yamo pia makundi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, ikiwemo mama lishe na maafisa usafirishaji. Kwa hiyo, itakuwa ni makundi halikadhalika mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili nilishawahi kujibu hapa. Nafikiri nilimjibu yeye Mheshimiwa Shangazi, kuhusiana na wachambuzi na aina ya uchambuzi wa mpira wa miguu ambao unafanyika kwenye nchi yetu. Serikali bado ina dhamira ya dhati kabisa ya kuhakikisha wachambuzi wetu wanapitia kozi japo fupi fupi kabla ya kukaa kwenye vyombo vya habari viwe ni redio ama televisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kwamba ndugu zangu/marafiki zangu wachambuzi hawapendi kulisikia jambo hili, lakini ni ukweli usiopingika kwamba hili linapaswa kufanywa kwa sababu liko kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016, Kifungu cha 19(1), kikishomwa pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2017. Kanuni ya 17(2)(a) vinataja kabisa aina ya watu wanaotakiwa kukaa kwenye vyombo vya Habari na vigezo

ambavyo wanatakiwa kuwa navyo kabla ya kuruhusiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili la kuwatengenezea utaratibu wa kuwapitisha kwenye kozi angalau fupi fupi kabla ya kuwaruhusu kukaa kwenye vyombo vya habari liko palepale. Kwa minajili ya jambo hili, tutawapitisha kwenye Chuo chetu cha Michezo Malya. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwenda tunaendelea, Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Malleko.

Na. 125

**Elimu ya Chanjo ya Wanyama**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utoaji chanjo dhidi ya magonjwa ya wanyama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetengeneza Kanuni ya Chanjo na Uchanjaji ambayo ilitolewa kupitia *GN* 180 ya Mwaka 2020. Aidha, katika kanuni hii inaelekeza kuwa uchanjaji wa mifugo ni wa lazima *(compulsory vaccination)*. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma ikiwemo kufanya uzinduzi wa uhamasishaji wa Kampeni ya Chanjo Kitaifa ambayo ilifanyika tarehe 18 -19 Desemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzinduzi huo ni sehemu ya mkakati ambayo ililenga kutoa elimu kwa wataalam kutoka Mamlaka ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Viongozi wa Vyama vya Wafugaji, Viongozi wa Vyama vya Kitaaluma na Wafugaji kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu Kampeni ya Chanjo

Kitaifa. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia makundi hayo itaendelea kuhamasisha kampeni hii na kutoa elimu nchi nzima. Ahsante

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya chanjo ili kudhibiti utumiaji holela au kupunguza utumiaji wa *anti-biotic?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kumekuwa na ongezeko kubwa sana la wanyama wanaozurura kama mbwa na paka hasa kwenye migahawa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti ongezeko hilo maana ni rahisi wanyama hawa kuwa na ugonjwa wa kimeta au *rabies* ambao unaweza kusababisha magonjwa na hatari kwa binadamu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la kwanza juu ya matumizi ya *antibiotic;* tayari Serikali imeshatoa maelekezo mbalimbali kupitia Maafisa Ugani wanaopatikana katika maeneo mbalimbali katika vijiji vyetu. Sasa hivi cha kwanza kabisa ambacho tunakifanya ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa matumizi sahihi ya *anti-biotic* zinazopatikana katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wafugaji popote walipo wanafahamu namna sahihi ya matumizi ya *anti-biotic* na wale ambao hawana huo ufahamu basi tumekuwa tukiwaelimisha na kuwaelekeza mahali sahihi; kwenda kujifunza kwa Maafisa Ugani ili waweze kutumia *anti-biotic* kwa mujibu wa utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo tu kwa mifugo bali pia kwa binadamu. Kwamba huwezi kutumia *antibiotic* ama dawa yoyote

ambapo daktari wa mifugo au wa binadamu bado hajathibitisha matumizi hayo. Tunaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji wote kwenda kwa Maafisa Ugani ili waweze kupata utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili la pili, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, baadhi ya maeneo hasa maeneo ya Kaskazini ongezeko la mifugo kama mbwa limekuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali tumeshatoa maelekezo kwa Maafisa Ugani na Serikali katika maeneo hayo kuchukua hatua dhidi ya mifugo yote isiyokuwa na wenyewe, hasa aina ya mbwa; mbwa akizurura mtaani kwako na hana mwenyewe na Serikali za mitaa zikajiridhisha kwamba mbwa huyu hana pa kwenda na pengine ameshapata maambukizi ya kichaa cha mbwa, hatua stahiki ambazo tumekwishawaelekeza ni pamoja na kuwaondoa Duniani ili mbwa hao wasilete madhara kwa binadamu, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Minza Simon, kwa niaba.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa naomba swali lake Namba 126 lipate majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini na kwanza ni utovu wa nidhamu, *no no no,* Mheshimiwa Hokororo.

Na. 126

**Uhitaji wa Gari la Zimamoto – Simiyu**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua magari ya Zimamoto kwa ajili ya Wilaya za Mkoa wa Simiyu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatekeleza mradi wa ununuzi wa magari 150 pamoja na vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka kampuni ya *NAFFCO FZCO (National Fire Fighting Manufacturing Company Free Zone Company)* iliyopo Dubai. Pindi magari yatakapowasili nchini, yatasambazwa nchi nzima ikiwemo wilaya za Mkoa wa Simiyu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa majibu yake ya msingi amesema magari hayo yatasambazwa nchini kote, tunataka kujua ni lini hasa magari hayo yatasambazwa, ikiwemo Mkoa wa Mtwara na Wilaya zake Masasi, Newala, Nanyumbu na Tandahimba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, magari haya yatawasili hapa nchini kwa awamu nne, awamu ya kwanza itaanza mwezi Aprili mwaka huu na kuendelea. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba magari haya yatasambaa maeneo yote aliyoyataja ikiwemo pia Mkoa wa Mtwara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

Na. 127

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi Tarafa za Daudi na Nambis - Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga vituo vya Polisi Tarafa za Daudi na Nambis Wilayani Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imetenga eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 2023 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja C sehemu ya Chamulinga, Kata ya Daudi. Ujenzi wa kituo umepangwa kutekelezwa kwenye awamu ya pili ya mpango wa ujenzi wa vituo vya polisi vya kata unaoshirikisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Tarafa ya Nambis hakuna eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi vya kata. Ninaomba kutumia fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri ya Mbulu kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Kata kwenye Tarafa ya Nambis. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Mbulu ni chakavu na kilijengwa muda mrefu miaka ya zamani. Je, Serikali ina mkakati gani wa ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Mbulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa makazi ya polisi katika Wilaya ya Mbulu yamechakaa sana hadi sasa. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kukarabati makazi ya polisi nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issaay, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Wizara kupitia Jeshi la Polisi itafanya tathmini ya uchakavu wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbulu pamoja na makazi ya askari ili kujua gharama inayohitajika na hatimaye kupanga kwenye mpango na kupangia bajeti tayari kwa ajili ya ukarabati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo ya wageni. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kaka yake kutoka Halmashauri ya Kisarawe, Mkoani Pwani, karibu. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Katibu Mstaafu wa CCM, Wilaya ya Singida Vijijini. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Ludewa, Mkoa wa Njombe. Wageni wengine saba wa Mheshimiwa Kamonga ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* wanaotokea Ludewa Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Vilevile, tunao wageni wa Mheshimiwa Stephen Byabato ambao ni wanafunzi 150 na Walimu sita wa Shule ya Sekondari ya

Wasichana Josiah kutoka Wilaya ya Bukoba Mjini, Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Anatropia Theonest pamoja na wazazi wa wanafunzi wanaosoma Shule ya *Anglo Junior* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, viongozi 30 wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(DARUSO)*. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba taarifa nzima iingie kwenye Kumbukumbu za Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136, Kanuni Ndogo ya 15 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Taarifa hii

inahusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara zifuatazo:-

(i) Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(ii) Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji;

(iii) Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano;

(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge, Sera na Uratibu na;

(v) Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati kwa Wizara inazozisimamia ni kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo na zile zinazoletwa chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo na taasisi zake; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya taarifa yetu inahusu shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa masuala yaliyobainika. Kwanza ni uchambuzi wa Miswada ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la utungaji wa Sheria za Nchi limeainishwa kwenye Ibara ya 64 ya Katiba, ambapo Bunge limepewa madaraka ya kutunga sheria za Tanzania Bara katika Ibara ya 64(1) na Sheria za Muungano katika Ibara ya 64(4). Aidha, Ibara ya 79 inaweka utaratibu kwamba, Bunge litatumia madaraka hayo kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria kabla ya kibali cha Rais ili kuwa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo na kwa kuzingatia Kanuni ya 79, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilijadili Miswada sita ambayo ni: -

(i) Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali minne;

(ii) Miswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, 2024;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya kina kuhusu uchambuzi wa maudhui ya Miswada hiyo ya sheria yanapatikana katika taarifa husika zilizowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Mei, 2024, Kamati ilipokea maelekezo toka ofisi yako kufanyia kazi mkanganyiko wa kisheria unaojitokeza katika tafsiri ya kifungu cha 80(2) cha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263. Kamati ilitekeleza jukumu hilo na ilikutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ambapo alikubali uwepo wa changamoto hiyo ya kisheria katika sheria hiyo na sheria nyingine zipatazo nne ambazo zilibainika kuweka masharti kuhusiana na rufaa ya maamuzi ya kiutawala kwenda Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutatua changamoto kwenye sheria zote nchini zenye changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika ili Kamati iwe katika nafasi nzuri zaidi ya kuzishauri Wizara inazozisimamia katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara hizo za ukaguzi zilifanyika katika mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma na Dodoma kati ya tarehe 11 – 17 Machi, 2024. Maelezo ya kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika katika ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo yanapatikana katika taarifa za Kamati zenye maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kila Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa isipokuwa kwa miradi michache ambayo Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo mahususi katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni. Miongoni mwa masuala ambayo yalibainika katika baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutokuwa na utamaduni wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati mdogo wa mara kwa mara kwa maana ya *regular maintenance* wa miradi ya ujenzi. Kwa sababu hiyo, miradi hiyo ambayo inatumia fedha nyingi za umma, huanza kupoteza ubora wake na kuchakaa katika muda mfupi;

(b) Miradi mingi inayotekelezwa kuwa ni ya muda mfupi na hivyo kutokuwa na tija kwa jamii husika; na

(c) Changamoto ya miradi kutokukamilika kwa wakati hali ambayo huchangiwa na ucheleweshwaji wa malipo kwa wakandarasi au kutosimamiwa vizuri kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 2(3) inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa za utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge katika mchakato wa bajeti kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kikamilifu masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge kwa kufanya ulinganifu baina ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha uliofuata. Aidha, Kamati iliangalia mwenendo wa makusanyo ya maduhuli na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kupima ufanisi wa utekekelezaji wa bajeti husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu uchambuzi wa bajeti za kila Wizara husika pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa kwa nyakati tofauti katika Mkutano Mkuu wa Pamoja wa Bajeti uliofanyika Mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake. Kwa nyakati tofauti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake. Msingi wa shughuli hii umejengwa katika

utekelezaji wa Madaraka ya Bunge kama chombo kikuu kwa niaba ya wananchi cha kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka mmoja Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za taasisi zifuatazo:-

(a) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake zote ambazo zimeainishwa kwenye taarifa iliyoingia kwenye kumbukumbu zako za Bunge;

(b) Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zake zote;

(c) Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano;

(d) Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na taasisi zake na;

(e) Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake zote zilizo chini ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya taarifa yetu inahusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Wizara inazosimamia. Kamati ilipokea taarifa za Wizara na taasisi inazosimamia kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yalitokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ya Februari, 2024 hadi Januari, 2025 iliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Maazimio ya Bunge uliofanywa na Wizara inazozisimamia na taasisi zilizopo chini yake. Kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo zaidi katika utekelezaji wake, Kamati imetoa ushauri mahususi kwa kila Wizara na taasisi

zake ili yakafanyiwe kazi zaidi ili kuboresha ustawi wa wananchi wa Tanzania na kukidhi matarajio yao kwa kufuata misingi iliyowekwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Aidha, kwa maazimio ambayo utekelezaji wake haujakamilika, Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kutekeleza maazimio hayo kama ilivyoazimiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika Wizara hii, Bunge liliazimia maazimio sita kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati iliyoingia kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa sehemu kubwa ya maazimio haya yametekelezwa kikamilifu na Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya wenye ulemavu katika mchakato wa usaili wa ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Katika Wizara hii, Bunge liliazimia maazimio matano kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati iliyoingia kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inapenda kukujulisha kuwa sehemu kubwa ya maazimio kwenye Wizara hii yametekelezwa kikamilifu isipokuwa kwenye azimio moja la uanzishwaji wa divisheni maalum ya Mahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa Mahakama Kuu divisheni ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi inajitosheleza katika kuamua mashauri yanayohusu dawa za kulevya nchini na mamlaka imeendelea kutoa mafunzo kwa waendesha mashtaka nchini wapatao 490.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria. Katika Wizara hii, Bunge liliazimia maazimio sita kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati iliyoingia kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Serikali imetekeleza maazimio kwa asilimia kubwa hasa kwenye ujenzi na ukarabati wa majengo ya

Mahakama isipokuwa kwa maeneo machache kama matumizi ya TEHAMA kwenye Mahakama za Mwanzo ambapo Kamati ilielezwa kwamba ukarabati wa majengo na miundombinu wezeshi ya TEHAMA ya Mahakama za Mwanzo utakapokamilika Mahakama hizi zitaanza kutumia mfumo wa usajili na kuratibu mashauri unaoujulikana kama *GOT e-case management system.*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati yamebainishwa kwenye taarifa ya Kamati iliyoingia kwenye kumbukumbu zako za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya taarifa yetu inahusu maoni na mapendekezo. Kwanza ni maoni ya jumla. Sehemu hii inabainisha mtazamo na maoni ya jumla ya Kamati yanayotokana na shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 na kuonesha maoni ya jumla kwa kila Wizara inayosimamiwa na Kamati. Aidha, maoni hayo yanalenga kujenga msingi wa hoja ya Kamati kuhusu mambo ya kufanyiwa kazi iwapo Bunge lako Tukufu litaridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora. Katika kuisimamia Wizara hii Kamati ilipitisha bajeti ya Wizara hii na kutembelea miradi ambayo ilitengewa bajeti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kujadili masuala mbalimbali ikiwemo kupata taarifa za utendaji kazi za Wizara hii na taasisi zilizo chini yake kwa kipindi cha Aprili 2024/2025. Kamati imebaini suala la upungufu wa rasilimali fedha na watu kwenye baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara hii, jambo ambalo linaleta ugumu kwa taasisi hizo kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba taarifa hii tayari ipo Mezani kwako na kwa maslahi ya muda

ninaomba uniruhusu niende moja kwa moja kwenye Maazimio ya Kamati ili kuweza kutoa mapendekezo kwa Bunge lako Tukufu juu ya maamuzi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia mapendekezo ya Kamati na kwenye kumbukumbu zako za Mezani ni 4.2.1 inayohusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa rasilimali watu na fedha kwenye Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini:

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa fedha, wataalamu na vitendeakazi kwenye Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU);

Na kwa kuwa, changamoto hiyo inapelekea taasisi hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iongeze bajeti kwa taasisi itakayoiwezesha taasisi hiyo kuajiri watumishi, kujenga ofisi hadi ngazi za wilaya na kununua vitendeakazi vitakavyoiwezesha kutekeleza majukumu yake kiufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Miradi ya *TASAF* nchini:

Kwa kuwa, Kamati imebaini kutokuwepo kwa miradi endelevu inayotekelezwa na *TASAF*, uelewa mdogo wa wananchi juu ya wanaostahili kuwa wanufaika wa *TASAF* na kuwepo na upungufu wa watumishi wa *TASAF* katika ngazi za wilaya nchini;

Na kwa kuwa, changamoto hizi zinapelekea baadhi ya miradi inayotekelezwa kuwa siyo ya kuendeleza jamii nzima na kuisaidia kiujumla kujikwamua kiuchumi ili kuondokana na kuwa tegemezi kwa Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ifanye jitihada za kutekeleza miradi ya *TASAF* ambayo ina tija zaidi na manufaa kwa wananchi na ambayo itawezesha wananchi kujiajiri kupitia miradi hiyo na hivyo kukuza kipato kwa wananchi.

(ii) Serikali ikishirikiana na viongozi wa ngazi zote nchini itoe elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya malengo ya miradi ya *TASAF* kuhusu sifa na vigezo vya wanaostahili kuwa wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfumo wa Kupima Utendaji kazi kwa Watumishi ambao unajulikana kama *PEPMIS* ambao kwa sasa unatumika kama *e-Utendaji* kwa watumishi waliopo maeneo ya vijijni:

Kwa kuwa, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya mtandao na vitendeakazi vinavyowezesha watumishi kujaza utekelezaji wa majukumu yao kwenye mfumo wa kupima utendaji kazi kwa watumishi ambao wanaishi maeneo ya vijijini;

Na kwa kuwa, changamoto hiyo husababisha baadhi yao kushindwa kujaza taarifa za utekelezaji wa majukumu yao katika mfumo huo kwa wakati na hivyo wengine kushindwa kufikisha asilimia zinazotakiwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Matumizi ya Mfumo wa Kupima Utendaji kazi kwa watumishi yaendane na utoaji wa vitendeakazi na kuboresha mtandao katika maeneo ya vijijini ili kuwawezesha watumishii kujaza taarifa za utendaji kazi wao kwa ufanisi;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa *PEPMIS* na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza kwa kipindi cha mwaka mmoja toka ilipoanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumebainika kuwepo kwa mifumo mingi ya TEHAMA inayotokana na mchakato wa kuinua vipaji kwenye Sekta ya TEHAMA.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa mifumo 18 iliyoibuliwa na vijana kupitia Programu ya Kukuza Vipaji vya TEHAMA zinazotekelezwa na Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao *(e-Government Research Innovation and Development Center)*;

Na kwa kuwa, mifumo hiyo inaonekana kuwa na mlengo unaofanana na kutotumika na taasisi nyingi za Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali kupitia Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao, itatangaza bunifu hizo zinazofanywa na vijana wa Kitanzania na kuzitafutia masoko ya ndani na nje;

(ii) Serikali iratibu mchakato wa kuunganisha mifumo hiyo na kuwa mfumo mmoja;

(iii) Serikali ihakikishe inapeleka mtandao maeneo ya vijijini ili kuwezesha watumishi wa umma waliopo maeneo hayo wautumie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya maoni ya Kamati ya Maazimio ya Bunge, yanajielekeza kwenye Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

(a) Imebainika kuwa ofisi hii ina changamoto ya kuwa na mfumo mmoja wa kutoa leseni na ulipaji wa kodi kwa wawekezaji nchini.

Kwa kuwa, Kamati imebaini uwepo wa masharti ya leseni nyingi zinazotolewa na Mamlaka tofauti tofauti za Serikali nchini kwa wawekezaji na wafanyabiashara;

Na kwa kuwa, masharti hayo yanaweza kuchukuliwa kama usumbufu na hivyo kupunguza kasi ya wawekezaji kuja nchini na kuwekeza;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iratibu utengenezwaji wa mfumo wa pamoja wa ulipaji kodi, mfumo wa kodi unaosomana kwa wawekezaji na wafanyabiashara nchini;

(ii) Kuwepo kwa mfumo mmoja wa utoaji leseni za biashara nchini kwa wawekezaji wazawa na wa kigeni ambao wataratibiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania; na

(iii) Serikali kupitia tovuti ya Kituo cha Uwekezaji ibainishe aina ya leseni zote mwekezaji anatakiwa kuwa nazo kwenye sekta tofauti za uwekezaji nchini na namna ambavyo ataweza kuzipata.

(a) Vituo Jumuishi vya Uwekezaji kutokuwa na watumishi wenye mamlaka ya kutoa maamuzi.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba watumishi wengi ambao wanafanya kazi katika Vituo Jumuishi vya Uwekezaji nchini kuwa hawana mamlaka ya kutoa maamuzi kwenye baadhi ya mambo yanayohitaji uharaka;

Na kwa kuwa, changamoto hiyo inasababisha kukwamisha baadhi ya taratibu za usajili na kuwahudumia wawekezaji nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kwamba watumishi wanaowekwa katika Vituo Jumuishi vya Uwekezaji kwa maana *One Stop Center*, wana uwezo na mamlaka ya kutoa maamuzi ili kukuza na kuboresha utoaji huduma kwa wekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi inayofuata ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. Changamoto ambayo ilibainika ni moja, ambayo ni kutokuwepo majengo ya kudumu kwa baadhi ya taasisi za Muungano upande wa Zanzibar.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kutokuwepo kwa majengo ya kudumu kwa taasisi za Muungano upande wa Zanzibar,

Na kwa kuwa, changamoto hiyo inasababisha Serikali kuingia gharama ya kulipa kodi za kukodi ofisi kwa upande wa Zanzibar,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe ujenzi wa ofisi na majengo ya kudumu kwa upande wa Zanzibar ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi inayofuata, ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Moja ya changamoto zilizobainika kwenye ofisi hii ni ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya zenye kemikali bashirifu nchini.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba kwa mwaka 2023, Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini ilifanikiwa kuzuia uingizaji nchini wa kemikali bashirifu kilogramu 1,057,738.55 na kukamatwa jumla ya kemikali bashirifu zenye ujazo wa lita 22,682 kwa kipindi cha Januari – Septemba, 2024,

Na kwa kuwa, changamoto ya ongezeko la matumizi ya kemikali hizi bashirifu *(NPS)*, zina viwango vikubwa vya kulevya mara 50 – 100 ukilinganisha na dawa za kulevya zinazodhibitiwa Kimataifa na kusababisha matatizo makubwa ya afya na athari za magonjwa mbalimbali ikiwemo utegemezi na uraibu usioponyeka kirahisi, magonjwa ya akili, moyo, mfadhaiko, kifafa na vifo vya ghafla kwa watumiaji,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe elimu inatolewa kuhusu uwepo wa aina mpya ya dawa za kulevya *(NPS)* na madhara ya kemikali hizo kwa jamii;

(b) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, ishirikiane na Taasisi ya Mamlaka ya Dawa na

Vifaatiba *(TMDA)*, Shirika la Viwango *(TBS)* na Bohari ya Dawa Tanzania *(MSD)* kudhibiti maduka ya dawa za binadamu kujihusisha na uuzwaji wa kemikali bashirifu nchini;

(c) Serikali iongeze bajeti ya mamlaka ili iweze kujenga vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kulevya hadi ngazi za mikoa;

(d) Kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa kwa maana ya *cargo scanners* katika sehemu za usafirishaji na upakiaji wa mizigo nchini;

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili katika ofisi hii, inahusu urejeshwaji wa miundombinu kwa maeneo yaliyokumbwa na maafa nchini.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa kumekuwa na changamoto ya urejeshwaji wa miundombinu kwenye maeneo yaliyokumbwa na maafa nchini;

Na kwa kuwa, changamoto hiyo husababisha wananchi kukosa huduma za msingi ikiwemo umeme, maji, barabara kwa muda mrefu,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa, Serikali irejeshe huduma muhimu za kijamii kwenye maeneo yaliyokumbwa na maafa hayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, malizia, nenda kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, malizia.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uridhie kwamba sehemu ya maazimio iliyobaki, iingie moja kwa moja kwenye kumbukumbu zako za Bunge kwa ofisi zote ambazo zinasimamiwa na Kamati yetu ya

Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria, na uridhie nihitimishe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nakupongeza kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu vizuri. Pia shukrani ziende kwa Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge, kwa ushirikiano anaonipatia pamoja na Kamati kwa ujumla. Kipekee zaidi nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa ushirikiano wao wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii. Kwa heshima kubwa, naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu zako za Kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru viongozi na watendaji wote wa Mhimili wa Utendaji kwa maana ya Serikali na Mhimili wa Mahakama *(The Judiciary)* kwa ushirikiano waliotupatia Kamati. Kwa ajili ya muda naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu zako za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee Kamati inatoa pole kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kuondokewa na aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume hiyo ya Mipango, Ndugu Lawrence Mafuru aliyefariki akipatiwa matibabu nchini India. Bwana alitoa, Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe,

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard. Kwa kipekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa kwa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**

1.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Taarifa hii inahusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambapo pamoja na masuala mengine, inaelezea kwa muhtasari kuhusu muundo na majukumu ya Kamati, pamoja na kuainisha mbinu zilizotumika kutekekeleza majukumu hayo.

b) Sehemu ya Pili inabainisha majukumu/shughuli zilizotekelezwa na kutoa ufafanuzi wa uchambuzi kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika.
c) Sehemu ya Tatu inahusu utekelezaji wa Maazimio ya
d) Bunge yaliotolewa kwenye Mkutano wa Kumi
e) Sehemu ya Nne ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na
f) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

1.2 **Muundo na Majukumu ya Kamati**
**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo imeundwa chini ya Kifungu cha 5(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni, Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zifuatazo:-

a) Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
b) Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji;
c) Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano;
d) Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge; na
e) Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati za Kisekta yameainishwa katika Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwa msingi huo Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya
c) Wizara inazozisimamia;
d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
e) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

### 1.3 Njia na Mbinu Zilizotumika Kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Majukumu hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 136 (3) na (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kutumia mbinu na njia zifuatazo: -

a) Kufanya vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za wizara na taasisi zake kwa lengo la kufahamu utendaji wa majukumu, mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo;

b) Kuchambua na kujadili miswada ya sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu miswada hiyo;

c) Kufanya ziara za mafunzo katika taasisi na maeneo mbalimbali ya kisekta kwa lengo la kuona na kujifunza namna ambavyo taasisi hizo zinatekeleza majukumu yake;

d) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kujiridhisha kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji na ufanisi wa miradi hiyo; na

e) Kupokea semina na mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujenga uelewa wa masuala mahsusi yanayotekelezwa na Wizara na taasisi zake, pamoja na wadau wengine.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MASUALA YALIYOBAINIKA

2.1 **Uchambuzi wa Miswada ya Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Jukumu la utungaji wa Sheria za Nchi limeainishwa kwenye Ibara ya 64 ya Katiba, ambapo Bunge limepewa madaraka ya kutunga sheria za Tanzania Bara katika Ibara ya 64(1) na Sheria za kimuungano katika Ibara ya 64(4). Aidha, Ibara ya 97 inaweka utaratibu kwamba, Bunge litatumia madaraka hayo kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria kabla ya kibali cha Rais ili kuwa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo na kwa kuzingatia Kanuni ya 97, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilijadili Miswada ya Sheria sita (6). Miswada hiyo ni: -

a) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, 2024;**

b) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024** [***The Wiritten Laws (Miscelaneous Amendment) Bill, 2024***]; ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

   (i) Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388.

   (ii) Sheria ya Madini Tanzania Sura ya 123.

   (iii) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280;

c) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024**;

d) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 [*The Wiritten Laws (Miscelaneous Amendment) (No.2) Bill, 2024*]**

(i) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432
(ii) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;
(iii) Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273;
(iv) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54;
(v) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
(vi) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70
(vii) Sheria ya Viwango, Sura ya 130 na
(viii) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127

e) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Namba 3) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]*** ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha haramu, Sura ya 423
(ii) Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211
(iii) Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201
(iv) Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386
(v) Sheria Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435
(vi) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418
(vii) Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha haramu, Sura ya 423
(viii) Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211
(ix) Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201
(x) Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386
(xi) Sheria Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435
(xii) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418

f) **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Namba 4) wa Mwaka 2024 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]** ambao ulikuwa unafanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya mwakili, Sura ya 341,

(ii) Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura ya 3,
(iii) Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291,
(iv) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54,
(v) Sheria ya Shirika la Soko la kariakoo, Sura ya 132,
(vi) Sheria Ya ardhi, Sura ya 113,
(vii) Sheria ya Madini, Sura 123; na
(viii) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya kina kuhusu uchambuzi wa maudhui ya Miswada hiyo ya sheria yanapatikana katika taarifa husika zilizowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, 28 Mei 2024 Kamati ilipokea maelekezo toka ofisi yako kufanyia kazi mkanganyiko wa kisheria unaojitokeza katika tafsiri ya kifungu cha 80(2) cha sheria ya Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi sura ya 263.

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilitekeleza jukumu hilo na ilikutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Ajira na watu wenye ulemavu ambaye alikubali uwepo wa changamoto hiyo ya kisheria katika sheria hiyo na Sheria nyingine zipatazo 41 ambazo zilibainika kuweka masharti kuhusiana na rufaa ya maamuzi ya kiutawala kwenda mahakama kuu ya Tanzania.Aidha Wizara iliahidi kushirikiana na ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali kutatua changamoto kwenye sheria zote nchini zenye changamoto hiyo**.**

### 2.2 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika ili Kamati iwe katika nafasi nzuri zaidi ya kuzishauri Wizara inazozisimamia katika Bajeti ya

Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ziara hizo za ukaguzi zilifanyika katika mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma na Dodoma kati ya tarehe 11 – 17 Machi, 2024 ambapo miradi ifuatayo ilitembelewa: -

a) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TAKUKURU Iringa, (Mradi Namba 6203)

b) Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mahenge Kilolo (Mradi Namba 6312)

c) Uwasilishaji wa Ruzuku kwa kaya maskini na miradi ya Jamii ya kutoa ajira ya muda-Uanzishwaji wa Shamba la Parachichi – Ekari 3, Ibumila Iringa-DC (Mradi Namba 6220)

d) Kituo Jumuishi cha utoaji haki, Njombe (Mradi Namba 6215)

e) Ujenzi wa Wodi ya Mama na mtoto-Hospitali ya Kibena-Njombe TC (Mradi Namba 6220)

f) Ujenzi wa kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Songea (Mradi Namba 6215)

g) Uwasilishaji wa Ruzuku kwa kaya maskini na Utekelezaji wa miradi ya Jamii ya kutoa ajira ya muda-Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Kijiji cha Lundusi-Songea DC **(Mradi Namba 6220**);

h) Uwasilishaji wa Ruzuku kwa kaya maskini na Utekelezaji wa miradi ya Jamii ya kutoa ajira ya muda-Ujenzi wa Soko la kisasa Madaba -Songea DC (Mradi Namba 6220);

i) Mfumo mpya wa kieletroni wa Taarifa za kiutumishi na malipo ya mishahara (home grown HCMIC) (Mradi Namba 6282);

j) Mfumo wa kieletroniki wa kushughulikia Rufaa na malalamiko na Ukaguzi wa uzingatiaji wa usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma (Mradi Namba 4246); na

k) Uboreshaji wa Utendaji Kazi wa Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa Umma kwa kutumia TEHAMA (Modernization of PSRS Business processes through IT), (Mradi Namba 6225.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika katika ziara za ukaguzi wa miradi hiyo, yanapatikana katika Taarifa za Kamati zenye maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kila Wizara husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa isipokuwa kwa miradi michache ambayo Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo mahsusi katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masuala ambayo yalibainika katika baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo;

a) Kutokuwa na utamaduni wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati mdogo wa mara kwa mara *(regular maintenance)* wa miradi ya ujenzi. Kwa sababu hiyo, miradi hiyo ambayo inatumia fedha nyingi za umma, huanza kupoteza ubora wake na kuchakaa katika muda mfupi.

b) Miradi mingi inayotekelezwa kuwa ni ya muda mfupi na hivyo kutokuwa na tija kwa jamii husika.

c) Changamoto ya miradi kutokukamilika kwa wakati hali ambayo huchangiwa na ucheleweshwaji wa malipo kwa wakandarasi au kutosimamiwa vizuri na wasimamizi wa miradi hiyo.

2.3 **Uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Bajeti ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Madaraka ya Bunge katika Mchakato wa Bajeti *(the budget cycle)* kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kikamilifu masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge kwa kufanya ulinganisho baina ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Aidha, Kamati iliangalia mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kupima ufanisi wa utekekelezaji wa bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge hili kupata picha ya masuala yaliyobainika katika uchambuzi wa Bajeti ya Serikali 2023/2024, ufuatao ni muhtasari wenye kuonyesha mwenendo wa Bajeti ya Wizara/Taasisi zinazosimamiwa na Kamati: -

**<u>Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora</u>**

a) Kwa upande wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

(i) Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliongezeka kwa wastani wa **asilimia 13.52** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili liliakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili

kuboresha ufanisi wa utendaji wake na kuhakikisha kwamba bajeti ya ofisi inaakisi mahitaji ya kifedha na hali ya uchumi.

(ii) Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Bajeti ya Ofisi hiyo imepungua kwa **asilimia 31.3** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ilibaini kwamba upungufu huo wa bajeti umechangiwa na ukomo wa Bajeti ya Serikali.

**Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji**

b) Kwa upande wa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

(i) Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliongezeka kwa wastani wa **asilimia 9.26** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili liliakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake na kuendana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bidhaa na huduma.

(ii) Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Bajeti ya Ofisi hiyo imepungua kwa **asilimia 31.3** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ilibaini kwamba upungufu huo umechangiwa na ukomo wa Bajeti ya Serikali. **Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)**

c) Katika bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Katika Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 bajeti iliongezeka kwa **asilimia 16.07** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili ni matokeo ya ushauri uliotolewa na Kamati ili kuwezesha Ofisi hiyo na taasisi zake ziwe na fedha ya kutosha kutekeleza majukumu yake.

(ii) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilibaini kwamba fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pungufu kwa **asilimia 65.03** ukilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu ya upungufu wa bajeti ya maendeleo ni kutokana na kutokuwepo kwa mradi mpya unaotekelezwa na Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi hii inaomba fedha za ukamilishaji wa mradi wa ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dodoma, Dar es salaam na Pemba ulioanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**<u>Ofisi ya Waziri Mkuu</u>**

d) Katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake, Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Kwa ujumla wake, hali ya upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu haukuwa wa kuridhisha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ukilinganisha na mwaka wa fedha ulioisha wa 2022/2023.Hadi wakati taarifa ya Kamati inawasilishwa Bungeni, Ofisi hiyo na Taasisi zake zilipokea wastani wa **asilimia 56.31** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliongezeka kwa **asilimia 20.7** ukilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/2024. Moja kati ya sababu ya ongezeko hilo ilikuwa ni utekelezaji wa maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi.

(iii) Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Bajeti ya Ofisi hiyo iliongezeka kwa **asilimia 1,097.7** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ilibaini kwamba ongezekeo la bajeti ilitokana na kuanzishwa kwa ofisi ya Naibu Waziri Mkuu katika Wiaxra hiyo na matumizi katika uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga Kura na maandalizi ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(i) Serikali ihakikishe kwamba, fedha zinapatikana kikamilifu kwenye Mradi Na.4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

(ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na idara zilizoko chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

(iii) Serikali ihakikishe kwamba ununuzi wa mashine za uchapaji pamoja na matengenezo ya mashine uchakavu unakamilika kwa wakati kabla ya kuanza kwa maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2024 na uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

**<u>Wizara ya Katiba na Sheria</u>**

e) Kwa upande wa Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

(i) Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliongezeka kwa wastani wa **asilimia 25** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili liliakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake.

(ii) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilibaini kwamba fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pungufu kwa **asilimia 30.73** ukilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Sababu ya kupungua huku kunatokana na ukomo wa bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu Uchambuzi wa Bajeti za kila Wizara husika, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa kwa nyakati tofauti katika Mkutano wa Kumi na moja wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2024.

### 2.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake

**Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Msingi wa shughuli hii umejengwa katika utekelezaji wa Madaraka ya Bunge kama chombo kikuu kwa niaba ya wananchi cha kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwaka mmoja Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa za taasisi zifuatazo:

**a) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

(i) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).
(ii) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
(iii) Taasisi ya Uongozi.
(iv) Wakala wa Ndege za Serikali.
(v) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)
(vi) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.
(vii) Tume ya Utumishi wa Umma.
(viii) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).
(ix) Watumishi Housing Investment (WHI).
(x) Sekretarieti ya Ajira.
(xi) Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

**b) Ofisi ya Rais –Mipango na Uwekezaji.**

(i) Ofisi ya Msajili wa Hazina.
(ii) Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).
(iii) Mamlaka ya Eneo Huru la Uwekezaji (EPZA).

**c) Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu**

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi.
(ii) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).
(iii) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.
(iv) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

**d) Wizara ya Katiba na Sheria**

(i) Tume ya Utumishi wa Mahakama.
(ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
(iii) Ofisi ya Taifa ya Mashitaka.
(iv) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.
(v) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA)
(vi) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
(vii) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.
(viii) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania.
(ix) Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KATIKA WIZARA ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika Vikao vya Kamati za Bunge vilivyofanyika kuanzia tarehe 13 – 25 Januari, 2025, Kamati ilipokea Taarifa za Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Maazimio hayo yalitokana na Taarifa za Mwaka Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria za Februari, 2024 hadi Januari, 2025 zilizowasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sehemu kubwa, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maazimio ya Bunge uliofanywa na Wizara

inazozisimamia na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo. Kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo zaidi katika utekelezaji wake, Kamati imetoa ushauri mahsusi kwa kila Wizara na taasisi zake ili yakafanyiwe kazi zaidi ili kuboresha ustawi wa wananchi wa Tanzania na kukidhi matarajio yao kwa kufuata misingi iliyowekwa kwenye ilani ya Uchaguzi ya chama cha Mapinduzi (CCM).

**Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**
**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako tukufu liliazimia mambo yafuatayo kwenye Wizara hii;

(i) Utekelezaji wa Miundombinu na taratibu za kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki katika mchakao wa usaili wa ajira.

(ii) Serikali ifanye jitihada za kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu za tamaduni Viongozi wa Jadai na kuhifadhi taarifa hizo kidigitali na ihakikishe kwamba inafanya kampeni maaluum ya kuhamasisha Wananchi kuenzi utamaduni, historia na mchango wa waasisi wa Taifa letu.

(iii) Mifumo ya upandishaji vyeo na mabadiliko ya kimuundo kwa Watumishi iboreshwe ili iende sambamba na mabadiliko ya mishahara

(iv) Serikali ione umuhimu wa kufanya ununuzi wa ndege zingine ili kuboresha utoaji huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

(v) Serikali ikamilishe Sera ya Taifa ya TEHAMA Serikalini na kufanya tathmini ya mifumo yote ndani ya Serikali na kubaini mifumo yote ambayo haina tija kwa Serikali na kuchukua hatua madhubuti za kuiondoa

(vi) Serikali ihakikishe kwamba kunakuwa na muunganiko wa mifumo ya Serikali kati ya Taasisi moja na Taasisi nyingine au Sekta moja na nyingine katika namna itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi bila vikwazo vyovyote vya kimfumo

**a) Utekelezaji wa Miundombinu na taratibu za kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki katika mchakao wa usaili wa ajira.**

**Mheshimiwa Spika**, Serkali kupitia Sekretarieti ya Ajira imetengeneza Kanuni zilizochapishwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 326 la tarehe 16/04/2021, ambapo Kanuni ya 17 ya Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma za mwaka 2021 zinatoa upendeleo maalum kwa watu.

**Mheshimiwa Spika** Vilevile katika kutekeleza azimio hili la Bunge Kamati ilielezwa kwamba katika usaili wa kuandika, watu wenye ulemavu hupatiwa kipaumbele kwa kuhakikisha hawakai kwenye foleni kwa muda mrefu na pia wakati wa usaili wale wenye uoni hafifu mitihani yao inakuwa na maandishi makubwa na wanaongezewa muda wa usaili, wasioona kabisa wanasomewa maswali na msaidizi na wale wasioona wala kusikia hupatiwa kifaa maalum cha nukta nundu. nchini.

Vile vile, katika ufaulu kwa mlemavu anayefikisha alama 50 huchaguliwa kuingia kwenye usaili wa mahojiano hata kama kuna wasailiwa wasio na ulemavu wenye ufaulu wa alama zaidi ya 50 na wakifika kwenye hatua ya usaili wa mahojiano wenye ulemavu hupatiwa kipaumbele. Kamati ilifafanuliwa Zaidi kwamba katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Januari, 2025 Sekretarieti ya Ajira imewapangia vituo vya kazi waombaji kazi wenye ulemavu 21 ambapo wanaume ni 16 na wanawake ni watano (5) katika Taasisi mbalimbali 16 za Umma.

**b) Serikali ifanye jitihada za kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu za tamaduni Viongozi wa Jadai na kuhifadhi taarifa hizo kidigitali na kufanya kampeni maaluum ya kuhamasisha Wananchi kuenzi utamaduni, historia na mchango wa waasisi wa Taifa letu**

**Mheshimiwa Spika** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imendelea kukusanya nyaraka kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kutunza historia ya nchi kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo na inaendelea kuhamasisha

umma kuenzi utamaduni, historia na mchango wa Waasisi wa Taifa kupitia vyombo vya habari (Televisheni, Radio, Magazeti na Mitandao ya Kijamii), Kuratibu na kushiriki katika maadhimisho, makongamano na midahalo mbalimbali ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa inayoandaliwa na wadau husika

**c) Mifumo ya upandishaji vyeo na mabadiliko ya kimuundo kwa Watumishi iboreshwe ili iende sambamba na mabadiliko ya mishahara**

**Mheshimiwa Spika** katika kusimamia na kutekeleza Azimio hili Serikali imeanzisha Mfumo wa kigitali unaofahamika kama (e-watumishi) ambapo kupitia utaratibu huu tarehe ya cheo kipya cha mshahara wa mtumishi unaotokana na kupandishwa cheo au kubadilishiwa Muundo/Kada wa Utumishi huanza mara baada ya kuidhinishwa kwa taarifa mpya katika Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi), hivyo kudhibiti uzalishaji wa malimbikizo ya Mishahara ya watumishi.

**d) Serikali ione umuhimu wa kufanya ununuzi wa ndege zingine ili kuboresha utoaji huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa.**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza hili Kamati ilielezwa kwamba kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi wa ndege mpya.

**e) Serikali ikamilishe Sera ya Taifa ya TEHAMA Serikalini na kufanya tathmini ya mifumo yote ndani ya Serikali na kubaini mifumo yote ambayo haina tija kwa Serikali na kuchukua hatua madhubuti za kuiondoa**

Mheshimiwa Spika Kamati ilielezwa kwamba Serikali imetekeleza Azimjo hili na mpaka Serikali inafika mbele ya kamati tayari ilikua imekwisha kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Serikali Mtandao na ipo katika hatua za kukusanya maoni ya Wadau.

**f) Serikali ihakikishe kwamba kunakuwa na muunganiko wa mifumo ya Serikali kati ya Taasisi moja na Taasisi nyingine au**

**Sekta moja na nyingine katika namna itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi bila vikwazo vyovyote vya kimfumo**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na kazi ya kuunganisha Mifumo ya TEHAMA katika Serikali ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Desembai, 2024, jumla ya Mifumo 202 kutoka kwenye taasisi za umma 179 imewezeshwa kubadilishana taarifa kupitia Mfumo wa Serikali wa kubadilishana Taarifa (GovESB).

**3.1 Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii Bunge liliazimia masuala yafuatayo:

(i) Kuhakikisha elimu ya madhara ya dawa za kulevya inaendelea kutolewa hususan mashuleni, vyuo vya elimu ya juu na program za redip televisheni na mitandao ya kijamii

(ii) Kampeni za uhamasishaji kupinga dawa za kulevya zianzie ngazi za vitongoji, vijiji, mitaa, tarafa, wilaya, Mikoa na Taifa.

(iii) Kuongeza vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini.

(iv) Kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa (Cargo scanner)

(v) Kuanzisha divisheni maalumu ya mahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya.

i) **Kuhakikisha elimu ya madhara ya dawa za kulevya inaendelea kutolewa hususan mashuleni, vyuo vya elimu ya juu na program za redip televisheni na mitandao ya kijamii**

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa Elimu Kamati ilielezwa kwamba Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini inaendelea kutoa Elimu kwa umma ikiwemo wanafunzi wa ngazi zote na wananchi kupitia makongamano na warsha mbalimbali pamoja na kupitia vyombo vya habari ikiwemo magazeti, televisheni na redio. Aidha kamati ilielezwa kwamba Mamlaka inashirikiana na Taasisi ya kupambana na rushwa nchini TAKUKURU katika kuanzisha klabu za kupinga dawaz akulevya kuanzia ngazi ya sekondari hadi chuo n ahadi kufikia Disemba mwaka 2024 kulikua na klabu zipatazo 15186 sehemu mbalimbali nchini.

ii) **Kampeni za uhamishaji kupinga dawa za kulevya zianzie ngazi za vitongoji, vijiji, mitaa, tarafa, Wilaya, Mikoa na Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali Kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya nchini ina programmu mbalimbali za kuwafikia wananchi na kuwaelimisha kuhusu madhara ya dawa za kulevya na kwa kupitia Tangazo la serikali namba 142 la tarehe 6 Aprili 2028 Mamlaka imekasimisha kazi zake za utoaji elimu kuhusiana na athari za dawa za kulevya kwenye Kamati za UKIMWI kwenye Mamlaka za Serikali za mitaa.

iii) **Kuongeza vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa azimio hili, Kamati ilitembelea Hospitali ya Taifa ya Mwananyamala kuona namna ambavyo Serikali inatoa msaada kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini, Vilevile Kamati ilipata nafasi ya kuongea nao kuhusu msaaada wanaoupata kutoka katika hospitali hiyo na namna ambavyo wale ambao wamepona wanasaidiwa na Hospitali katika kujinasua na changamoto za kiuchumi kwa kupewa ajira za muda mfupi katika kitengo cha waraibu wa dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba katika kusimamia hilo Mamlaka imesimamia uanzishwaji wa nyumba maalumu za upataji nafuu (Sober House) zipatazo 63 ambazo hadi kufikia Disemba 2024 zilikua zimeshahudumia waraibu 17,600, Ujenzi na Uanzishwaji vituo vya kutoa msaada kwa waraibu vipatavyo 17 na hadi kufikia Disemba 2024 vituo hivyo vilisajili waraibu 18,600 na kwa mujibu wa taarifa ya hali ya hali ya dawa za kulevya nchini yam waka 2023 takibani watu 903,062 ambao ni waraibu wa dawa za kulevya na vilevi vingine walitibiwa katika vitengo vya afya ya akili katika hospitali za Wilaya,Mkoa na Hospitali za rufaa za kanda.

iv) **Kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa (Cargo scanner)**

**Mheshimiwa Spika** katika kutekeleza hili Serikali kupitia Mamlaka ya kudhibiti ya dawa za kulevya imefanya ziara katika maeneo ya mipakani na kusisitiza maafisa kukagua dawa za kulevya kwa kutumia Mdaki (cargo scanners). Aidha Kamati ilielezwa kwamba Mamlaka ya Bandari nchini ina mdaki 10,7 katika bandari ya Dar es Salaam,2 bandari ya tanga na 1 Bandari ya Mtwara.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini ila bado kuna haja ya kuhakikisha kwamba mdaki (Cargo scanner) zinaongezwa katika Bandari zetu, maeneo ya mipakani na ili kudhibiti vikali uingizwaji wa dawa za kulevya nchini Serikali inashirikiana na Kampuni za usafirishaji katika mchakato wa upakiaji na upakuaji wa mizigo inayongia nchini.

v) **Kuanzisha divisheni maalumu ya mahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya**.

**Mheshimiwa Spika** Azimio hili halikutekelezwa na badala yake Kamati imeelezwa kwamba kwa sasa Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Kuhujumu Uchumi inajitosheleza katika kuamua mashauri yanahusu madawa ya kulevya nchini na Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo kwa Waendesha mashata

nchini wapatao 490 katika mikoa tofauti kuhusu kuendesha masahauri yanayohusu dawa za kulevya

(a) **Wizara ya Katiba na Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara hii Bunge liliazimia masuala yafuatayo:

(i) Majengo ya Mahakama za Mwanzo yaboreshwe kwa kufanyiwa ukarabati unaostahili;

(ii) Serikali ijenge majengo ya Mahakama za Mwanzo kwenye maeneo ambayo hayana Mahakama za Mwanzo.

(iii) Kuanzisha divisheni maalumu ya kimahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya.

(iv) Serikali iwaongeze jukumu Wanasheria wa Halmashauri kutoa msaada wa kisheria kwa Wananchi kwenye baadhi ya maeneo yasiyo na Wasaidizi wa Msaada wa Kisheria (Para Legals).

(v) Serikali itenge bajeti itakayo boresha miundombinu ya taasisi hizo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao

(vi) Serikali iajiri watumishi wa kutosha kwenye Taasisi hizo kwa kuzingatia ikama ya Taasisi.

**3.1.1 Utekelezaji kuhusu Ukarabati na uboreshwaji wa majengo ya Mahakama.**

**Mheshimiwa Spika**, Mahakama ya Tanzania inatekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (Judiciary Infrastructure Plan: 2021/2022 – 2025/2026). Kupitia Mpango huo, Mahakama inajenga na kukarabati Mahakama za Mwanzo.

**Mheshimiwa Spika** Kamati imeelezwa kwamba Hadi Januari, 2025, yapo majengo 935 ya Mahakama za Mwanzo. Kati ya majengo hayo 191 yapo kwenye hali nzuri; 454 yanahitaji kujengwa upya; na 290 yanahitaji kukarabatiwa.

**3.1.2 Serikali ijenge majengo ya Mahakama za Mwanzo kwenye maeneo ambayo hayana Mahakama za Mwanzo.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeileza Kamati kwamba mpaka janurai 2025 walipowasilisha taarifa ya utekelezaji tayari ujenzi wa majengo 72 ya Mahakama za Mwanzo kwenye maeneo tofauti nchini bado unaendelea.

Vilevile Kamati ilielezwa kwamba kati ya majengo hayo, majengo 60 yanajengwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia na majengo 12 kwa kutumia fedha za maendeleo za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kuhakikisha inajenga Mahakama maeneo mbalimbali nchini ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali ijitahidi kutenga fedha za ndani katika kutekeleza miradi hiyo.

**3.1.3 Utekelezaji kuhusu matumizi ya miundombinu ya kwenye mahakama za mwanzo nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sasa Mahakama za mwanzo nchini zimeanza kutumia miundombinu ya TEHAMA katika kutoa huduma kwa wananchi na zinatoa huduma za TEHAMA kwa kutumia mfumo wa kusajili Mashauri ujulikanao kama "Primary Court Mobile App". Mfumo ambao unawezesha Mahakama kupata taarifa za mashauri ya Mahakama za Mwanzo.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba pindi ukarabati wa Majengo na Miundombinu wezeshi ya TEHAMA ya Mahakama za Mwanzo utakapokamilika, Mahakama hizi zitaanza kutumia mfumo wa kusajili na kuratibu Mashauri ujulikanao kama JoT eCase Management System (eCMS).

3.1.4 **Utekelezaji kuhusu Kuanzishwa kwa divisheni maalumu ya kimahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kwamba kwa sasa Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Kuhujumu Uchumi inajitosheleza katika kuamua mashauri yanahusu madawa ya kulevya nchini.

**Mheshimiwa Spika Vilevile Kamati imeelezwa kwamba** Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa mwaka 2024 ilisajili jumla ya mashauri 170 na kumaliza mashauri 157 sawa na asilimia 92. Mahakama hiyo ilifunga na mashauri 57. Mahakama hiyo pia kwa mwaka 2024 ilitumia wastani wa siku 181 kusikiliza mashauri ya uhujumu uchumi.

**3.1.5 Serikali iwaongeze jukumu Wanasheria wa Halmashauri kutoa msaada wa kisheria kwa Wananchi kwenye baadhi ya maeneo yasiyo na Wasaidizi wa Msaada wa Kisheria (Para Legals).**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza hili Kamati ilielezwa kwamba Wizara imeanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mamlaka zote 184 za Serikali za Mitaa. Aidha, wataalam 449 wameajiriwa kwa ajili ya kuwezesha utendaji kazi wa madawati hayo. Lengo la kuanzishwa kwa Madawati hayo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi ya msingi.

**Mheshimiwa Spika** vilevile inaendelea kushirikiana na wadau wa Sheria mbalimbali nchiniikiwemo Chama cha Mawakili Tanganyika katika kutoa msaada wa kisheria kwa Wananchi kwenye baadhi ya maeneo yasiyo na Wasaidizi wa Msaada wa Kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati imeelezwa kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali meandaa Mwongozo wa Madawati ya Ushauri wa Kisheria katika ngazi ya Mikoa na Wilaya. Pamoja na majukumu mengine, Madawati hayo yanajukumu la

kuhakikisha Wananchi wenye uhitaji wa msaada wa kisheria wanahudumiwa ipasavyo.

3.1.6 **Serikali itenge bajeti itakayo boresha miundombinu ya taasisi hizo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao**.

**Mheshimiwa Spika** katikakutekeleza hili Kamati ilielezwa kwamba serikali iliongeza Bajeti za taasisi zilizo Chini ya Wizara ya katiba na Sheria ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Aidha Kamati ilielezwa kwamba bado Serikali ina mikakati ya kuongeza Bajeti ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania katika mwaka 2025/2026 hususan katika bajeti ya Maendeleo ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake hususan jukumu la mapitio ya sheria na utafiti.

**3.1.7 Serikali iajiri watumishi wa kutosha kwenye Taasisi hizo kwa kuzingatia ikama ya Taasisi.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeendelea kuajiri kukidhi uhitaji wa watumishi katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ikiwemo Mahakama ambayo hadi kufika Disemba 2024 iliajiri watumishi 607, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watumishi 7, Ofisi ya Taifa ya mashtaka watumishi 141, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali watumishi 312, Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania watumishi 3 na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora watumishi 9.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali katika Kuajiri watumishi ila Kamati bado inaona kuna haja ya kuendelea kuajiri kwakua uhitaji wa watumishi katika taasisi zilizo chini ya Wizara Ya Katiba na Sheria hauendani na kasi ya kuajiri na ukizingatia umuhimu wa sekta ya Sheria nchini.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, Kamati imeridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Bunge.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inabainisha mtazamo na maoni ya jumla ya Kamati yanayotokana na shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 na kuonesha maoni ya jumla kwa kila wizara inayosimamiwa na Kamati.Aidha maoni hayo yanalenga kujenga msingi wa hoja ya Kamati kuhusu mambo ya kufanyiwa kazi iwapo Bunge lako Tukufu litaridhia.

**a) Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora.**

**Mheshimiwa Spika** katika kuisimamia Wizara hii kamati ilipitisha bajeti ya Wizara hii na kutembelea miradi ambayo ilitengewa bajeti kwa mwaka wa fedha ulioisha wa 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika** kamati ilikutana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kujadili masuala mbalimbali ikiwemo kupata taarifa za utendaji kazi wa Wizara hiyo na Taasisi zilizo chini yake kwa kipindi cha Aprili hadi Januari 2025.

**Mheshimiwa Spika** licha ya Kamati kuridhishwa na utendaji Kazi wa Serikali kupitia Wizara hii bado kamati inadhani kuna umuhimu wa baadhi ya mambo kufanyiwa kazi ili kuleta ustawi mpana wa maendeleo kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika** Kamati imebaini suala la upungufu wa rasilimali fedha na watu kwenye baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, jambo ambalo linaleta ugumu kwa taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshmiwa Spika,** pamoja na uwepo wa changamoto hizo, Kamati inaipongeza Wizara kupitia mradi wa TASAF kwa

kuendelea kujenga miradi inayolenga kuwakwamua wananchi kiuchumi na kwa kuendelea kutoa afua kwa kaya maskini nchini. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo upungufu wa watumishi.

**Mheshimiwa Spika** Kamati pia inaipongeza Serikali kupitia wakala wa serikali mtandao (e-GA) kwa kuendelea na mchakato wa kuinua vipaji kwenye sekta ya TEHAMA ambao umepelekea kutengenezwa kwa mifumo mingi ya kurahisisha utendaji kazi wa Serikali na taasisi zake kwa njia ya mtandao.

**Mheshimiwa Spika** Kamati ina maoni kuwa ubunifu wa mifumo hiyo Uendane na matumizi kwa kupeleka mtandao hadi maeneo ya vijijini ili kuwezesha watumishi wa umma waliopo maeneo ya hayo kuweza kuitumia mifumo hiyo katika utendaji kazi wao.

**b) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba licha ya Wizara hii kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania kutangaza fursa za Uwekezaji nchini ni maoni ya Kamati kwa Serikali kuhakikisha kunakua na mfumo mmoja wa kodi na utoaji wa leseni miongoni mwa mamlaka za Serikali na Taasisi zake ili kupunguza mlolongo usio wa lazima kwa wawekezaji nchini.

Vilevile Kamati inasisitiza kwamba utoaji huduma ya Uwekezaji mahala pamoja (one stop facilitation centre) uendane na matumizi ya mifumo ambayo itawezesha utoaji huduma wa haraka kwa wawekezaji nchini.

**c) Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**

**Mheshimiwa Spika**; Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi inayofanya katika kudumisha muungano na kutatua changamoto mbalimbali za Muungano.

**Mheshimiwa Spika**; licha ya kutatua changamoto za Muungano ikiwemo ufunguzi wa ofisi za Muungano upande wa Zanzibar Kamati ina maoni kwamba Serikali ijenge jengo moja (Muungano House) ambalo litatumiwa na taasisi zote za Muungano katika utoaji huduma kwa upande wa Zanzibar.

**d) Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Ofisi ya waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kwa kutekeleza majukumu yake kwa namna ambayo inalenga kujenga na kulinda ustawi wa wananchi wa Tanzania. Hata hivyo palipo na mafanikio hapakosi changamoto.

**Mheshimiwa Spika** miongoni mwa Changamoto hizo ni Pamoja na Kuchelewa kwa urejeshwaji wa miundombinu ya Barabara, Umeme na maji kwa maeneo yaliyokumbwa na maafa.

Vilevile Kamati ina maoni kwamba Serikali ichukue hatua za haraka kudhibiti maafa ambayo siyo ya asili ambayo kwa kiasi kikubwa huchangiwa na shughuli za binadamu.

**Mheshimiwa Spika** kwa upekee Kamati inaipongeza Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za Kulevya nchini inayosimamiwa na Wizara hii kwa kutekeleza majukumu yake ya kupambana na dawa za kulevya nchini. Aidha kamati imebaini uwepo wa matumizi ya kemikali Bashirifu kama mbadala wa dawa za kulevya hivyo Kamati inaishauri Mamlaka iendelee kudhibiti na kupambana na uingizwaji wa Dawa za kulevya nchini na iendelee kuzishirikisha mamlaka nyingine za serikali kama Shirika la Viwango Tanzania(TBS), Mamlaka ya Dawa(TMDA) na Bohari ya dawa (MSD) ili kuhakikisha kwamba, taasisi hizi zinashirikiana kwa pamoja kudhibiti uchepushaji wa kemikali na dawa halali kutumika kinyume na matumizi yaliyokusudiwa (dawa za kulevya).

**Mheshimiwa Spika** Kupitia Baraza la kuinua wananchi kiuchumi (NEEC) ambalo linatekeleza jukumu lake hadi ngazi za wilaya, Kamati imebaini kuwepo kwa mifuko Zaidi ya 70 inayoratibiwa na

Baraza ili kuwezesha wananchi kiuchumi, ni maoni ya kamati kuwa, mifuko na mikopo inayoratibiwa na Baraza hili iendane na kutoa elimu kwa wananchi hao ili wananchi waweze kuelewa lengo la mifuko na mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, pia tunaipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais kwa ujumla, kwa kupitisha sheria za Uchaguzi nchini ambazo zinaendana na falsafa ya R nne "4 R'S) za mheshimiwa Rais ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), mabadiliko (Reforms), Ustahimilivu (Resilience) na Kujenga Upya (Rebuilding).

Aidha ni maoni ya kamati kuwa, ili kuakisi falsafa hii ya Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ni vyema Tume Huru ya Taifa ya uchaguzi ijitahidi kuwafikia wananchi wote kwa kuweka vituo vya kupigia kura karibu na makazi ya watu na maeneo yanayofikika kwa urahisi na wananchi walio wengi hasa wa maeneo ya vijijini.

**e) Wizara ya Katiba na Sheria**

**Mheshimiwa Spika** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mama Samia Legal Aid Campaign ambayo imezinduliwa katika mikoa kumi na saba (17) nchini**.**

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kwamba uzinduzi wa Kampeni hizi unaoendelea kufanyika nchini ushirikishe wadau mbalimbali wa mikoa husika ili kuleta hamasa na kuweza kuwafikia walengwa wa kampeni hii ambao ni wananchi kwa ukaribu.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati imebaini kuwa, licha ya kuwepo kwa miradi mingi ya kutoa msaada ya kisheria nchini bado kuna changamoto ya uelewa wa masuala ya kisheria kwa wananchi walio wengi hasa waliopo maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina kuwa Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya Kisheria na vyombo vya Utoaji haki nchini.

## 4.2 Mapendekezo

### 4.2.1 Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora

(i) **Uhaba wa rasilimali watu na Fedha kwenye Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini.**
**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa fedha, wataalamu na vitendea kazi kwenye Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU),

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo inapelekea Taasisi hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu nchini,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali iongeze bajeti kwa taasisi itakayoiwezesha Taasisi hiyo kuajiri watumishi, kujenga ofisi hadi ngazi za Wilaya na kununua vitendea kazi vitakavyoiwezesha kutekeleza majukumu yake kiufanisi.

(a) **Utekelezaji wa Miradi ya TASAF nchini.**
**KWA KUWA** Kamati imebaini kutokuwepo kwa miradi endelevu inayotekelezwa na TASAF, uelewa mdogo wa wananchi juu ya wanaostahili kuwa wanufaika wa TASAF na kuwepo na upungufu wa watumishi wa TASAF katika ngazi za Wilaya nchini,

**NA KWA KUWA** Changamoto hizo zinapelekea miradi inayotekelezwa kuwa si ya kuendeleza jamii nzima na kuisaidia kiujumla kujikwamua kiuchumi ili kuondokana na kuwa tegemezi kwa Serikali,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ifanye jitihada za kutekeleza miradi ya TASAF ambayo ina TIJA ZAIDI na manufaa kwa wananchi na ambayo itawezesha wananchi kujiajiri kupitia miradi hiyo na hivyo kukuza kipato kwa wananchi.

(ii) Serikali ikishirikiana na viongozi wa ngazi zote nchini itoe elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya malengo ya mradi wa TASAF kuhusu sifa na vigezo vya wanaostahili kuwa wanufaika.

**(b) Mfumo wa kupima utendaji kazi kwa Watumishi (PEPMIS) ambayo kwa sasa inatambulika kama eUtendaji kwa watumishi waishio maeneo ya vijijni.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini uwepo wa changamoto ya mtandao na vitendea kazi vinavyowezesha watumishi kujaza utekelezaji wa majukumu yao kwenye mfumo wa kupima utendaji kazi kwa watumishi ambao wanaoshi maeneo ya vijijini,

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo husababisha baadhi yao kushindwa kujaza taarifa za utekelezaji wa majukumu yao katika mfumo huo kwa wakati, na hivyo wengine kushindwa kufikisha asilimia zinazotakiwa,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Matumizi ya mfumo wa Kupima Utendaji kazi kwa watumishi yaendane na utoaji wa vitendea kazi na kuboresha mtandao katika maeneo ya vijijini ili kuwawezesha watumishi kujaza taarifa za utendaji kazi wao kwa ufasaha; na

(ii) Serikali ifanye tathimini ya utekelezaji wa Mfumo wa PEPMIS na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza kwa kipindi cha mwaka mmoja toka ulipoanza kutumika.

**(c) Kuwepo kwa Mifumo mingi ya TEHAMA inayotokana na mchakato wa kuinua vipaji kwenye sekta ya TEHAMA.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa mifumo 18 iliyoibuliwa na vijana kupitia programu ya kukuza vipaji vya TEHAMA zinazotekelezwa na kituo cha utafiti na ubunifu wa Serikali mtandao (e-Government, Research Innovation and development Centre) (eGOVRIDC),

**NA KWA KUWA**, mifumo hiyo inaonekana kuwa na mlengo unaofanana na kutotumika na Taasisi nyingi za Serikali,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali kupitia kituo cha utafiti na ubunifu wa serikali mtandao inatangaza bunifu hizo zinazofanywa na vijana wa kitanzania na kuzitafutia masoko ya ndani na nje bunifu/program hizo,

(ii) Serikali iratibu mchakato wa kuunganisha mifumo hiyo na kuwa Mfumo mmoja; na

(iii) Serikali ihakikishe inapeleka mtandao maeneo ya vijijini ili kuwezesha watumishi wa umma waliopo maeneo hayo wanatumia mifumo hiyo.

**4.2.2 Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji.**

**a) Kutokuepo kwa mfumo mmoja wa kutoa leseni na ulipaji wa kodi kwa wawekezaji nchini**

**KWA KUWA** Kamati imebaini uwepo wa masharti ya leseni nyingi zinazotolewa na mamlaka tofauti za Serikali nchini kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

**NA KWA KUWA** masharti hayo yanaweza kuchukuliwa kama usumbufu na hivyo kupunguza kasi ya wawekezaji kuja kuwekeza nchini,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iratibu utengenezwaji wa mfumo wa pamoja wa Ulipaji kodi (Mifumo ya kodi kusomana) kwa wawekezaji na wafanyabiashara nchini;

(ii) Kuwepo kwa mfumo mmoja wa utoaji leseni za biashara nchini kwa wawekezaji wazawa na wa kigeni ambao utaratibiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania; na

(iii) Serikali kupitia tovuti ya kituo cha Uwekezaji ibainishe aina ya leseni zote mwekezaji anatakiwa kuwa nazo kwenye sekta tofauti za uwekezaji nchini na namna ambayo ataweza kuzipata.

**b) Vituo Jumuishi vya Uwekezaji kutokua na watumishi wenye mamlaka ya kutoa maamuzi;**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba watumishi wengi ambao wanafanya kazi katika vituo jumuishi vya Uwekezaji nchini kuwa hawana mamlaka ya kutoa maamuzi kwenye baadhi ya mambo yanayohitaji uharaka.

**NA KWA KUWA** changamoto hiyo inapelekea kukwamisha baadhi ya taratibu za kusajili na kuwahudumia wawekezaji nchini.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba;
Serikali ihakikishe kwamba watumishi wanaowekwa katika vituo jumuishi vya Uwekezaji (One Stop Centre) wana uwezo na mamlaka ya kutoa maamuzi ili kukuza na kuboresha utoaji huduma kwa wawekezaji nchini.

**4.2.3 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**

**(a) Kutokuwepo majengo ya kudumu kwa baadhi ya Taasisi za Muungano Upande wa Zanzibar.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kutokuwepo kwa majengo ya Kudumu kwa Taasisi za Muungano upande wa Zanzibar.

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo inapelekea Serikali kuingia gharama ya kulipa kodi za kukodi ofisi kwa upande wa Zanzibar;

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe ujenzi wa Ofisi na majengo ya kudumu kwa upande wa Zanzibar ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

### 4.2.4 Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge Na Uratibu)

a) **Ongezeko la Matumizi ya dawa za kulevya zenye Kemikali bashirifu nchini**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba kwa mwaka 2023 Mamlaka ya kuzuia na kupambana na Dawa za kulevya nchini ilifanikiwa kuzuia uingizaji nchini wa kemikali bashirifu Kilogragmu 157,738.55. na kukamata jumla ya kemikali bashirifu zenye ujazo wa lita 22,682 kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2024

**NA KWA KUWA** Changamoto ya ongezeko la matumizi ya kemikali hizi Bashirifu "NPS" zina viwango vikubwa vya kulevya mara 50 hadi 100 ukilinganisha na dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa na hupelekea matatizo makubwa ya afya na athari za magonjwa mbalimbali ikiwemo utegemezi na uraibu usioponyeka kirahisi, magonjwa ya akili, moyo, mfadhaiko, kifafa na vifo vya ghafla kwa mtumiaji

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba

a. Serikali ihakikishe elimu inatolewa kuhusu uwepo wa aina mpya ya dawa za kulevya (NPS) na madhara ya kemikali hizo kwa jamii.

b. Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini ishirikiane na Taasisi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Shirika la Viwango (TBS)na Bohari ya Dawa Tanzania (MSD) kudhibiti maduka ya dawa za binadamu kujihusisha na uuzwaji wa kemikali bashirifu nchini.

c. Serikali iongeze bajeti ya mamlaka ili iweze kujenga Vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kulevya hadi ngazi ya mkoa.

d. Kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa (*Cargo scanners*) katika sehemu za usafirishaji na upakuaji mizigo nchini.

b) **Urejeshwaji wa miundombinu kwa maeneo yaliyokumbwa na maafa nchini.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwa, kumekua na changamoto ya urejeshwaji wa miundombinu kwenye maeneo yaliyokumbwa na maafa nchini.

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo hupelekea wananchi kukosa huduma za msingi ikiwemo umeme, maji na Barabara kwa muda mrefu.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kuwa, Serikali irejeshe huduma muhimu za kijamii kwenye maeneo yaliyokumbwa na maafa hayo.

c) **Changamoto ya Vituo vya kujiandikisha na vya kupiga kura.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba kumekua na changamoto ya umbali wa vituo vya kujiandikishia wapiga kura, umbali wa vituo vya kupiga kura kwa maeneo ya vijijini na uchache wa watumishi wa kusimamia zoezi hilo.

**NA KWA KUWA** Changamoto hiyo inapelekea wananchi wengi kushindwa kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpiga kura na kushindwa kushiriki katika kutimiza haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wao.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba

(i) Vituo vya kuandikisha wapiga kura na vituo vya kupiga kura viwekwe karibu na makazi ya wananchi ili waweze kushiriki na kutekeleza haki yao ya kikatiba.

(ii) Serikali ihakikishe inapeleka watumishi wa kutosha katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kusimamia zoezi hilo.

**4.2.5 Wizara ya katiba na Sheria**

**(a) Wananchi kutokua na uelewa na Elimu ya kisheria na kutokufahamu sehemu sahihi za kupeleleka malalamiko yao.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini sehemu kubwa ya wananchi kutokua na uelewa wa kutosha na masuala yahusuyo sheria na;

**NA KWA KUWA** hali hii husababisha baadhi kupeleka masuala ya kisheria kwenye vyombo visivyo na mamlaka na wengine kushindwa kabisa.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia legal Aid Campaign) na ikishirikiana na Asasi za Kiraia nchini inawafikia wananchi wote nchini hasa waishio maeneo ya vijijini.

(b) **Ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi wa Mahakama.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi wa mahakama nchini;

**NA KWA KUWA** changamoto hiyo inasababisha wananchi kutokuwa na Imani na Mahakama na vyombo vya utoaji haki nchini.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe inawachukualia hatua za kinidhamu watumishi ambao watabainika kuwa na ukosefu wa maadili na kushindwa kutimiza majukumu yao ipasavyo.

(c) **Upungufu wa Bajeti na watumishi katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya Bajeti na upungufu wa rasilimali watu kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini.

**NA KWA KUWA** Upungufu huo unapelekea Tume hii ambayo ndio jicho la serikali kushindwa kutimiza majukumu yake kwa weledi na ufanisi kwa kushindwa kufika maeneo mengi nchini.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2025/2026 ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ya kutoa taarifa za uvunjivu wa haki za Binadamu na kuhakikisha Serikali na Taasisi zake zinafuata misingi ya utawala bora.

(d) **Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya mara kwa mara kwenye sheria nyingi nchini.**

**KWA KUWA** Kamati imebaini kwamba Serikali imekuwa ikileta mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya mara kwa mara Bungeni ili kufanyiwa marekebisho na kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo.

**NA KWA KUWA** Changamoto hii huweza kuonekana kama kuna upungufu wa tafiti za kutosha kwenye sheria zetu nchini.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iiwezeshe Tume ya kurekebisha Sheria kwa kuitengea fungu la maendeleo ili iweze kutekeleza jukumu la kufanya tafiti kwa sheria kabla hazijaletwa Bungeni.

(ii) Serikali ihakikshe kwamba inatenga Bajeti ya kutosha kwa Tume ya kurekebisha Sheria ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

(e) **Mkanganyiko wa tafsiri ya Kisheria katika kifungu cha 80(2) cha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na Sheria Nyingine nchini**.

**KWA KUWA** Kamati imebaini kuwepo kwa mkanganyiko wa kisheria katika tafsiri ya kifungu cha 80(2) cha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263, na kuwepo kwa changamoto ya kisheria katika sheria nyingine 41 zinazotumika nchini;

**NA KWA KUWA** mkanganyiko huo hupelekea changamoto ya tafsiri ya Sheria hizo katika mahakama zetu na vyombo vyote vya utoaji haki nchini;

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali ipitie Sheria hizo zote na kuzifanyia marekebisho ili kutatua changamoto zinazijitokeza katika utekelezaji wake.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha nakupongeza kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu vizuri; pia Shukrani ziende kwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanazofanya.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo (Mb), kwa ushirikiano anaonipa pamoja na Kamati kwa ujumla. Kipekee zaidi nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - **Mjumbe**

4. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - **Mjumbe**
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb – **Mjumbe**
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb – **Mjumbe**
7. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb – **Mjumbe**
8. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb – **Mjumbe**
9. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb – **Mjumbe**
10. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb – **Mjumbe**
11. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb – **Mjumbe**
12. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb – **Mjumbe**
13. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb – **Mjumbe**
14. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb – **Mjumbe**
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb – **Mjumbe**
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb – **Mjumbe**
17. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb – **Mjumbe**
18. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - **Mjumbe**
19. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - **Mjumbe**
20. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - **Mjumbe**
21. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - **Mjumbe**
22. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - **Mjumbe**

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa, niwashukuru viongozi wote wa Mhimili wa Utendaji *(The Executive)* kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake. Kwa kipekee, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Hamza Johari, Mb. – **Mwanasheria Mkuu wa Serikali**
2. Mhe. George Huruma Mkuchika, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais**
3. Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
4. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti, ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**
5. **Mh. Prof Kitila Alexander Mkumbo, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji)**
6. Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, Mb. – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)**

7. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb. – **Waziri wa Katiba na Sheria**
8. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – **Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
9. Mhe. Deus Clement Sangu Mb. – **Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti, ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**
10. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb. - **Naibu Waziri, Ofisi ya Rais –Mipango na Uwekezaji**
11. Mhe. Khamis Hamza Khamis, Mb. -**Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira**.
12. Mhe. Jumanne Abdallah Sagini, Mb. -**Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria.**

**Mheshimiwa Spika**, vilevile niwashukuru Watendaji wote wa Mhimili wa Utendaji *(The Executive*) na Mhimili wa Mahakama *(The Judiciary)* kwa ushirikiano walioipatia Kamati. Kwa niaba yao wote naomba niwatambue viongozi wao kama ifuatavyo: -

1. Dkt. Jim James Yonazi – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**
2. Ndg. Juma Selemani Mkomi – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti, ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**
3. Mhandisi. Cyprian John Luhemeja – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)**
4. Ndg. Eliakim Chacha Maswi – **Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria**
5. Dkt. Tausi Mbaga Kida – **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji)**
6. Ndg. Abdallah Hassan Mitawi**-Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.**
7. Prof. Elisante Ole Gabriel – **Mtendaji Mkuu wa Mahakama**

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee Kamati inatoa pole kwa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa kuondokewa na aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Ndg. Lawrence Nyasebwa Mafuru aliyefariki akipatiwa matibabu katika hospitali ya Apollo nchini India mnamo tarehe 9 Novemba 2024.Hakika atakumbukwa kwa uzalendo na utumishi wake uliotukuka, bidii na ubunifu

alipotumikia nafasi mbalimbali ndani ya Serikali na Taifa lake kwa ujumla. ***(Bwana alitoa ..Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe)***

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge **Ndg. Baraka I. Leonard** na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa Uratibu wa Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**5.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako sasa liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
05 Februari, 2025

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 – Januari, 2025 ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hiyo imeweka sharti la lazima kwa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Bungeni taarifa ya mwaka ya shughuli zake ili ijadiliwe katika Mkutano wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda au *scope* ya taarifa: Taarifa inafafanua shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka kuanzia mwezi Februari, 2024 – Januari, 2025. Matokeo yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati na mapendekezo kwa Bunge kuhusu nini kifanyike kutokana na yaliyobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo unatokana na masharti yaliyofafanuliwa katika misingi mbalimbali kama kuzingatia Katiba ya Nchi, Sheria za Nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia zifuatazo: -

(i) Kufanya mapitio ya matoleo ya magazeti ya Serikali yanayowasilishwa Bungeni;

(iii) Kufanya uchambuzi wa awali wa Sheria Ndogo ili kutathmini namna Sheria Ndogo zilivyozingatia mashari ya Katiba, Sheria Mama na sheria nyingine za nchi;

(iv) Kuhakiki mtiririko wa maudhui ikilinganishwa na masharti yanayowekwa katika Sheria Ndogo;

(v) Uoanishaji wa masharti ya Sheria Ndogo inayohusika na misingi iliyowekwa katika Katiba na sheria nyingine za nchi;

(vi) Kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu Sheria Ndogo hizo; na

(vii) Mahojiano na mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo kwa idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngazi zilizotumika wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, zinajenga maoni ya Kamati ambayo ni msingi wa maazimio ya Bunge yanayopendekezwa katika taarifa hii. Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka 2024, zinaainishwa kwa kujumuishwa katika maeneo mawili ambayo ni: -

(i) Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na, Mkutano wa Kumi na Saba; na

(ii) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa 12, Mkutano wa 13, Mkutano wa 14 na Mkutano wa 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa na matokeo kuripotiwa Bungeni. Katika kipindi cha mwaka mmoja, Kamati ilifanya shughuli za uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano, hali kadhalika uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo 38 za Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano, yaliwasilishwa Bungeni katika Taarifa ya Kamati mnamo tarehe 4 Septemba, 2024 katika Mkutano wa 16 wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo 22 za Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita tarehe 4 Septemba, 2024. Maazimio yote yalitekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ambayo matokeo yake hayajaripotiwa Bungeni; taarifa hii inaripoti kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge pamoja na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Matokeo ya uchambuzi wa shughuli zote mbili yanaripotiwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba. Uchambuzi wa Sheria Ndogo 54 zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba, umefanyika katika kipindi kinachoripotiwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako kuwa, matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo yanayowasilishwa kupitia taarifa hii, yamemeng'enywa ili kuliwezesha Bunge kupima kuhusu hatua stahiki za kuchukua dhidi ya dosari zinazobainishwa, kwa urahisi wa kufuatilia, jedwali la uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba, vimeambatanishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili hiyo, ili Bunge liweze kufanya uamuzi ulio na tija, sehemu hii ya taarifa inaweka bayana mifano ya dosari zilizobainika wakati wa uchambuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba: Katiba ya Nchi ndiyo Sheria Kuu na inapaswa kuzingatiwa na sheria zote nchini. Ibara ya 64(5) ya Katiba inaelekeza kuwa sheria zote zinazotungwa hazipaswi kupingana au kukiuka masharti ya Katiba, ni lazima zifuate masharti ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, Sheria Ndogo ambayo ni sehemu ya Sheria ya Nchi inayofafanua Sheria ya Bunge, pia haitarajiwi kukiuka masharti yanayowekwa na Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yamebaini Sheria Ndogo zenye Vifungu vilivyo na maudhui yanayokiuka masharti ya Katiba. Mfano wa Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yanayokiuka Katiba ni Kanuni za Nidhamu kwa wanafunzi wa Shule ya Sheria *(Law School)*, 2024, tangazo la Serikali na. 365 la mwaka 2024. Kanuni ya 23(3) inahusu mwanafunzi au mtuhumiwa kutokuwepo wakati wa kusikilizwa kwa shauri lake la kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni inaruhusu kuendelea kusikilizwa kwa shauri pasipo kuzingatia sababu za msingi zinazoweza kusababisha mwanafunzi huyo kutohudhuria kikao hicho. Ibara ya 13(6)(a) ya Katiba, inaelekeza kwamba wakati wa haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa maamuzi na Mahakama au chombo kingine kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kwamba masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 23 yanakiuka haki ya mtu kusikilizwa kwa mujibu wa Katiba hali inayoweza kusababisha kutumiwa vibaya na wenye mamlaka dhidi ya mwanafunzi huyo jambo ambalo linakinzana na sifa ya Sheria bora ya kuzuia unyanyasaji, kulinda wanyonge na kusimamia usawa wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi: Bunge linapotunga sheria zake, huweka vifungu vinavyozielekeza mamlaka nyingine kutunga Sheria Ndogo ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria iliyotunga na Bunge, maelekezo ya Bunge huwa ni kwa kutaja maeneo mahususi ambayo sheria ndogo

inapaswa kuakisi au kuwezesha utekelezaji wa jumla wa masharti ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa Sheria ya Bunge kupitia Sheria Ndogo, Sheria ya Tafsiri ya Sheria inaweka misingi ya uandishi, tafsiri, matumizi na mambo mengine muhimu kuhusu sheria za nchi kwa ujumla. Kifungu cha 36 (1) cha sheria hiyo, kimeweka masharti yanayokataza Sheria Ndogo kwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo kuwa zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi. Mfano wa sheria hizo ni Kanuni za Uwindaji wa Kitalii Tangazo la Serikali Na. 780 la Mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 14(8) ya Kanuni hizi inataja adhabu kwa mtu yeyote atakayewasilisha taarifa za uongo wakati wa kuomba kibali au leseni, adhabu kwa kosa hilo ni kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha juu cha adhabu ya kifungo cha miaka mitatu kinachowekwa na Sheria Ndogo hii kinakinzana na kiwango cha juu cha kifungo kilichowekwa na Kifungu cha 105 cha Sheria Mama ambacho ni miaka mitano. Ukinzani huo ni kinyume na masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria, na pia ni kinyume na azma ya Sheria ya Bunge kuhusu adhabu kwa mtu yeyote atakayewasilisha taarifa za uongo wakati wa kuomba kibali au leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, adhabu iliyowekwa inaathiri uhalali wa kifungu hiki kwa kuwa unavuka mamlaka yake na kuingia katika ubatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia. Pamoja na masuala mengine, uandishi wa sheria hulenga kuweka masharti mbalimbali ambayo zao la utekelezaji wake ni kushughulikia, kufanikisha au kutatua jambo fulani miongoni mwa wanaolengwa na masharti yanayohusika. Matokeo ya uchambuzi yanabainisha masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia ikilinganishwa na lengo la Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari hiyo imebainika katika Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, 2024 Tangazo la Serikali Na. 815 la Mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo linaonesha mfano wa kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi ambapo pamoja na kuweka sharti la kuomba kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi kwa ajili ya biashara, kibali hicho pia kimetaja wahusika wanaopaswa kuomba kibali cha kusarifisha mazao ya uvuvi ikiwemo samaki kwa matumizi ya nyumbani. Kwa mantiki ya masharti hayo, mwananchi yeyote aliye katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ambaye atahitaji kupata samaki kwa matumizi ya nyumbani, atapaswa kuomba kibali cha kusafirisha samaki hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti haya hayana uhalisia katika utekelezaji wake na yanaweza kutafsirika kuwa ni kero kwa wananchi wanaonunua na kusafirisha mazao hayo kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni dosari ya kutoendana na misingi ya Uandishi wa Sheria. Sheria hutungwa kwa ajili ya kufanikisha jambo au mambo mahsusi yaliyokusudiwa na sheria inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia lengo lililokusudiwa, sheria hupaswa kuwa na maudhui yanayoeleweka, kuwa na masharti

yanayolengwa kuwepo katika sheria inayohusika, na kuwa na ukamilifu wa kimaudhui.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa misingi hiyo ni kuwezesha sheria kueleweka na kutekelezeka kwa urahisi na wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebainisha dosari za sheria ndogo kutozingatia masharti ya uandishi. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni Kanuni za Uwindaji wa Kitalii, 2024 Tangazo la Serikali Na. 780 la mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umebaini dosari katika Kanuni ya 29(4)(b) inayotaja adhabu ya kuwinda simba aliye chini ya umri wa miaka minne. Kamati imebaini dosari ya uandishi katika Kanuni ya 29 ambazo kwa pamoja zinaweka adhabu moja ya faini ya shilingi milioni tano kwa makosa yasiyofanana. Makosa hayo ni kuwinda simba chini ya umri wa miaka minne, faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya kwanza ya utendaji wa kosa; faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya pili ya utendaji wa kosa; au faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya tatu ya utendaji wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari hiyo ina athari za kukosesha uwiano wa haki *(proportional justice)* kutokana na kutozingatia muktadha wa makosa ikilinganishwa na adhabu stahiki. Aidha, makosa hayo ya uandishi wa adhabu ni kana kwamba yanalenga kuchochea utendaji wa makosa ya uwindaji kwa kutoa adhabu ndogo kwa kadiri mtenda kosa anavyorudia kutenda kosa linalofanana kwa mara nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ni dosari za uandishi wa majedwali. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Jedwali ni sehemu ya sheria, hivyo linastahili kuwa na misingi inayofanikisha lengo la sheria. Kwa mantiki hiyo, Bunge linapofuatilia sheria ndogo huangazia majedwali katika sheria hizo ili kujiridhisha na masuala mbalimbali yanayoweza kuathiri tija ya sheria ndogo yenyewe sambamba na Sheria ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya uandishi wa majedwali katika sheria ndogo imebainika katika Sheria Ndogo za *The Law School of Tanzania Students General Welfare, Conduct and Disciplinary Matters Rules, 2024* Tangazo la Serikali Na. 615 la mwaka 2024. Dosari ya uandishi ilibainika katika Jedwali la Pili linalohusu Kanuni za mavazi ya wanafunzi. Jedwali hili la Pili linaweka adhabu inayomtaka mwanafunzi atakayekiuka kanuni za mavazi kutakiwa kurudi nyumbani kubadilisha mavazi aliyoyavaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umebaini kasoro ya uandishi ambapo maelezo kuhusu sharti la mwanafunzi kurejea nyumbani hayajawekewa kifungu na wala hayapo ndani ya jedwali linalohusika. Hali hiyo inasababisha maelezo hayo kukosa nguvu ya kisheria lakini pia, changamoto ya kufanya rejea kuhusu sehemu yanapopatikana masharti hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nne na Mkutano wa Kumi na Tano; misingi ya utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge, upo wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati imefuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa tarehe 4 Septemba, 2024 kuhusu Sheria Ndogo 38 zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Kumi na Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uangaliaji na ufuatiliaji wa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji, ulidadisi mambo manne yafuatayo: -

(i) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio;

(ii) Iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(iii) Iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali; na

(iv) Iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye maoni na mapendekezo.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mapendekezo: Kutokana na matokeo ya uchambuzi, naliomba Bunge lijadili taarifa hii na kupitisha maazimio kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na Katiba:-

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba, na hivyo kuwa kinyume na misingi ya sheria inayotambua ukuu wa Katiba;

Na kwa kuwa, ukiukwaji wa masharti ya Katiba kwa sheria ndogo yoyote au sheria ya Bunge ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba ambayo inabatilisha sheria inayokinzana nayo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizoweka Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba zifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi:-

Kwa kuwa, zipo sheria ambazo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na sheria nyingine za

nchi, jambo ambalo siyo dhamira ya Bunge kukabidhi mamlaka Serikalini madaraka ya kutunga sheria, ni ukiukwaji wa katazo lililowekwa na Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, na halisaidii utekelezaji wa Sheria Mama inayohusika au Sheria nyingine ya nchi ilivyostahili:-

Na kwa kuwa, kuwepo kwa sheria ndogo zinazokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi, ni kuvuka mipaka iliyowekwa na Bunge;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo ambazo zimebainika kukinzana na masharti ya Sheria Mama na sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti yasiyo na uhalisia:-

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria:-

Kwa kuwa, baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba zimebainika kuwa na dosari ya kutokuendana na misingi ya uandishi wa sheria;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo ambazo zimebainika na dosari hizo, zirekebishe dosari za kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari za uandishi wa Majedwali:-

Kwa kuwa, Majedwali ni sehemu ya sheria kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria na yanastahili kusomwa kwa pamoja na vifungu vinavyohusika;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotunga sheria ndogo zinazobainika kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurekebisha dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo na madhara yake:-

Kwa kuwa, dosari zilizobainika kwenye Sheria Ndogo kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali la Uchambuzi ambalo ni Kiambatisho Na. 1 cha Taarifa hii, ni jambo linaloendeleza madhara yasiyokubaliwa;

Na kwa kuwa, kuendelea kwa madhara ya dosari zilizobainika kwenye Sheria Ndogo baada ya kuazimiwa na Bunge kwamba zirekebishwe, ni suala ambalo, linaweza kuliweka Bunge katika hali ya kutoeleweka kwa wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na Sheria Ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii: -

(i) Zitekeleze maazimio haya kwa kasi inayotakiwa ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainishwa; na

(ii) Ziwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo wakati wa vikao vya Kamati kuekelea Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, yaani Mkutano wa Bajeti ujao 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokukamilika kwa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyolenga kurekebishwa kwa sheria ndogo:-

Kwa kuwa, athari za dosari za Sheria Ndogo zinafikia hatua ya juu ya kushughulikiwa kwa marekebisho ya Sheria Ndogo kutangazwa katika Gazeti la Serikali, imebainika mamlaka ambazo hazijafikia hatua za kutangaza marekebisho ya Sheria Ndogo ni kutokana na kuwa na mlolongo mrefu wa hatua za ukamilishaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizobainika kutokuwa zimefikia hatua ya kutangaza marekebisho hayo kuondoa mlolongo mrefu wa hatua za kufanya marekebisho hayo na ziwasilishe taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge wakati wa vikao vya Kamati kuekelea Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na kwako wewe binafsi kwa uongozi wenu mahiri wa Bunge, ambao umeweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati namshukuru Mheshimiwa William Vanging'embe Lukuvi, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kwa uratibu unaowezesha mawasiliano mazuri kati ya Serikali na Kamati yangu hivyo kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa ushirikiano anaoipatia Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuijadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha

Februari, 2024 hadi Januari, 2025 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KWA KIPINDI CHA JANUARI 2024 HADI FEBRUARI 2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Imetolewa chini ya Kifungu cha 136(15) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]

## SEHEMU YA KWANZA
## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Februari 2024 hadi Januari 2025 ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni hiyo imeweka sharti la lazima kwa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake, ili ijadiliwe katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa inayowasilishwa Bungeni leo, inaelezea kwa undani shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha mwaka mmoja na kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hizo, zimeeleza wazi kuhusu majukumu na msingi wa shughuli za Kamati ya Sheria Ndogo.

#### 1.1.1 Madhumuni ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa Bunge kuitumia Kamati hii katika udhibiti wa utekelezaji wa madaraka ya kutunga Sheria yaliyokabidhiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini unakua na tija iliyokusudiwa kwa Kamati kuwasilisha Taarifa yake kwa Bunge

lenyewe. Lengo la kuwasilisha taarifa ni kulifahamisha Bunge kuhusu hali ya utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maelezo hayo, Taarifa hii inayowasilishwa leo mbele ya Bunge, inalenga kuripoti mambo makuu matatu, ambayo ni, kuangazia hali ya jumla kuhusu sheria ndogo zinazotumika nchini kwa kipindi cha kuanzia Februari 20224 hadi Januari 2025, hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwa kipindi hicho na kutoa mapendekezo mbalimbali yanayohitaji kufanyiwa kazi kutokana na maoni ya Kamati kuhusu hali hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni hayo yanatimia kwa kutoa ufafanuzi wa ujumla kuhusu hali ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge ya Kutunga Sheria yaliyokasimiwa Serikalini na Matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowekwa Mezani Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba. Vilevile, Taarifa hii inaripoti matokeo ya uchambuzi Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Maazimio hayo yanahusu sheria ndogo zilizowekwa Mezani Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano.

### 1.1.2 Mawanda (*Scope*) ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Mawanda ya Taarifa hii kulingana na madhumuni niliyoyabainisha, yanagusa masuala yafuatayo: -

(i) Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwezi Februari 2024 hadi Januari, 2025;
(ii) Matokeo yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati; na
(iii) Mapendekezo kwa Bunge kuhusu nini kifanyike kutokana na yaliyobainika kwa kipindi kinachoripotiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli zinazoripotiwa ambazo zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari 2024 hadi Januari 2025 zitaliwezesha Bunge kufuatilia namna madaraka ya

kutumga sheria ndogo yanavyotumika. Ufuatiliaji huo ni jukumu la msingi la Bunge na unachangia katika kulisimamia lengo la Serikali ambalo ni ustawi wa wananchi kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka masharti kuhusu muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Kwa uzingatiaji wa masharti hayo, naomba kubainisha Muundo wa Taarifa hii ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tatu:

(i) Sehemu ya Kwanza ni utangulizi ambao unatoa maelezo ya jumla yanayojenga msingi wa maudhui ya Taarifa hii, pia kuwezesha majadiliano ya Bunge;

(ii) Sehemu ya Pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari 2024 hadi Januari 2025. Sehemu hii inafafanua kwa kina kuhusu shughuli hizo, msingi wa shughuli hizo, pia inaonesha mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati; na

(iii) Sehemu ya mwisho ambayo ni ya Tatu inajumuisha maoni ambayo chimbuko lake ni shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja. Dhumuni la sehemu hii ni kujenga msingi wa mapendekezo katika hoja ya Kamati inayojadiliwa Bungeni leo. Aidha, sehemu hii inatoa Mapendekezo kwa mfumo wa Hoja kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu mfumo wa maneno ya Hoja. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi kuhusu masuala yaliyobainika wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka kuanzia Februari 2024 hadi Januari 2025.

**Mheshimwa Spika,** Mwisho wa Taarifa hii ni kutoa hoja ili kulipa Bunge lako fursa ya kuunga mkono na kuijadili inavyostahili. Kwa hatua hiyo, Bunge linaweza kukamilisha mjadala na kufanya

uamuzi kuhusu eneo la udhibiti wa madaraka ya kutunga sheria ndogo yanayokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Muundo huu wa Taarifa umeakisi wasilisho halisi la Taarifa yenyewe na pamoja na viambatisho ambavyo ni sehemu ya Taarifa na vinastahili kuingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Kwa msingi huo, naomba Bunge liipokee na kuijadili taarifa ya Kamati pamoja na viambatisho vyake vyote ambavyo ni: -

**Kiambatisho Na. 1** ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba; na

**Kiambatisho Na. 2** ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano.

**Mheshimiwa Spika,** Viambatisho hivyo ni muhimu kwa kuwa vinatoa ufafanuzi kwa kina kuhusu mambo yote yanayotokana na uchambuzi wa ndogo sambamba na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Lengo lake ni kuonesha hali halisi ya mambo yaliyobainishwa ambayo yataliwezesha Bunge kusimamia madaraka yake ya kutunga sheria iliyoyakabidhi kwa mamlaka nyingine serikalini.

### 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo zinatokana na masharti yaliyofafanuliwa katika misingi mitatu ambayo ni: -

#### 1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 (1) ya Katiba inaweka mgawanyo katika utekelezaji wa mamlaka ya nchi. Mgawanyo huo

unalitambua Bunge kuwa ndio chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Pamoja na mamlaka yaliyoelezwa katika Ibara ya 4, pia kwa mujibu wa Ibara ya 97 (5) ya Katiba, Bunge limepewa uwezo wa kukabidhi kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka Kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria kanuni zilizowekwa na mtu yeyote au idara yoyote ya serikali.

### 1.3.2 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.*1)

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ni sheria inayoweka kanuni za msingi kuhusu maana, ufafanuzi, namna ya uandishi, matumizi na mambo mengine kuhusu misingi ya sheria za nchi. Lengo la sheria hii ni kuimarisha sheria za nchi kwa minajili ya kuleta utangamano na uwazi wa sheria zote nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa msingi huu, mfumo wowote utungaji wa sheria ndogo nchini pamoja na mchakato wa kuanzisha matumizi yake unapaswa kuakisi masharti yaliyowekwa na sheria hii. Hivyo hivyo, uchambuzi wa sheria ndogo unaofanywa na Kamati sambamba na Bunge linapojadili Taarifa hii pia huzingatia vigezo vilivyobainishwa katika masharti ya sheria hii.

### 1.3.3 Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika,** Chimbuko la Kanuni za Kudumu za Bunge ni Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kanuni hizi zinaweka utaratibu wa kutekeleza Shughuli za Bunge. Utaratibu huo ni kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Shughuli za Bunge, Sekretarieti ya Bunge na Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Sheria Ndogo inayoripoti shughuli zake leo.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Bunge zinafafanua muundo na utaratibu wa utekelezaji wa majukumu na mamlaka ya Bunge na Kamati zake zinazojumuisha Kamati hii. Aidha, Kanuni hizo zinabainisha masharti mbalimbali kuhusu uendeshaji wa shughuli

za Bunge na Kamati zake. Naomba kulihakikishia Bunge lako kwamba, shughuli zote zinazoripotiwa katika taarifa hii zinatokana na masharti yaliyowekwa katika Kanuni za Bunge.

### 1.4 Njia Zilizotumika Katika Kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge inaweka sharti la kila taarifa ya Kamati ya Bunge inayowasilishwa Bungeni kubainisha njia zilizotumika katika kutimiza majukumu yake. Kwa kuzingatia sharti hilo, Taarifa hii inaeleza njia ambazo Kamati ilitumia kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni: -

(i) Mapitio ya matoleo ya Magazeti ya Serikali yaliyowasilishwa Bungeni kwa kipindi kinachoripotiwa katika Taarifa hii. Mbinu hii iliwezesha Kamati kuandaa orodha na jumla ya sheria ndogo zote zilizotangazwa kwenye Magazeti hayo. Aidha, kupitia mbinu hiyo Kamati ilibaini mwelekeo na wigo wa shughuli ya uchambuzi wa sheria ndogo pamoja na kubaini sekta zinazohusika na sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni;

(ii) Uchambuzi wa awali wa sheria ndogo ili kubaini masharti yanayowekwa na sheria hizo. Mbinu hiyo, ililenga kufanya tathmini ili kuona namna sheria ndogo zilivyozingatia masharti ya Katiba, sheria mama na sheria zingine za nchi;

(iii) Uhakiki wa mtiririko wa maudhui ukilinganishwa na masharti yanayowekwa katika sheria ndogo. Mbinu hii ilifanikisha kubaini iwapo kuna ukamilifu uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukabidhi madaraka ya ufafanuzi uliotakiwa kufanywa na sheria ndogo inayohusika;

(iv) Uoanishaji wa masharti ya sheria ndogo inayohusika na misingi iliyowekwa katika Katiba na sheria nyingine za nchi. Lengo ni kujiridhisha na namna sheria ndogo inavyozingatia misingi ya sheria za nchi;

(v) Kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu sheria ndogo. Njia hii ilidhamiria kushirikisha wanaolengwa na sheria

ndogo ili kupata mtazamo wao kuhusu masuala mbalimbali, hatimaye kuiwezesha Kamati kuchambua kwa kina sheria ndogo; na

(vi) Mahojiano na mamlaka zilizotunga sheria ndogo kwa idhini ya Bunge. Mbinu hii ililenga kuiwezesha Kamati kupima uthabiti wa hoja dhidi ya ufafanuzi wa mamlaka zinazohusika, jambo linalosaidia kuiwezesha Kamati kuwa na mapendekezo ya maazimio ya Bunge yanayotekelezeka.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulihakikishia Bunge lako kuwa, njia zilizotumika wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati zimesaidia kubainika kwa mambo mbalimbali yanayojenga maoni ya Kamati ambayo ni msingi wa Maazimio ya Bunge yanayopendekezwa katika taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka 2024, zinahusu utekelezaji wa majukumu ya msingi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Shughuli hizo kwa ujumla zinaainishwa kwa kujumuishwa katika maeneo mawili ambayo ni:

(i) Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba; na

(ii) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye, Mkutano wa Kumi na Mbili, Mkutano wa Kumi na Tatu, Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi Tano.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo za Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano

yaliwasilishwa Bungeni katika Taarifa ya Kamati mnamo tarehe 4 Septemba, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge. Katika Taarifa hii matokeo ya Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba, yanaripotiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo za Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Tatu wa Bunge yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita tarehe 4 Septemba, 2024. Taarifa hii inaripoti Matokeo ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi Nne na Mkutano wa Kumi na Tano.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati zinazoripotiwa zimetokana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1. Aidha, utaratibu uliotumika umefuata masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hivyo, shughuli zinazoripotiwa zinalisaidia Bunge kuwajibika katika utekelezaji wa shughuli zake kwa lengo la kuhakikisha kwamba, sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa kama inavyoelekeza katika Ibara ya 9 (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.1.1 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa na Matokeo Kuripotiwa Bungeni

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Januari 2024 hadi Agosti 2024, Serikali iliweka Mezani Bungeni Magazeti yaliyotangaza sheria ndogo. Jumla ya sheria ndogo thelathini na nane (38) zilichambuliwa na matokeo yake yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na maazimio yaliyolenga kurekebisha dosari yalitolewa na kupitishwa na Bunge. Naomba kuthibitisha kuwa mjadala wa Bunge ulikuwa na tija kwa wananchi na wapo waliopongeza kupitia vyombo vya Habari, warsha na makongamano mbalimbali.

**2.1.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ambao Matokeo Yake Yaliripotiwa Bungeni**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Bunge ndilo lenye dhamana ya kuweka sheria za nchi zinazowezesha ustawi wa wananchi, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyolenga kuweka sawa masharti ya kisheria nchini. Kwa kipindi cha Januari 2024 hadi Agosti 2024, Kamati ilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa dosari katika jumla ya sheria ndogo ishirini na mbili (22) zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mbili na Mkutano wa Kumi na Tatu. Maazimio yote kuhusu Sheria Ndogo hizo yalitekelezwa. Sheria ndogo hizo zilikuwa chini ya Wizara Tisa ambazo ni: -

(i) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa dosari mbili (02);

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliyokuwa na sheria ndogo mbili (02) zilizobainika kuwa na dosari sita (06);

(iii) Wizara ya Kilimo iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) zilizobainika kuwa dosari kumi na sita (16);

(iv) Wizara ya Uchukuzi iliyokuwa na sheria ndogo sita (06) zilizobainika kuwa dosari thelathini (30);

(v) Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliyokuwa na sheria ndogo mbili (02) zilizobainika kuwa dosari kumi na mbili (12);

(vi) Wizara ya Maji iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa dosari moja (01);

(vii) Wizara ya Nishati iliyokuwa na sheria ndogo tatu (03) zilizobainika kuwa dosari ishirini na nne (24);

(viii) Wizara ya Fedha iliyokuwa na sheria ndogo nne (04) zilizobainika kuwa dosari kumi na nane (18); na

(ix) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyokuwa na sheria ndogo mbili (02) zilizobainika kuwa dosari tisa (09).

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu huo ulilіweka Bunge katika nafasi yake ya kusimamia utekelezaji wa madaraka ya kuweka sheria ndogo yaliyokabidhiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini. Kamati itaendelea kuutumia utaratibu huo ili kulisaidia Bunge katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**2.1.3 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kimeweka sharti kwa sheria ndogo zote zinazotangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita za vikao vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapisha toleo la Gazeti lililotangaza sheria ndogo hizo. Sheria ndogo zilizotangazwa kwenye Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba zipo chini ya Wizara tisa (09) zifuatazo: -

(i) Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira;
(iii) Wizara ya Viwanda na Biashara;
(iv) Wizara ya Uchukuzi;
(v) Wizara ya Fedha;
(vi) Wizara ya Katiba na Sheria;
(vii) Wizara ya Maliasili na Utalii;
(viii) Wizara ya Afya; na
(ix) Wizara ya Ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua sheria ndogo hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 10 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Matokeo ya uchambuzi huo yanaripotiwa

katika Taarifa hii ili kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi bayana unaohusu dosari zilizobainika wakati wa uchambuzi. Ufafanuzi wa matokeo hayo unapatikana katika **kipengele cha 2.2.**

**2.1.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ambao Matokeo yake Hayajaripotiwa Bungeni**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano, ambao matokeo yake hayajaripotiwa, unahusu sheria ndogo thelathini na nane (38). Maazimio kuhusu sheria ndogo hizo yalitolewa katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa tarehe 4 Septemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia kuwa Kamati ya Sheria Ndogo ni nyenzo ya Bunge ya kufuatilia utekelezaji wa madaraka ya kuweka sheria ndogo yanayokabidhiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Matokeo ya uchambuzi huo yanafafanuliwa katika **kipengele cha 2.3** cha Taarifa hii.

**2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa sheria ndogo hamsini na nne (54) zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba umefanyika kwa lengo la kufanikisha wajibu wa Bunge kudhibiti mamlaka yake ya kutunga sheria za nchi. Kwa desturi za uendeshaji wa Bunge letu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imekuwa karakana muhimu ya Bunge lako ambapo wajibu wa udhibiti wa sheria ndogo huanza kutekelezwa. Dhima kuu ya Kamati wakati wa uchambuzi ni kubainisha dosari na baadaye kulishauri Bunge kuhusu hatua muhimu za kuchukua.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mantiki hiyo, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo ni muhimu kuwasilishwa Bungeni ili iwe rahisi kwa Bunge kudhibiti madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine serikalini. Ninaomba kulihakikishia Bunge lako kuwa, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo yanayowasilishwa kupitia taarifa hii, yamemeng'enywa ili kuliwezesha Bunge kupima kuhusu hatua stahiki za kuchukua dhidi ya dosari zinazobainishwa. Kwa urahisi wa kufuatilia, Jedwali la Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba limeambatishwa. Jedwali hilo linachanganua sheria ndogo zenye dosari mbalimbali kama ifuatavyo: - (i) Dosari mbili (02) ya kukinzana na masharti ya Katiba;

(ii) Dosari mbili (03) za kukinzana na masharti Sheria Mama na sheria nyingine za nchi;

(iii) Dosari thelathini na tano (34) za kuweka na masharti yasiyo na uhalisia katika utekelezaji;

(iv) Dosari thelathini na tisa (39) za kutoendana na misingi ya uandishi; na

(v) Dosari kumi na saba (17) za uandishi wa Majedwali.

**Mheshimiwa Spika**, Dhumuni la sheria ndogo ni kutoa ufafanuzi na kutekeleza masharti yaliyowekwa na sheria ya Bunge. Hivyo, kuwepo na dosari au hitilafu zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati, zinaweza kukwamisha lengo la Bunge kuhusu utekelezaji wa sheria ya Bunge. Kwa msingi huo, Bunge halitarajiwi kuendelea na utungaji wa sheria zake pasipo kuelekeza kufanyika kwa marekebisho ya dosari zilizopo katika sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa minajili hiyo, ili Bunge liweze kufanya uamuzi ulio na tija, sehemu hii ya taarifa inaweka bayana mifano ya dosari zilizobainika wakati wa uchambuzi kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya nchi ndiyo Sheria Kuu na inapaswa kuzingatiwa na sheria zote nchini. Ibara ya 64(5) ya Katiba inaelekeza kuwa Sheria zote zinazotungwa hazipaswi kukiuka masharti ya Katiba. Hali kadhalika, sheria ndogo ambayo ni sehemu ya sheria za nchi inayofafanua sheria ya Bunge, pia haitarajiwi kukiuka masharti yaliyowekwa na Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kujiridhisha na msingi wa kutokuwa na sheria zinazokiuka masharti yaliyowekwa na Katiba, Kamati ilichambua sheria ndogo kwa kulinganisha maudhui yake na masharti yaliyomo katika Katiba. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa, zipo baadhi ya sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na vifungu vyenye maudhui yanayokiuka masharti Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa sheria ndogo hizo ni, **Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, 2024 (TS Na. 266 la 2024).** Kifungu cha 5 kinaweka wajibu kwa kila mfugaji chini ya sheria ndogo hii. Kifungu cha 5 (h) kinaweka wajibu kwa mfugaji kutokaribisha wafugaji wengine bila kibali cha Halmashauri. Wajibu huo haujaonesha unalenga kuzuia wafugaji kukaribishwa wakiwa na mifugo yao, badala yake umezuia kwa ujumla kukaribishwa kwa mfugaji bila kibali cha Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati unaona wajibu huo ukibaki kama ulivyo kwa kuweka sharti la kukaribisha mfugaji kwa sharti la kuomba kibali, pasipo kuonesha sharti la kibali kuwa ni kwa mfugaji anayekuja na mifugo yake, ni kana kwamba unakiuka haki na uhuru wa wananchi kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo jingine.

**Mheshimiwa Spika,** mfano mwingine wa sheria ndogo iliyobainika kuwa na masharti yanayokiuka Katiba ni **Kanuni za nidhamu kwa Wanafunzi, 2024 (TS Na. 365 la 2024)**. Kanuni ya 23(3) inahusu

Mwanafunzi (Mtuhumiwa) kutokuwepo wakati wa kusikilizwa kwa shauri la nidhamu. Kanuni inaruhusu kuendelea kusikilizwa kwa shauri, pasipo kuzingatia sababu za msingi zinazoweza kusababisha mwanafunzi huyo kutohudhuria kikao hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 13(6)(a) ya Katiba inaelekeza kwamba wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu. Kamati inaona kwamba, masharti yaliyowekwa na **Kanuni ya 23(3)** yanakiuka haki ya mtu kusikilizwa kwa mujibu wa Katiba, hali inayoweza kusababisha kutumiwa vibaya na wenye mamlaka dhidi ya mwanafunzi huyo, jambo ambalo linakinzana na sifa ya sheria bora ya kuzuia unyanyasaji, kulinda wanyonge na kusimamia usawa na haki za binadamu.

**2.2.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge linapotunga sheria zake huweka vifungu vinavyozielekeza mamlaka nyingine kutunga sheria ndogo ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge. Maelekezo ya Bunge huwa ni kwa kutaja maeneo mahsusi ambayo sheria ndogo inapaswa kuakisi au kuwezesha utekelezaji wa jumla ya masharti ya sheria ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa sheria ya Bunge kupitia sheria ndogo, Sheria ya Tafsiri ya Sheria inaweka misingi ya uandishi, tafsiri, matumizi na mambo mengine muhimu kuhusu sheria za nchi kwa ujumla. Kifungu cha 36 (1) cha sheria hiyo, kimeweka masharti yanayokataza sheria ndogo kwenda kinyume na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Kwa kuzingatia masharti hayo ambayo Kamati huyatumia kama rula ya kuweka unyoofu wa sheria ndogo, Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo makuu yafuatayo: -

(i) Ulinganifu wa malengo ya sheria ndogo ya yale ya sheria inayotekelezwa;

(ii) Ulinganifu wa adhabu za sheria ndogo na sheria inayotekelezwa;

(iii) Ulinganifu wa taratibu zinazowekwa na sheria ndogo na sheria inayotekelezwa; na

(iv) Ulinganifu wa lugha iliyotumika katika sheria ndogo na madhumuni ya sheria inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi yanayoripotiwa leo yanaonesha, baadhi ya sheria ndogo kuwa zina masharti yanayokinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi. Mfano wa sheria hizo ni **Kanuni za Uwindaji wa Kitalii (Tangazo la Serikali Na. 780 la mwaka 2024)**. Kanuni ya 14(8) ya Kanuni hizi inataja adhabu kwa mtu yeyote atakayewasilisha taarifa za uongo wakati wa kuomba kibali au leseni. Adhabu kwa kosa hilo ni kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi milioni tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au vyote.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwango cha juu cha adhabu ya kifungo cha miaka mitatu kinachowekwa na sheria ndogo hii kinakinzana na kiwango cha juu cha kifungo kilichowekwa na kifungu cha 105 cha sheria mama ambacho ni miaka mitano. Ukinzano huo ni kinyume na masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria lakini pia ni kinyume na azma ya sheria ya Bunge kuhusu adhabu kwa mtu yeyote atakayewasilisha taarifa za uongo wakati wa kuomba kibali au leseni. Kwa mantiki hiyo adhabu iliyowekwa inaathiri uhalali wa kifungu hiki kwa kuwa unavuka mamlaka yake na kuingia katika ubatili.

### 2.2.3 Dosari ya Kuweka Masharti Yasiyo na Uhalisia

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na masuala mengine, uandishi wa sheria hulenga kuweka masharti mbalimbali ambayo zao la utekelezaji wake ni kushughulikia, kufanikisha au kutatua jambo fulani miongoni mwa wanaolengwa na masharti yanayohusika.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa Kamati yanabainisha masharti yaliyowekwa na sheria ndogo ambayo utekelezaji wake hauna uhalisia ikilinganishwa na lengo la sheria ndogo. Dosari hiyo imebainika katika **Sheria ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, 2024 (TS Na. 815 la mwaka 2024).** Matokeo ya uchambuzi ya sheria ndogo hii yalibaini dosari hiyo katika Jedwali la Tatu la sheria ndogo inayoonesha mfano wa kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuweka sharti la kuomba kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi kwa ajili ya biashara kibali hicho pia kimetaja wahusika wanaopaswa kuomba kibali cha kusarifisha mazao ya uvuvi ikiwemo samaki kwa matumizi ya nyumbani. Kwa mantiki ya masharti hayo, mwananchi yeyote aliye katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ambaye atahitaji kupata samaki kwa matumizi ya nyumbani atapaswa kuomba kibali cha kusafirisha samaki hao. Masharti haya hayana uhalisia katika utekelezaji wake na yanaweza kutafsirika kuwa ni kero kwa wananchi wanaonunua na kusafirisha mazao hayo kwa matumizi ya nyumbani.

**Mheshimiwa Spika,** dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia ambayo utekelezaji unaweza kuleta changamoto yameonekana pia katika **Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia Kwenda Nje ya Nchi (TS Na. 807 la mwaka 2024).** Dosari inayobainishwa na Kamati ipo katika **Kanuni ya 9** ambayo inahusu muda wa matumizi ya Kanuni kuwa ni ndani ya kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe ya kuchapishwa sheria ndogo katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia muda uliowekwa na Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia Kwenda Nje ya Nchi kuhusu matumizi yake**, Kanuni ya 9(2)** inaweka katazo la kusafirisha venia baada ya miaka miwili ya matumizi ya Kanuni kumalizika. Kamati iliona kwamba, Kanuni haijaweka mazingira yatakayowezesha ruhusa ya kusafirisha venia nje ya nchi baada ya kumalizika kwa muda wa miaka miwili ya matumizi ya Kanuni kwa wasafirishaji ambao tayari walikua wameanza mchakato wa usafirishaji ilhali

ukomo wa miaka miwili umewakuta hawajamaliza zoezi la usafirishaji wa venia.

**Mheshimiwa Spika,** katazo la kusafirisha venia ndani ya miaka miwili pasipo kuweka mazingira yanayotambua wasafirishaji ambao walianza mchakato wa usafirishaji ambao haujaisha ndani ya miaka miwili linaweza kumuathiri msafirishaji mwenye sababu ya msingi ambaye amezidi miaka miwili kwa mujibu wa masharti ya kanuni. Aidha, masharti ya miaka miwili ya kutumika kwa kanuni ni kama hayana uhalisia kwa utaratibu wa ufanyaji wa biashara.

### 2.2.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, sheria hutungwa kwa ajili ya kufanikisha jambo au mambo mahsusi yaliyokusudiwa na sheria inayohusika. Ili kufikia lengo lililokusudiwa, sheria hupaswa kuwa na maudhui yanayoeleweka, kuwa na masharti yanayolengwa kuwepo katika sheria inayohusika; na kuwa na ukamilifu wa kimaudhui. Uzingatiaji wa misingi hiyo ni kuwezesha sheria kueleweka na kutekelezeka kwa urahisi na wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri sheria hizo. Ili kujiridhisha na uzingatiaji wa misingi ya uandishi wa sheria inayowekwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kamati ilitaka kujiridhisha na masuala kama vile: -

(i) Iwapo sheria inayotoa mamlaka ya kuwa na sheria ndogo inayohusika imerejewa inavyostahili;

(ii) Iwapo Mamlaka iliyoweka sheria ndogo inayohusika imebainishwa;

(iii) Iwapo makosa ya uandishi yanahusu kutokidhi haja ya sheria mama;

(iv) Iwapo imejumuisha mambo mahimu iliyopaswa kuyaweka;

(v) Iwapo imebainisha namna ya utekelezaji wa masharti ya vifungu vya sheria ndogo; na

(vi) Iwapo imeweka kwa usahihi tarakimu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati unaoripitiwa katika taarifa hii unabainisha dosari za sheria ndogo kutozingatia masharti ya uandishi. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni **Kanuni za Uwindaji wa Kitalii, 2024 (TS Na. 780 la mwaka 2024).**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unabainisha dosari katika Kanuni ya 29(4)(b) inayotaja adhabu ya kuwinda simba aliye chini ya umri wa miaka minne. Kamati imebaini dosari ya uandishi katika Kanuni ya 29(4(b)(i), (ii) na (iii) ambazo kwa pamoja zinaweka adhabu moja ya faini ya shilingi milioni tano kwa makosa yasiyofanana. Makosa hayo ni kuwinda simba chini ya umri wa miaka minne faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya kwanza ya utendaji wa kosa; faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya pili ya utendaji wa kosa; au faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya tatu ya utendaji wa kosa.

**Mheshimiwa Spika,** makosa ya uandishi yanayobainishwa na Kamati katika sheria ndogo hii yana athari ya kukosesha uwiano wa haki (*proportional justice*) kutokana na kutozingatia muktadha wa makosa ikilinganishwa na adhabu stahiki. Aidha, makosa hayo ya uandishi wa adhabu ni kana kwamba yanalenga kuchochea utendaji wa makosa ya uwindaji kwa kutoa adhabu ndogo kwa kadiri mtenda kosa anavyorudia kutenda kosa linalofanana kwa mara nyingi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** dosari ya uandishi pia ilibainika katika Sheria ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa (TS Na. 811 la mwaka 2024). Sehemu G (II) ya Jedwali la Kwanza inahusu ada na ushuru wa kuendesha shughuli za michezo ya kubahatisha. Uchambuzi wa Kamati umebaini Sehemu G (II) imeweka ada ya Mashine ya kubetisha au gulugulu kuwa ni shilingi 30,000 ambayo utaratibu wake wa utozaji umewekwa kwa vipindi viwilli tofauti yaani, kwa mwaka na kwa mwezi. Makosa ya

uandishi kwa kuweka vipindi viwili tofauti vya ukusanyaji wa ada unatatiza watekelezaji wa sheria kuhusu kipindi kinachokusudiwa hali inayoweza kuathiri malengo ukusanyaji wa ada na ushuru yaliyokusudiwa na sheria ndogo.

### 2.2.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Tafsri ya Sheria, Jedwali ni sehemu ya sheria hivyo linastahili kuwa na misingi inayofanikisha lengo la sheria. Jedwali hutoa ufafanuzi zaidi wa vifungu vya sheria, kwa msingi huo dosari katika uandishi wa majedwali ina athari kwa kifungu kinacholianzisha. Kwa mantiki hiyo, Bunge linapofuatilia sheria ndogo huangazia majedwali katika sheria hizo ili kujiridhisha na masuala mbalimbali yanayoweza kuathiri tija ya sheria ndogo yenyewe sambamba na sheria ya Bunge. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kujiridhisha na mambo yafuatayo: -

(i) Iwapo Kifungu wezeshi cha Jedwali hilo kimerejewa na kuoneshwa; na

(ii) Iwapo Jedwali linatoa ufafanuzi uliokamilika.

**Mheshimiwa Spika,** dosari ya uandishi wa majedwali katika sheria ndogo imebainika katika sheria ndogo za **The Law School of Tanzania (Students General Welfare, Conduct and Disciplinary Matters) Rules, 2024 (TS Na. 615 la mwaka 2024). Dosari ya uandishi ilibainika katika** Jedwali la Pili lilonahusu Kanuni za mavazi kwa wanafunzi. Jedwali la Pili linaweka adhabu inayomtaka Mwanafunzi atakayekiuka kanuni za mavazi kutakiwa kurudi nyumbani kubadilisha mavazi aliyovaa.

Uchambuzi umebaini kasoro ya uandishi ambapo maelezo kuhusu sharti la mwanafunzi kurejea nyumbani hayajawekewa kifungu na wala hayapo ndani ya Jedwali linalohusika. Hali hiyo inasababisha maelezo hayo kukosa nguvu ya kisheria lakini pia, changamoto ya kufanya rejea kuhusu sehemu yanapopatikana masharti hayo.

**2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nne na Mkutano wa Kumi na Tano**

**Mheshimiwa Spika,** Katika misingi ya utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge, upo wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo kwa niaba ya wananchi. Kwa desturi ya kibunge, Kamati za Bunge ni nyenzo muhimu ya kuliwezesha Bunge kutoa picha halisi ya utekelezaji uliofanyika. Naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati imefuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano. Ufuatiliaji huo ulifanyika kwa kuchambua taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa tarehe 4 Septemba, 2024 wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio uliangalia hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio hayo katika jumla ya sheria ndogo thelathini na nane (38). Uangaliaji na ufuatiliaji wa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji ulidadisi mambo manne yafuatayo: -

(i) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio;

(ii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(iii) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali; na

(iv) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kufafanua hatua zilizofikiwa pamoja na kubainisha Wizara zinazohusika katika utekelezaji wa Maazimio

ya Bunge. Lengo la ufafanuzi huu ni kuliwezesha Bunge kubaini hatua ya utekelezaji wa maazimio yake na kufanya uamuzi stahiki. Naomba kubainisha Wizara Sita (06) zilizohusika na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Fedha iliyokuwa na sheria ndogo mbili (02) zilizobainika kuwa na dosari kumi na tatu (13);
(ii) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa na dosari tano (05);
(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenyeulemavu iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa na dosari moja (01);
(iv) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliyokuwa na sheria ndogo ishirini na nne (24) yenye dosari sabini na moja (71);
(v) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa na dosari nne (04); na
(vi) Wizara ya Uchukuzi iliyokuwa na sheria ndogo tisa (09) iliyobainika kuwa na dosari thelathini na tano (35).

**Mheshimiwa Spika,** Hatua zilizofikiwa na Wizara zilizotajwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano). Pamoja na Jedwali hilo, kwa ajili ya kuwezesha majadiliano ya Bunge juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua zilizofikiwa kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki na kutangazwa

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Rasimu ya Marekebisho iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ni hatua muhimu ya kushughulikia maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa dosari iliyobainika.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji unabainisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo uliofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki ili zitangazwe katika Gazeti la Serikali. Uchambuzi umebainisha kwamba, hadi wakati Kamati ilipokutana na Wizara zinazohusika, ni sheria ndogo mbili (02) tu, zilizokuwa na hoja zilizofika hatua hii. Wizara zinazohusika na sheria ndogo hizo ni: -

(i) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) ambayo ni *Regulations under the Atomic Energy (Protection from Ionizing and Non-Ionizing Radiation) (Amendments) 2023* yenye jumla ya hoja nne (04); na

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) ya *the social Security Schemes (Use of Member's Benefits Etitlements (Collateral for Home Mortgage) (Amendments), 2024* iliyokuwa na hoja moja (01).

**2.3.2 Hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yoyote ya sheria ndogo hayawezi kuanza kutekelezwa kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Tathmini iliyofanywa na Kamati kupitia taarifa zilizowasilishwa imeonesha kwamba, hadi tarehe 24 Januari, 2025, sheria ndogo thelathini na sita (36) zilikua zimefikia hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Naomba kuzitambua Wizara zinazohusika na sheria ndogo hizo kama ifuatavyo: -

(i) Wizara ya Fedha iliyotangaza marekebisho ya Kanuni mbili(02) katika Gazeti la Serikali ambazo ni:-

a) *The Accountants and Auditors (Appeals Board) (Amendment) Rules, 2024* kupitia Tangazo la Serikali Na. 469/2024 la tarehe 14/6/2024; na

b) *The Banking and Financial Institutions (Compulsory Liquidation) (Amendment) Regulations, 2024* kupitia Tangazo la Serikali Na. 1077 la tarehe 20/12/2024.

(i) Wizara ya Viwanda na Biashara iliyotangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 870 la tarehe 18/10/2024 imefanya marekebisho ya hoja moja (01) kupitia The *College of Business Education (Examinations) (Amendments) Rules*, 2024;

(ii) Wizara ya Uchukuzi iliyotangaza marekebisho katika sheria ndogo tisa (09) katika Gezati la Serikali. Sheria ndogo hizo ni:

a) *The Civil Aviation (Heliports)(Amendments), Regulations, 2024* kupitia Tangazo la Serikali Na. 2 la tarehe 5 Januari, 2024;

b) *The Civil Aviation (Operation of Aircraft - Helicopter Operations) (Amendments) Regulations, 2024* Tangazo la Serikali Na. 3 la tarehe 5 Januari, 2024;

c) *The Civil Aviation (Certification, Licensing and Registration of Aerodromes) (Amendments), Regulations, 2024* Tangazo la Serikali Na. 5 la tarehe 5 Januari, 2024;

d) *The Civil Aviation (Instruments and Equipment) (Amendments) Regulations ,2024* Tangazo la Serikali Na. 6 la tarehe 5 Januari, 2024;

e) *The Civil Aviation (Aerodrome Design and Operations) (Amendments) Regulations, 2024*

Tangazo la Serikali Na. 7 la tarehe 5 Januari, 2024;

f) *The Civil Aviation (Facilitation of Air Transport) (Amendments) Regulations, 2024* Tangazo la Serikali Na. 8 la tarehe 5 Januari, 2024;

g) *The Land Transport Regulatory Authority (Terms and Conditions for Provision of Regulated Services) (Amendments, Rules, 2024* Tangazo la Serikali Na. 15 la tarehe 12 Januari, 2024;

h) *Rules under the Land Transport Regulatory Authority*
*(Complaint Handling Procedures), 2024* Tangazo la
Serikali Na. 16 la tarehe 12 Januari, 2024; *na*

i) *Regulations under The Railways (Open Access), 2024* Tangazo la Serikali Na. 213.

(iii) Ofisi ya Rais TAMISEMI iliyotangaza marekebisho ya sheria ndogo ishirini na nne (24) katika Gazeti la Serikali ambazo ni: -

a) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmshauri ya Wilaya ya Geita ya Mwaka 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 24 la tarehe 17 Januari, 2025;

b) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2023 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 436 la tarehe 31 Mei, 2024;

c) Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 25 la tarehe17 Januari, 2025;

d) Sheria Ndogo ya (Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 439 la tarehe 31 Mei, 2024;

e) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 26 la tarehe 17 Januari, 2025;

f) Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, 2023 iliyotangazwa Gazeti la Serikali Na. 27 la tarehe 17 Januari, 2025;

g) Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, 2023 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 28 la tarehe 17 Januari, 2025;

h) Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, 2023 iliyotangazwa Gazeti la Serikali Na. 32 la tarehe 17 Januari, 2025;

i) Sheria Ndogo Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, 2023 ilitangazwa Gazeti la Serikali Na. 29 la tarehe 17 Januari, 2025;

j) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 438 la tarehe 31 Mei, 2024;

k) Sheria Ndogo ya Kuzuia Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 ilyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 434 la tarehe 31 Mei, 2024;

l) Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, 2023 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 30 la tarehe 17 Januari, 2025;

m) Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, 2023 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 31 la tarehe 17 Januari, 2025;

n) Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 859 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

o) Sheria Ndogo ya (Usafi Wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 860 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

18 Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Mji Mafinga, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 865 la tarehe Oktoba, 2024;

p) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Mafinga, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 866 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

18 Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 864 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

q) Sheria Ndogo ya Mji wa Kihistoria wa Mikindani na Maeneo mengine ya Urithi yaliyohifadhiwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Mikindani, 2024 iliyotangazwa Gazeti la Serikali Na. 862 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

18 Sheria Ndogo ya Kilimo na Usalama wa Chakula za Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani la 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 863 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

r) Sheria Ndogo ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 861 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

s) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida, 2024 iliyotangazwa Gazeti la Serikali Na. 869 la tarehe 18 Oktoba, 2024;

t) Sheria Ndogo ya Usafi na Kuhifadhi Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 868 la tarehe 18 Oktoba, 2024; na

u) Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, 2024 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 867 la tarehe 18 Oktoba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** hatua ya kutangaza marekebisho ya sheria katika Gazeti la Serikali ni ya juu kabisa na inayoonesha kufanyia kazi maazimio ya Bunge kwa ukamilifu. Wizara zilizofika hatua hii ni za kupongezwa kwa kuondoa dosari mbalimbali zilizobainika katika sheria zinazohusika, hivyo kupunguza kero kwa

wanaoguswa moja kwa moja, kuondoa mkwamo wa utekelezaji wa sheria ndogo zenyewe pamoja na sheria mama. Hatua hii ni budi kufikiwa na Wizara nyingine ambazo bado zipo hatua za nyuma za utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

### 2.3.3 Kutotekelezwa kwa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilipoazimia kuhusu kuzitaka mamlaka zinazohusika na sheria ndogo kutekeleza maazimio yake lililenga kuondosha dosari zinazoweza kukwamisha dhamira ya sheria mama, kuleta kero kwa wananchi na kutatiza utekelezaji wake. Kamati imebaini baadhi ya hoja zilizopatiwa Maazimio ya Bunge hazijatekelezwa kutokana na michakato na hatua mbalimbali zinazopaswa kufuatwa ili kufanya marekebisho ya sheria kama yalivyoazimiwa na Bunge. Sheria ndogo zilizo katika hatua hiyo ni mbili zilizo chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, ambazo ni: -

a) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, 2024 ambayo haijatekeleza hoja nne (04) zilizoazimiwa na Bunge; na

b) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida, 2024 ambayo haijatekeleza hoja tatu (03) zilizoazimiwa na Bunge ili zifanyiwe marekebisho

**Mheshimiwa Spika,** kutokutekelezwa kwa maazimio kwa maeneo yalibainika kuwa na dosari ni kuendeleza changamoto ambazo zinaweza kukwamisha utekelezaji mzuri wa sheria ndogo hivyo kukwamisha malengo yaliyokusudiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati hii imepewa majukumu ya kuchambua sheria ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa

na masharti ya Katiba, sheria inayotekelezwa na sheria ndogo inayohusika pamoja na sheria nyingine za nchi. Kamati imechambua kwa kuzingatia vigezo hivyo ambapo kupitia uchambuzi unaofanywa na Kamati, Bunge huutumia katika kusimamia matumizi ya madaraka yake ya kutunga sheria iliyoyakabidhi kwa mamlaka nyingine ili kutunga sheria ndogo.

### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sheria ndogo kwa kiasi kikubwa zinanagusa shughuli mbalimbali za maisha ya kila siku ya wananchi walio wengi. Ninaliomba Bunge lako liyasome, kuyatafakari na hatimaye lipokee mapendekezo yote yaliyomo katika Taarifa hii na hatimaye liyaazimie. Ili kuliwezesha Bunge kufikia uamuzi wa kuazimia mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa mtazamo wa Kamati unaotokana na uchambuzi kama ifuatavyo: -

#### 3.2.1 Dosari ya Sheria Ndogo kuwa na Masharti Yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio sheria kuu inayoweka majukumu ya mihimili ya dola na kuweka misingi ya mbalimbali inayotungiwa sheria na vyombo mbalimbali ili kufanikisha masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Inatarajiwa kwamba, sheria ndogo zinazotungwa zinakuwa na maudhui yenye kuendana na misingi iliyowekwa na Katiba ili kufanikisha malengo mapana ya kikatiba. Sheria ndogo inapokinzana na Katiba ni jambo lisilovumilika na Bunge kwakuwa linaweza kuwa kikwazo katika ustawi wa wananchi kijamii, kiuchumi na kisiasa.

#### 3.2.2 Dosari ya Sheria Ndogo kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Bunge linapotunga sheria yake huweka kifungu mahsusi kinachokasimu mamlaka yake ya kutunga sheria kwa Waziri, mtu au taasisi. Lengo la kufanya hivyo ni kurahisisha utekelezaji wa sheria ya Bunge (mama). Ikiwa sheria ndogo

inayotungwa kwa minajili ya kuwezesha sheria ya Bunge imeweka maudhui yanayokinzana na sheria ya Bunge ni dhahiri kwamba lengo la sheria ya Bunge haliwezi kufikiwa.

Kamati ina maoni kwamba, sheria ndogo zote zilizobainika kukinzana na masharti yaliyowekwa na sheria mama au sheria nyingine za nchi zinapaswa kuangaliwa kwa chijo angavu ili kuondoa dosari za kukinzana na sheria.

### 3.2.3 Sheria Ndogo Kuwa na Masharti Yasiyozingatia Uhalisia

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ndogo zenye Masharti yasiyozingatia uhalisia zinaweza kukwamisha malengo ya Bunge kutunga sheria mama inayohusika. Ni maoni ya Kamati kuwa, zaidi ya kukwamisha malengo ya sheria mama, sheria ndogo zenye dosari hiyo zinaweza kusababisha kero kwa Wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kuona madaraka yake yanayokabidhiwa kwa mamlaka nyingine hayatumiki kusababisha kero kwa wananchi.

### 3.2.4 Dosari ya Sheria Ndogo Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Ufasaha katika uandishi wa sheria hufanikisha kueleweka kwa sheria ndogo inayohusika. Aidha, huweka maudhui yenye tafsiri inayokusudiwa na sheria inayohusika. Ni mtazamo wa Kamati kuwa, sheria ndogo zilizo na makosa ya uandishi kama vile kuruka au kutojumuisha maudhui yaliyopaswa kuwemo katika sheria, kukosea tarakimu kama vile katika viwango vya ada, ushuru na tozo mbalimbali, kuweka maudhui yenye kutatiza uelewekaji (*ambiguous contents*) zinaweza kuondoa maana iliyokusudiwa na kuzuia kufanikiwa kwa malengo ya sheria mama au sheria ndogo inayohusika.

### 3.2.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika**, Majedwali ni sehemu ya sheria ambayo husomwa kwa pamoja na vifungu vinavyohusika kwa ajili ya

kukamilisha madhumuni ya kifungu kinachohusika. Kamati ina maoni kuwa, misingi ya uandishi wa majedwali isipozingatiwa ipasavyo, ni jambo linaloweza kutatiza ukamilifu wa vifungu vya sheria ndogo kwa jumla. Hali hiyo itaathiri utekelezaji wa sheria ndogo yenyewe halikadhalika sheria ya Bunge.

### 3.2.6 Utekelezaji wa Maazimio Yanayohusu Kurekebisha Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, Uamuzi wowote hutokea baada ya uchambuzi na tafakuri ya kina kuhusu jambo linalotarajiwa kutolewa uamuzi. Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo yalitokana na tafakuri kuhusu dosari zilizobainika wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo. Kwa kuzingatia uzito wa maazimio ya Bunge, ilitarajiwa Mamlaka zinazohusika kuwa zimetekeleza maazimio hayo haraka. Ni maoni ya Kamati kwamba, kutofikia hatua ya kutangaza marekebisho ya maazimio ya Bunge ni kuendeleza madhara yanayotokana na dosari za sheria ndogo.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Mapendekezo ya Kamati ni maoni yake yaliyotokana na shughuli zinazoripotiwa katika Taarifa hii. Shughuli hizo zimebainisha uchambuzi na yatokanayo na uchambuzi huo. Kutokana na matokeo ya uchambuzi, Kamati inazingatia masharti ya Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge kuhusu mfumo wa maneno kwenye mapendekezo yake na kuliomba Bunge lijadili Taarifa hii na kupitisha maazimio kama ifuatavyo: -

### 3.3.1 Sheria Ndogo Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Katiba

**KWA KUWA**, Baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya katiba, na hivyo kuwa kinyume na misingi ya sheria inayotambua Ukuu wa Katiba,

**NA KWA KUWA**, Ukiukwaji wa masharti ya Katiba kwa sheria ndogo yoyote au sheria ya Bunge ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba ambayo inabatilisha sheria inayokinzana nayo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizoweka sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanye marekebisho.

### 3.3.2 Dosari ya Kuwa na Masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**KWA KUWA**, Zipo sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo ambalo –

(i) si dhamira ya Bunge kukabidhi mamlaka serikalini madaraka ya kufafanua sheria yake;

(ii) ni ukiukwaji wa katazo lililowekwa na Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; na

(iii) halisaidii utekelezaji wa sheria mama inayohusika au Sheria nyingine ya nchi ilivyostahili,

**NA KWA KUWA,** Kuwepo kwa sheria ndogo zinazokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi –

(i) ni kuvuka mipaka iliyowekwa na Bunge ambalo halitarajii na haliwezi kutarajia sheria inayotokana na Bunge kukasimu madaraka yake, ikiuke Sheria za Bunge,

(ii) ni jambo linalobatilisha sheria ndogo hizo kwa kiasi inachokiuka au kukinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo ambazo zimebainika kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

### 3.3.3 Masharti Yasiyo na Uhalisia

**KWA KUWA**, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, jambo linaloweza kukwamisha utekelezaji wake,

**NA KWA KUWA**, Athari ya ugumu katika utekelezaji wa sheria ndogo ni jambo linaloathiri tija ya sheria ndogo hizo na kuondoa mantiki ya kukabidhi madaraka ya Bunge kutunga Sheria,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

### 3.3.4 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria

**KWA KUWA,** Baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba, zimebainika kuwa na dosari ya kutokuendana na misingi ya uandishi wa sheria,

**NA KWA KUWA,** Uandishi wa sheria ndogo usioendana na misingi ya uandishi wa sheria –

(i) unaweza kuathiri maana iliyokusudiwa katika sheria ndogo inayohusika; na

(ii) unaweza kuwa sehemu ya chanzo cha sheria ndogo kushindwa kufanikisha madhumuni ya sheria ya Bunge,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo ambazo zimebainika na dosari hizo, zirekebishe dosari za kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

### 3.3.5 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**KWA KUWA**, Majedwali ni sehemu ya sheria kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria na yanastahili kusomwa kwa pamoja na vifungu vinavyohusika, lakini baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali;

**NA KWA KUWA**, Dosari za uandishi wa Majedwali ya baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa na kuripotiwa katika Taarifa hii:

(i) ni jambo linaloweza kukanganya ufafanuzi unaotolewa kuhusu kifungu kinachohusika,

(ii) ni chanzo cha kutatiza utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika kutokana na kukosa ukamilifu,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari za uandishi wa majedwali, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

### 3.3.6 Kurekebisha Dosari Zilizobainika kwenye Sheria Ndogo na Madhara Yake

**KWA KUWA**, Dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali la Uchambuzi ambalo ni Kiambatisho Na. 1 cha Taarifa hii, ni jambo –

(i) linaloendeleza madhara yasiyokubaliwa na Bunge lenye madaraka halisi ya kutunga sheria za nchi,

(ii) linalohitaji hatua stahiki za Bunge linalokabidhi madaraka yake kwa mamlaka zilizoweka sheria ndogo ambazo zimebainka kuwa na dosari na kutakiwa kurekebishwa,

**NA KWA KUWA**, Kuendelea kwa madhara ya dosari zilizobainika kwenye sheria ndogo baada ya kuazimiwa na Bunge kwamba zirekebishwe, ni suala ambalo:

(i) linaweza kuliweka Bunge katika hali ya kutoeleweka miongoni mwa wananchi ambao wanalitarajia kuhakikisha kwamba, sheria zote za nchi zinakidhi mahitaji badala ya kuwa na dosari,

(ii) linaweza kuwa, linatokana na Bunge kutopatiwa Taarifa za utekelezaji wa Maazimio yake,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii:

(i) zitekeleze maazimio haya kwa kasi inayotakiwa ili kuepusha madhara ya dosari zilizobainishwa; na

(ii) ziwasilishe Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo wakati wa vikao vya Kamati kuekelea Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge

### 3.3.7 Kutokukamilika kwa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yaliyolenga Kurekebishwa kwa Sheria Ndogo

**KWA KUWA**, Athari za dosari za sheria ndogo zinafikia hatua ya juu ya kushughulikiwa kwa marekebisho ya sheria ndogo kutangazwa katika Gazeti la Serikali, lakini –

(i) zimebainika mamlaka ambazo hazijafikia hatua za kutangaza marekebisho ya sheria ndogo, kutokana na kuwa na mlolongo mrefu wa hatua za ukamilishaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge,

(ii) hali inayosababisha Wananchi kuendelea kuathiriwa na madhara ya dosari katika sheria ndogo licha ya

Bunge kuwa na maazimio yaliyolenga kuonda athari za dosari,

**NA KWA KUWA**, Kuendelea kwa dosari za sheria ndogo na athari zinazotokana na dosari hizo ni jambo linalostahili kupatiwa maelezo ya Mamlaka zinazohusika ili kutatua tatizo la msingi linaloweza kuwa linakwamisha dhamira ya Bunge,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizobainika kutokuwa zimefikia hatua ya kutangaza marekebisho ya sheria ndogo,

(i) kuondoa mlolongo mrefu wa hatua za kufanya marekebisho yanayokusudiwa; na

(ii) ziwasilishe taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge wakati wa vikao vya Kamati kuekelea Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge.

### 3.4 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa uongozi wako mahiri wa Bunge, ambao umeweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya sheria ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Umahiri wao katika kazi umewezesha kukamilika taarifa hii inayosomwa mbele ya Bunge lako leo hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

i) Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – **Mwenyekiti**;
ii) Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mb – **M/ Mwenyekiti;**
iii) Mhe. Amour Khamis Mbarouk, Mb;
iv) Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb;
v) Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, Mb;

vi) Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb;
vii) Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, Mb;
viii) Mhe. Hamida Mohammed Abdallah, Mb;
ix) Mhe. Ally Mohamed Kassinge, Mb;
x) Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb;
xi) Mhe. Maryam Omar Said, Mb;
xii) Mhe. Zulfa Mmaka Omar, Mb;
xiii) Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb;
xiv) Mhe. Amina Bakar Yusuf, Mb;
xv) Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb;
xvi) Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb;
xvii) Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb;
xviii) Mhe. Ummy Ally Mwalimu, Mb;
xix) Mhe. Michael Constantino. Mwakamo, Mb;
xx) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb;
xxi) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb; na
xxii) Mhe. Ally Juma Makoa, Mb.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati nimshukuru Mhe. William Vanging'embe Lukuvi, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu unaowezesha mawasiliano mazuri kati ya Wizara na Kamati hivyo, kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri waliohusika na sheria ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao pia uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ya uchambuzi wa sheria ndogo na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, nichukue fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao usio kifani katika Vikao vya Uchambuzi wa sheria ndogo na Vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kuishukuru kwa dhati Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard kwa ushirikiano anaoipatia Kamati hatimaye kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## 3.5 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**
5 Februari, 2025

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante. Sasa tunaanza uchangiaji. Naanza na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, jiandae Dkt. Nahato, Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambao zipo Mezani kwetu. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wote wawili kwa uwasilishaji wao mahiri. Pia nawapongeza Wajumbe wa Kamati hizi mbili, yaani ile ya Utawala, Katiba na Sheria na Wajumbe wa Sheria Ndogo kwa kazi zao ambazo zimewasilishwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa za kina na ambazo zinaonesha ni jinsi gani Kamati hizo zipo makini na zimetuletea taarifa ambazo zina mambo mengi ambayo yanatuonesha kwa kipindi cha muda huo nini kimefanyika katika Kamati zetu hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza mchango wangu naomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nampongeza kwa sababu ya uchapakazi wake na kazi kubwa anayoifanya katika kutuletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza kwa tuzo maalumu ambayo ameipata jana. Hii inaonesha ni jinsi gani amewekeza katika sekta ya afya. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Rais, hongerani Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, pia, hongerani watendaji wote wa Wizara zote ambao wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa tukio ambalo linaendelea sasa hivi kule uwanjani kwa kuteuliwa kwake kuwa Mgombe wa Kiti cha Urais wa Chama chetu pendwa, Chama cha Mapinduzi. Siyo hivyo tu, nampongeza Balozi, Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza, pia na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuteuliwa kupeperusha bendera kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yetu kwamba leo wametambulishwa, Wana-CCM, tutaingia kazini kutafuta kura na ushindi mkubwa utapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wetu, kwamba malengo makuu ya kutungwa kwa Sheria Ndogo ni kuweka mazingira wezeshi ili Sheria Mama ziweze kutekelezwa, lakini kama ilivyowasilishwa pale kwenye taarifa, kuna sheria ndogo nyingine zimekuja na masharti ambayo hayana uhalisia, hivyo kusababisha mambo makubwa mawili: Kwanza, kutokutekelezeka kwa Sheria Mama, na pia, kuzua kero katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tumetoa azimio pale kwamba masharti yote ambayo hayana uhalisia, yarekebishwe ili yaendane na malengo ya kuanzishwa kwa kanuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nami nitajikita katika maeneo matatu; Sheria Ndogo tatu. Sheria ya kwanza ni kama ilivyosomwa pale; Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ambayo ni *GN* na, 814 ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wakati wanatafsiri hii Sheria ya Madini ya Ujenzi, wamejumuisha na tofali kwamba ni sehemu ya madini ya ujenzi. Sasa hii inaweza kuleta kero kwa watendaji ambao watatafsiri kwa jumla matumizi ya kifungu hiki kwamba, watakamata na tofali ambazo hazihusiki kama madini ya ujenzi kwa sababu, kimsingi siyo aina zote za tofali ni aina ya madini ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofali zile za udongo, unaweza ukajumuisha kwenye madini ya ujenzi, lakini zile tofali nyingine siyo za madini ya ujenzi. Kwa hiyo, hii ni changamoto ambayo tumeibaini na inaweza kuleta kero wakati watumishi wa halmashauri wanatekeleza hiyo kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni nyingine ni Kanuni ya Bima ya Afya kwa wote ile *GN* namba 809 Kanuni Namba 24. Hapa inaweka ukomo wa wanachama katika Skimu ya Bima ya Afya. Inasema, mwanachama asipochangia kwa miezi mitatu, basi huduma itasitishwa. Sasa, huyu ni mtumishi wa umma na mtumishi wa umma hachangii kwa kupeleka yeye mwenyewe kwenye skimu. Wajibu wa mtumishi wa umma amepewa mwajiri wake kwamba lazima awasilishe kila mwezi. Sasa kwa kifungu hiki ataumizwa mtumishi wa umma ilhali yeye sio wajibu wake kupeleka kila mwezi, ni mwajiri wake ambaye anatakiwa apeleke kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa vifungu kama hivi vinasababisha kero kwa watumishi, vinasababisha malalamiko

kwa watumishi na hivyo kusababisha watu kutoona umuhimu wa sheria iliyoanzishwa wakati kuna kifungu hiki ambacho hakina uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kwenye Kamati yetu tumependekeza kwamba vifungu kama hivi virekebishwe kuleta uhalisia. Kifungu hiki hakina uhalisia kwa sababu mtumishi hapeleki fedha kwenye skimu kila mwezi. Mtumishi wa umma anapeleka kwa kukatwa mshahara wake na mwajiri wake ndiyo anayetakiwa kupeleka kwenye mfuko kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunatarajia vifungu kama hivi vitarekebishwa, ili Sheria Ndogo zitimize lengo lake la msingi kurahisisha utekelezaji wa sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nimetoa mifano miwili tu ya hizi Sheria Ndogo ambazo zimetungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, chini ya Mheshimiwa Mchengerwa. Kwa kweli, kuna kazi kubwa sana wameifanya. Hapo zamani kulikuwa na dosari nyingi sana zinaonekana katika Sheria Ndogo ambazo zinawasilishwa katika Kamati yetu, lakini sasa hivi kuna makosa machache sana kama haya ambayo yanaweza kurekebishika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Dkt. Nahato, jiandae Dkt. Chamuriho na Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika mawasilisho mawili yaliyowasilishwa na Wenyeviti wa Kamati za Sheria. Awali ya yote, napenda kuwapongeza sana, wamewasilisha vizuri na kwa umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia, nichukue nafasi ya kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupendekezwa kuwa Mgombea wa Urais akiwa pamoja na Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uhakika tunategemea Chama cha Mapinduzi kitashinda uchaguzi wa mwaka huu kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, nawapongeza sana. Vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa jinsi anavyoendesha Bunge letu pamoja na Naibu Spika kwa jinsi pia, unavyoendesha Bunge kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika Sheria Ndogo kama tulivyoziona katika Kamati yetu. Sheria Ndogo dhumuni lake ni kutoa ufafanuzi wa utekelezaji wa masharti yaliyowekwa na Sheria ya Bunge. Hata hivyo, wakati tukiendelea na uchambuzi katika sheria zetu, tulibaini dosari mbalimbali na mojawapo ambayo mimi nitaeleza ni kasoro za uandishi katika sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano tu wa sheria ambazo zimeonesha makosa ya kiuandishi yaliyojitokeza wakati tunachambua katika Kamati yetu ya Sheria Ndogo. Moja ni Tangazo la Serikali Na. 778 la Mwaka 2024, Kifungu cha 11. Pia kuna Tangazo la Serikali Na. 814 la Mwaka 2024, Kifungu cha 12 na Tangazo la Serikali Na. 263 la Mwaka 2024, Kifungu cha Nne, pamoja na Tangazo la Serikali 366 la Mwaka 2024, Kanuni ya 8C. Hizo ni baadhi tu ya sheria ambazo tumeona zina makosa ya kiuandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa makosa haya ya kiuandishi unaweza kukwamisha lengo la Bunge kuhusu utekelezaji wa sheria zilizotungwa na Bunge. Makosa hayo yanaweza kupotosha lile jambo ambalo lilikusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandishi ni taaluma ambayo inatakiwa izingatiwe sana, kwani neno linapokosewa linaleta

maana tofauti. Kwa hiyo, katika Kamati yetu tuligundua kwamba, makosa hayo ya sheria ambayo hayaendani na misingi yanaweza kuathiri maana iliyokusudiwa katika Sheria Ndogo inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaweza kuwa ni sehemu ya chanzo cha Sheria Ndogo kushindwa kufanikisha madhumuni ya sheria pale ambapo sheria hizo zimekuja katika Kamati zikiwa na makosa ya kiuandishi. Hivyo basi, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja inasisitiza mamlaka zinazokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo ziwe makini katika uandishi. Makosa ambayo hayana sababu kuwepo katika sheria hiyo yarekebishwe, ili yanapokuja katika Kamati basi tusitumie muda mrefu kukosoa uandishi ambao unajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati pia tulipendekeza zirekebishwe dosari hizo ili ziweze kuendana na sheria ambazo zinategemewa kutumika katika nchi yetu na hasa pale Bunge linapokuwa limetunga sheria zinapoenda kutumika zikiwa na dosari za uandishi zinapotosha maana ambayo ilitegemewa. Kwa kuondoa makosa hayo ya kiuandishi, basi sheria hizi zitakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wizara zote ambazo walikubaliana na Kamati na kwenda kurekebisha makosa au dosari zote za uandishi zilizojitokeza na hivyo, sasa sheria zetu zimesomeka vizuri zikiwa na uandishi ulio mzuri. Ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, jiandae Mheshimiwa Kapinga. Jiandae Dkt. Kikoyo.

**MHE. *ENG.* DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja hizi ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti

wawili. Kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutuongoza vizuri kwa kutekeleza vizuri falsafa zake nne za *4R* kwa kusisitiza Utawala Bora wa Sheria, sifa ambazo zimemfanya achaguliwe tena kuwa mgombea pekee wa Chama chetu cha Mapinduzi, na sifa ambazo zinamfanya apate tuzo mbalimbali za Kimataifa, kama aliyoipata jana. Kwa hiyo, tunampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuwapongeza Wenyeviti wote wawili kwa uwasilisho wao mzuri wa hoja zilizotolewa. Vilevile napenda kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu Wizara zote kuja kuwasilisha katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu ambalo Bunge limepewa katika Ibara ya 64 (1) ya Katiba la Kutunga Sheria na Kuzisimamia pamoja na ile ya kumkabidhi mtu yeyote kufanya shughuli hiyo, Ibara 97 (5), lazima tulilinde kwa wivu mkubwa. Hivyo, hizi dosari mbalimbali ambazo tunaziona ni lazima zirekebishwe ili tuendane vizuri na kusudio la Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia majedwali yaliyowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba na ningependa kutoa mifano ifuatayo ya dosari hizo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tangazo la Serikali Na. 264 ambalo Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru, Halmashauri ya Biharamulo. Jedwali la Nne limetoza ushuru kwa wanyama wachache kuliko wale ambao wanapatikana katika masoko yetu. Hiyo inaweza kusababisha halmashauri hiyo kukosa ushuru na ikapingana na lengo la sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukiangalia katika Sehemu C ya jedwali hilo hilo, utakuta kuna mazao ya misitu ambayo yametoza ushuru wa milango, madirisha, fito na kadhalika, lakini hawakusema kama wanatoza kwa mlango mmoja, milango yote au kadhaa. Hivyo, hiyo inaleta sintofahamu kwa kutoweka kipimo,

na italeta utashi kwa watekelezaji ambao wanaweza wakapotosha lengo jema la sheria iliyotungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Tangazo la Serikali Na. 510 ambazo ni Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Simanjiro na vilevile ukiangalia jedwali lake la kwanza kipengele cha Sita, kuna Ada ya Wakandarasi imesema kwa kila cheti inatoa asilimia mbili. Sasa unajiuliza, hii asilimia mbili kwenye kila cheti cha mkandarasi ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, hii italeta mkanganyiko kwa sababu, siyo kodi inayotozwa kwenye *Certificate* ya Mkandarasi, bali walikuwa wana maana ya kitu kingine kabisa, *appreciations certificates.* Kwa hiyo, Kamati imewaelekeza wakalibadili hilo liende vizuri, ili hawa wakandarasi wetu wasipate changamoto katika utekelezaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tukiangalia katika ada na ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Kifungu cha 15, Namba mbili, kimeweka utaratibu wa kuuza bidhaa ambazo zimekamatwa na Halmashauri, lakini Kifungu hicho hicho kiko kimya kuhusu hela za ziada ambazo zitabaki. Kwa hiyo, tumewaelekeza kwamba, ukikamata bidhaa ukaiuza, utakavyorudisha ile fedha, chenji ni lazima umrudishie mwenyewe na haiwezi ikabaki kwa halmashauri tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna jedwali la kwanza Sehemu J, ambayo haina uhalisia katika utozaji wa *CSSR* ambayo wamepanga kwamba, wanatoza Ushuru wa *CSSR* wa shilingi 100/= tu kwa kilo moja ya dhahabu. Sasa ukiangalia thamani ya dhahabu kilo moja na kutoza ushuru wa shilingi 100/=, unaona hii hapa ni lazima kuna kosa katika uandishi wa hilo jedwali. Hivyo tumesema likabadilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Chunya hiyo hiyo, jedwali hilo hilo la kwanza, kipengele cha kwanza, cha nne na cha tano, wametoza ushuru wa mazao kwa asilimia tatu, lakini hawakusema hii asilimia tatu ni ya kitu gani? Hivyo, tumewashauri

waende wakabadilishe ili kuweza kuweka mizania sawa. Kwamba anayetoza ushuru aweze kuelewa ni kitu gani hasa ambacho anaweza akatakiwa kutoza huo ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante *Doctor*.

**MHE. *ENG.* DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kikoyo na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini pia, niwapongeze Wenyeviti waliotuwasilishia taarifa hapa, wamewasilisha kwa weledi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pale ambapo Mheshimiwa Dkt. Chamuriho amekomea, na hasa, eneo hili la majedwali. Kabla sijaendelea, kwa ujumla wake tu niipongeze Serikali kwa namna inavyofanya kazi nzuri ya utunzi wa sheria hizi, hasa hasa hizi Sheria Ndogo. Kwamba, ni jukumu ambalo wamekasimiwa, lakini wamelifanya kwa weledi mkubwa, hasa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande huu wa majedwali ambao Mheshimiwa Dkt. Chamuriho alikua anauongelea, kuna baadhi ya maeneo ambapo ukamilifu wa sheria hizi ndogo na sheria kwa ujumla ni pamoja na majedwali yaliyopo mle. Ili sheria hizi ziweze kutumika vizuri ni pamoja na uandishi mzuri wa majedwali haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali linalohusu Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Tangazo la

Serikali 811 la Mwaka 2024, katika Sehemu J, jedwali la kwanza ambalo linahusu Ushuru wa Kusafirisha Mifugo ya Samaki, hata Mwenyekiti hapa amelieleza vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kipengele kile cha 18B, ambacho kinatoza ushuru wa shilingi 300/= kwa ndoo ya lita 20 ya samaki, lakini hawajatuambia ni kiasi gani kitatozwa kwa vipimo vya chini ya ndoo ya lita 20. Kutokuwepo kwa kiasi hicho kwa kipimo hicho na kiasi hicho kinaleta mkanganyiko kwa vipimo vya chini ya ndoo ya lita 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wahusika wanapotunga majedwali haya, ni vizuri sana wakaweka vizuri chini ya kipimo kile kwa sababu, wananchi wengine siyo lazima wabebe samaki wa ujazo ule, kwa maana ya ndoo ya lita 20. Je, tukimkuta mtu amebeba ndoo ya lita 10, huyo atatozwa shilingi ngapi? Ukikuta wasimamizi wasio wazuri, basi wanaweza wakakanganya hapa, ikaleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Sheria ya Ada ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi, Halmashauri ya Kalambo, Tangazo la Serikali Na. 815, Jedwali la tatu, kuhusu kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi; jedwali linaweka sharti la kwamba, kila anayesafirisha mazao hayo ya uvuvi, ikiwemo hata ya kutumia nyumbani, awe na kibali. Sasa tunajiuliza, anayeenda kutumia samaki nyumbani, atakuwa na kibali cha kusafirisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalisia ni kwamba siyo kweli, hawa watu watasafirisha kwa kawaida tu. Kwa hiyo, watunzi wa sheria wanapotunga haya majedwali na kuweka hizi sheria lazima wawe wazi kupunguza hii mikanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningeenda eneo lile ambapo sheria hizi ndogo zinakinzana ama zinaonekana kukinzana na Katiba. Kwa mfano, Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Tangazo la Serikali Na. 266 la Mwaka 2024, Kifungu Kidogo cha Tano, kinaweka wajibu kwa mfugaji, kinaweka wajibu kwa

wafugaji kwamba, mfugaji wa eneo husika hapaswi kumkaribisha mfugaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba, mfugaji wa pale Shinyanga hapaswi kumkaribisha mfugaji anayetoka eneo lingine, lakini wako na nia fulani. Wao kwenye Kanuni hii hawajaweka sharti kwamba, ni mfugaji yupi ambaye hapaswi kukaribishwa. Mfugaji mwenyewe tu hapaswi kumtembelea mfugaji mwenzake akajifunza ama mfugaji mwenye mifugo ndio hapaswi kukaribishwa? Lakini inawezekana kabisa wao walilenga mfugaji mwenye mifugo ndio hapaswi kukaribishwa na mfugaji aliyepo kwenye Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kuweka masharti ya namna hii yanapingana kabisa na Katiba ambayo inaruhusu watu kutembea kutoka eneo moja. Watu wana haki ya kutoka eneo moja kwenda eneo lingine na hivyo, kama wana nia ya kukataza wafugaji na mifugo yao, basi wangeweka wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine la kanuni ambalo pia, linapingana na Katiba ni Kanuni ya Nidhamu kwa Wanafunzi, ya Tangazo la Serikali 365, Kifungu cha 23 (3), ambacho kinaruhusu shauri kusikilizwa pasipo kuwepo kwa mtuhumiwa. Kifungu hiki kinapingana kabisa na Ibara ya 13B, Kifungu Kidogo cha A, ambacho kinataka pale ambapo maamuzi yanayofanyika juu ya mtu, awepo pale aweze kusikilizwa, lakini kanuni hii inasema shauri hili linaweza kusikilizwa pasipo kuwepo huyo mtuhumiwa, moja kwa moja inapingana na Ibara ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono maazimio yote. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kikoyo. Jiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Dkt. Tadayo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia Taarifa ya Kamati hizi, naipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa kazi ambayo imefanyika na inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi napenda kuchangia suala la haki kwa watu wetu hususan Mahakama za Mwanzo. Naishukuru Serikali kwa kipindi hiki kwa maboresho makubwa ambayo yamefanyika na yanaendelea kufanyika kuboresha Mahakama zetu za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa iliyowasilishwa na Kamati yangu ya Utawala, Katiba na Sheria, kipengele cha tatu, kipengele cha kwanza, namba moja, idadi ya majengo ambayo yamejengwa Mahakama za Mwanzo na tunaipongeza Serikali. Inasema mpaka Januari yalikuwepo majengo 935 ya Mahakama za Mwanzo, na kati ya hayo 191 yapo kwenye hatua nzuri ya ujenzi. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wingi wa watu wetu wanatumia hizi Mahakama za Mwanzo katika hatua zao za mwanzo za kutafuta haki, lakini hizi Mahakama za Mwanzo narejea kauli ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Siku ya Sheria juzi aliwaasa Majaji na Mahakimu wasiwe miungu watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Sheria na Katiba ikazichunguze na kumulika jicho kwenye Mahakama za Mwanzo katika hatua za utoaji wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ipo Kamati ya Maadili ya kuwawajibisha hao Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, lakini jukumu hili linaonekana Wakuu wa Wilaya wengi hawalifahamu au hawalifanyii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara husika wakaandae waraka mahsusi kwa Wakuu wetu wa Wilaya, wakawachunguze Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wote, pale wanapotoa haki, ili wananchi wetu wapate haki yao

kulingana na makosa; au kesi wanazozipeleka Mahakamani, kwani kule kuna shida kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeongelea uboreshaji wa sheria za nchi hii. Kwenye hili tunayo Tume ya Kurekebisha Sheria, imetajwa kwenye wasilisho la Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Tume hii inalenga kuboresha sheria zetu, lakini kazi ambayo inafanywa na hii Tume ni ndogo na tatizo ni ukosefu na ufinyu wa bajeti wanayopewa. Napendekeza na kushauri tunapokwenda kwenye bajeti, kwani tume hii ni muhimu sana katika kuboresha sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa tunazo sheria nyingi zimepitwa na wakati, sasa, ni wajibu wa hii tume kufanya marejeo ya mara kwa mara kuhakikisha kwamba, sheria zetu zinaendana na wakati, lakini hawawezi kufanya hii kazi kama bajeti yao na mafungu yao hayawezi kuwaruhusu na hawawezi kuwa na watumishi ambao wanakidhi viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza, kushauri na ninakubaliana na taarifa ya Kamati yangu kwamba tume hii iangaliwe hasa tunapokwenda kwenye kipindi cha Bajeti ya Serikali Kuu, tuwapatie fedha ya kutosha ili waweze kufanya kazi ya kurekebisha sheria zetu ziende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwenye hili tena, kwa kweli yamefanyika maboresho makubwa sana kwenye Mahakama zetu. Sisi ambao tumetoka kwenye Mahakama, enzi za nyuma Mahakama nyingi kusema kweli kuingia ilikuwa ni shida, lakini ukiangalia sasa majengo mengi hasa Mahakama Kuu na Rufaa kweli kazi kubwa imefanyika na inaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Serikali kwa kuja na Mfumo wa TEHAMA hasa hii ambayo inaitwa *Government of Tanzania eCase Management System,* imerahisisha na kupunguza muda wa ku-*file* kesi Mahakamani na kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa tumezoea ukienda kwenye *corridor* mnaitwa na wakati mwingine hata sauti huisikii, lakini kwa sasa kwa mfumo uliopo kwa kweli asiyeona haambiwi tazama. Kazi imefanyika na naipongeza Serikali, naomba iendelee kufanya maboresho hasa kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya sheria yanayofanyika yaingizwe kwenye sheria zetu haraka sana. Tunajikuta tuna sheria, lakini tuna viraka vingi ambavyo vipo nje ya sheria zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali tunapofanya marejeo na marekebisho ya sheria, yale marekebisho yanayofanywa yaingizwe kwenye sheria mara moja ili watumiaji wa hizo sheria wasiwe wanababaika na wakati mwingine watumie sheria ambazo zimesharekebishwa, wakati mwingine kupata yale marekebisho inachukua muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza Serikali kwa msaada wa kisheria ambao unatolewa kwa wananchi hasa wale ambao hawana uwezo wa kutafuta na kuwalipa Mawakili. Kazi kubwa imefanyika hasa kwa wananchi ambao kipato chao hakiwaruhusu kuwatafuta wanasheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wote hapa kumtafuta mwanasheria ni ghali sana, wananchi wengi wamekuwa wakipoteza haki zao kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kuwatafuta na kuwalipa Mawakili wa kujitegemea. Kwa msaada huu unaoendelea wa kisheria ukiunganishwa na Samia *Legal Aid* nina uhakika wananchi wetu watapata haki zao ambazo zilikuwa zinapotea kwa sababu ya kutoweza kuzilipia kwa mawakili wa kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono, na ninashukuru sana kwa kunipatia fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, jiandae Dkt. Tadayo atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kusema Bungeni siku ya leo. Nianze kwanza kwa kuunga mkono maazimio yaliyoletwa mbele ya Bunge letu Tukufu na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kuchangia kwenye eneo la Kanuni za Bima ya Afya kwa Watu Wote za Mwaka 2024. Moja kwa moja, naomba nichangie kwenye Kifungu cha 16 cha Kanuni hizo. Kwa wanaofuatilia, wanaweza kupenda kufanya rejea ya sheria mama (Sheria ya Bima ya Afya kwa Watu Wote ya Mwaka 2023) hususan kwa kuzingatia Kifungu cha Tano, Kifungu cha 25 na Kifungu cha 35 cha sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vyote hivi vinahusiana moja kwa moja na bima ya afya kwa watu wasio na uwezo. Vifungu hivyo kwa sababu ya muda, sitavirejea vyote, lakini vinahusisha mambo yanayohusiana na namna ya kuwatambua na kuwahudumia watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maelekezo yanayotolewa na sheria mama, ni kwamba zitaundwa kanuni kwenye kile Kifungu cha 35 cha sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliteuliwa na Mheshimiwa Spika kwenda kuungana na Kamati ya Sheria Ndogo ili kuzipitia kanuni hizo. Kwa hiyo, tulipoenda kukaa na Kamati ile tulibaini upungufu mwingi sana ambao unaelekezwa na sheria, lakini haujawekwa kwenye kanuni ambazo zililetwa tuzifanyie uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, maeneo ambayo hayakufanyiwa kazi ipasavyo na Waziri aliyetunga hizo, kanuni mojawapo ni eneo la Kanuni ya 16 ambalo linahusiana na watu wasio na uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninazungumza haya na ninapenda tuzingatie *Executive Order* iliyotolewa na Rais wa Marekani Januari 20, ambapo kwa kiasi kikubwa unaona kuna

*shift* ya *health funding* ambayo itatokea kwenye *health system* duniani, kwa sababu Marekani anajiondoa kwenye kuchangia baadhi ya huduma muhimu ambazo na sisi tulikuwa wafaidika wa huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika *Executive Order,* ile Rais wa Marekeni amesitisha kwa miezi mitatu (siku 90) kwamba tusipate mchango wa *PEPFAR* hapa Tanzania. *PEPFAR* inahudumia waathirika wa virusi vya UKIMWI kuanzia matibabu, *orphans and vulnerable children* na huduma za *VCT* za kupima virusi vya UKIMWI, wapatao *1.5 million* ambao ni Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hii inatosha kuwa-*wakeup call* hususan kwa sisi wawakilishi wa Tanzania hapa Bungeni kuanza kufikiria kuwekeza zaidi kwenye mfumo wa afya ambao utatutosheleza kuwahudumia Watanzania zaidi ya milioni 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tishio hili la kusitisha huduma kwa miezi mitatu kwanza wakati wanafanya uchambuzi hatujui baada ya miezi mitatu nini kitatokea? Vipi wakiamua kusitisha *indefinitely.* Katika hiki kipindi cha miezi mitatu Watanzania wanaopata dawa za kufubaza VVU zaidi wa milioni 1.5 wanahudumiwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa unazungumza Bungeni katika kipindi kama hiki halafu ukazitazama zile sheria zetu; Sheria ya Bima ya Afya, Sheria ya Bima pamoja na Kanuni za Bima ya Afya kwa Watu Wote, unaona wazi kabisa kwamba bado hatujaweka *commitment* ya kutosha ya jinsi gani tutatoa huduma za afya kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kwamba ili huduma za Bima ya Afya ziweze kufanikiwa, ni lazima kile Kifungu cha Tano cha kwenye sheria mama ambacho kimesitishwa ukisoma kwenye kanuni na Tangazo la Serikali Namba 700A la Agosti 14, 2024, kwamba Kifungu cha Tano kisifanye kazi na vifungu vingine vingi. Kwa nini kinasitishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasitishwa kwa sababu Kifungu kile cha Tano cha kwenye sheria mama kinaweka ulazima wa kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya ya aina mojawapo *(mandatory enrollment)* kwenye *universal health insurance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, kama hakuna *mandatory enrollment,* maana yake hakuna Bima ya Afya kwa sababu katika *pillars* za Bima ya Afya kunatakiwa kuwe kuna *population coverage, service coverage,* pia kunatakiwa kuwe na *financial protection.* Haya mambo yote katika mfumo ambao tumeutengeneza hapa Bungeni na alioenda kumalizia Mheshimiwa Waziri hayaonekani, maana yake ni kwamba *threat* ya Watanzania kukosa huduma bora za afya ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu ya muda, napenda kupendekeza Serikali ikazifanyie marekebisho upya hizi kanuni ili waweke michango ya uhakika kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Watu Wote, hususan watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama takwimu za *NBS,* wapo takribani 26.4% ambao kwa idadi, kwa kuzingatia Sensa ya Mwaka 2022 wanafika takribani Watanzania milioni 16.3. Kama utawachangia tu takribani shilingi 150,000/= kila mmoja kwa mwaka, maana yake Serikali inatakiwa iwe na bajeti isiyopungua shilingi trilioni 2.44 kwa ajili ya kuwakatia bima 26.4% tu ya Watanzania, jambo ambalo halionekani, na michango hiyo haijawekwa *explicit* kwenye hizi kanuni ambalo lilipaswa kuwa takwa la sheria mama ambayo linawekwa katika Kifungu cha 35 cha Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mapendekezo hayo ya ushauri wangu yaende yakafanyiwe kazi ili mfumo wetu wa Bima ya Afya wa Watu Wote uweze kutimia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Tadayo, halafu Mheshimiwa Jonas na Mheshimiwa Hamida wajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Awali ya yote, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote pamoja na taasisi zao ambao tunafanya nao kazi kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Wamekuwa na ushirikiano mzuri sana na tunawapongeza na kuwashukuru kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono Maazimio ya Kamati zote mbili, lakini nitazungumzia upande wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za taasisi mbalimbali za Kimataifa zinaonesha kwamba, hali ya uchumi wa nchi yetu unakua. Ukiacha hizo taarifa, hata ukiangalia kwa macho unaona vitu viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, unaona kweli hali ya uchumi wetu inakwenda vizuri sana; na cha pili unaona kwamba bado tunao uwezo mkubwa sana wa kuendelea kukuza uchumi wetu, hasa kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo kutufanya tujitosheleze kwa chakula na kuweza kuuza nje; pia mazao ya biashara ambayo ukiacha kuuza pia ni malighafi. Kwa hiyo, tuna *potential* kubwa ya kukuza sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mito mingi, kwa hiyo, tuna uwezo wa kuzalisha umeme zaidi. Kwa hiyo, kwa maneno mengine ni kwamba nchi yetu ipo katika *tipping point,* yaani mazingira ambayo uchumi wake unaweza ukakua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, katika mazingira kama hayo ni lazima suala la utawala wa sheria litamalaki. Utawala wa sheria kama wengi mnavyofahamu historia yake kwenye Karne ya sita, saba, na nane huko India ulianza kwanza kwa kuwawajibisha

watawala kwamba, Mfalme ambaye hawezi kuwalinda watu wake alikuwa anapigwa mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaenda, baadaye wakaja watu wenye akili zaidi *(philosophers)* wakasema haiwezekani kuwajibisha upande mmoja, lazima kuwajibisha pande zote mbili kwamba, lazima kuwe na kitu juu yetu ambacho kinatuongoza. Ndiyo mambo ya sheria yakaanza kutungwa na watu wote wawe sawa mbele ya sheria na waziheshimu sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo wazi kwamba kukosekana kwa utawala wa sheria kumevunja heshima ya nchi nyingi sana hasa za dunia ya tatu, kumewaletea vurugu nyingi sana. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli ni la msingi sana, ndiyo maana katika hatua hii ni lazima kwa dhati kabisa tumpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa *champion* kwenye eno hili la utawala wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na uwekezaji mkubwa sana kwenye sekta ya sheria katika kipindi hiki kama alivyochangia rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, kwa sisi ambao tumekaa kwenye sekta hii muda mrefu tunaona kabisa kwamba, tulikotoka kulikuwaje na tulipo ni wapi, na mtumaini kule mbele ambako tunaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia amekuwa Mwalimu kwenye eneo hili, kwanza kwa kuanzisha *4R* ili tuweze kutekeleza na kuweza kufaidi huu uwekezaji kwenye sekta ya sheria. Pia, suala zima la hii Tume ya Hakijinai pamoja na suala la *Legal Aid* ambalo sasa hivi linaendelea. Haya maeneo yote matatu ni muhimu katika kuvuna faida zinazotokana na uwekezaji mkubwa ambao umefanyika kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi sasa inabakia kwa watendaji na wataalam kufanya kazi yao kwa weledi bila uwoga ilimradi tu wanafuata sheria na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa dhati katika maeneo yanayohusiana na sheria na masuala ya utoaji haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi kama yetu ambayo tuna Katiba inayotambua haki za msingi za binadamu na pia tuna ile sheria ya kukazia zile haki *(Basic Rights, Duty and Enforcement Act)* Sura ya Tatu, Sheria ambayo inatuwezesha sasa kukaza zile haki ambazo zipo ndani ya ule mkataba wa haki za binadamu ili tuweze kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama hayo, hakuna sababu ya mtu kunyimwa haki yake iliyoko ndani ya sheria. Ni masuala tu ya utekelezaji, wakati mwingine unakuwa dhaifu, lakini kwa kweli ikikosekana haki, tusiilaumu Serikali wala sheria, tulaumu watendaji wanaohusika na maeneo hayo kwa sababu sheria zipo na zinatoa kila fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu ya kuchelewesha au kunyima dhamana kwa kosa ambalo lina dhamana, kwa sababu hata kama sheria unayo-*deal* nayo haitaki, basi Katiba ipo na imeruhusu, na Katiba ndiyo sheria mama, hakuna asiyejua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siku zote nasema, sekta ya sheria Tanzania ina uwezo wa kukua na kutoa haki kwa kila mtu, kwa sababu ukishaanza na Katiba na sheria ku-*enforce* zile haki zilizoko ndani ya Katiba, basi hakuna sababu ya kukosa haki yoyote ndani ya nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya makubwa ambayo tunayo, lakini tunahitaji pia kuendelea kuwekeza hasa katika Ofisi ya *DPP* kwa sababu ndiyo *custodian* wa Hakijinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Hakijinai zinawahusu watu wadogo, ndizo ambazo zikikosekana, nchi inakuwa na vurugu nyingi sana. Kwa hiyo, tuwekeze zaidi Ofisi ya *DPP,* bajeti pamoja na watumishi na *training.*

Mheshmiwa Naibu Spika, pia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo ndiyo inalinda haki zetu zote za mikataba na uwekezaji

na sasa hivi dunia inakoelekea, lazima ofisi ile iweze kuwa na viwango vya Kimataifa. Kwa hiyo, nawatia moyo kwamba walete bajeti ya kutosha, nasi Wabunge tuipitishe, ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo niwaalike Jimboni kwangu Mwanga, tunahitaji Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya TAKUKURU. Uwanja tunao, waweke kwenye bajeti waje pale tujenge. Mheshimiwa Simbachawene amenitazama, nina uhakika anataka kuleta Ofisi ya TAKUKURU pale kuijenga. Karibu sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kengele imelia, nimalizie na suala moja tu la madawa ya kulevya. Naipongeza sana Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, wanafanya kazi nzuri sana na kila mtu anaona, lakini vita hii ni kubwa sana. Kila dunia inavyoendelea, *population* inavyokua na maendeleo yanavyoongezeka, hii vita inazidi kuwa kubwa. Kwa bahati mbaya sana inaendana na hii vita ya mambo ya ushoga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, lazima tu-*integrate* hili suala kuanzia kwenye mitaala yetu ya shule za msingi. Mtoto anapoingia Darasa la Kwanza afundishwe ubaya wa madawa ya kulevya, afundishwe ubaya wa ushoga, afundishwe ubaya wa ulevi wa kupindukia. Akienda Kanisani, akienda kwenye *Sunday School*, kwenye Madrasa nako afundishwe hivyo hivyo; na wakirudi nyumbani kwenye familia tutilie mkazo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii vita inakwenda kuwa *personal,* yaani haitakuwa tena kutegemea Serikali. Itategemea kila mmoja amefundishwa nini na anakua kuelekea wapi? Tusitake kufikia hatua ambazo wenzetu huko nje wamefikia sasa hivi, mpaka Rais analazimika kutoa amri nyingi za kufuta vitu ambavyo vimeshajiingiza sana kwenye jamii kiasi kwamba vinakuwa shida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, machache yangu ni hayo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Jonas; Mheshimiwa Hamida Abdallah jiandae na Mheshimiwa Maryam.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambazo ziko Mezani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa uwasilishaji wa taarifa za Kamati zao kwa weledi mkubwa sana. Nawapongeza Kamati ya Sheria Ndogo kwa namna ambavyo wameweza kujikita katika kuchambua sheria mbalimbali na kuweka mambo sawa ili kuhakikisha kwamba wanaokwenda kusimamia sheria hizi, basi waende kusimamia vizuri, kuhakikisha tunaleta ustawi wa wananchi wetu katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo imeainisha mambo mbalimbali baada ya kufanya uchambuzi wa sheria hizi, na kuona kwamba kuna dosari mbalimbali ambazo zimeonekana kwamba ni kero kwa watumiaji wa sheria hizi, ama katika usimamizi wa sheria hizi. Kwa hiyo, nawaomba katika maeneo yote yaliyoonekana yana dosari, basi wahusika waende wakayafanyie marekebisho ili twende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Halmashauri ya Mafinga, *TS* Na. 211. Sehemu ya 10 ya Jedwali la kwanza inahusu ushuru wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika kipengele hiki, kuna tatizo. Kipengele kina tatizo la kuweka ada ya shilingi 200/= kwa wapaaji wa samaki, na ukiangalia samaki huyo anaanza kulipiwa tozo kuanzia kwa mvuvi mwenyewe. Mvuvi husika anamuuzia mteja mwingine ambaye anakwenda kuuza hadi kwa huyu mtu mdogo kabisa ambaye ameacha kuwa kibaka mtaani akaamua kwenda katika maeneo haya na kutafuta ajira ya

kupaa samaki ili kumfanya mteja atoke katika eneo hili akiwa na samaki ambao wakosafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani tukafanyie marekebisho eneo hili ili kutenda haki kwa wananchi wetu na vilevile kuendelea kuleta ustawi kwa wananchi wetu na kuongeza ajira kwa vijana ambao wanakosa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Tangazo la Serikali Na. 815, Sheria ya Mwaka 2020, Jedwali la Tatu linahusu kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi. Katika maeneo haya, tumeona kwamba kuna tatizo; na niseme tu kwamba, jedwali limeweka sharti la kuomba kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kila mtu anavyokwenda kununua samaki kwa ajili ya matumizi ya nyumbani akaombe kibali halmashauri? Naona hii haijakaa sawa. Kwa hiyo, halmashauri husika ama Wizara ya TAMISEMI wakahakikishe kwamba eneo hili wanalitazama vizuri ili kuhakikisha kwamba linafanyiwa marekebisho ili tafsiri yake iweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile nawapongeza Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa ambao umefanyika wiki moja iliyopita na kuridhia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ndiye Mgombea wa Urais wa Chama cha Mapinduzi pamoja na mgombea mwenza wake Balozi Emmanuel John Nchimbi. Pia Rais wa Zanzibar kuwa ndiye mgombea wa Urais wa mwaka huu wa 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pamoja nawatakia kila la heri. Mwenyezi Mungu awaweke salama, awaweke katika afya njema ili maazimio yetu yaweze kutekelezwa kwa sababu bado tunawahitaji kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Bado

Watanzania tunahitaji Marais hawa waendelee kuwa Marais wetu ili mambo yetu yaweze kuwa safi. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa sababu anasimamia masuala yote ya sheria na kuharakisha kwenda kwenye utekelezaji wa matumizi ya sheria hii. Mwisho, nawapongeza Katibu wetu wa Kamati ya Sheria Ndogo, pamoja na msaidizi wake kwa namna ambavyo anatufanya sisi Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kuendesha shughuli zetu kwa weledi mkubwa. Tunawashukuru na tunawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam, halafu wajiandae Naibu Waziri Muungano, Naibu Waziri Utumishi, Waziri wa Mipango, na Waziri wa Katiba na Sheria.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia ili nami niweze kusema neno katika maazimio haya mawili yaliyopo Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Wenyeviti wa Kamati zetu zote mbili kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kuhakikisha Wajumbe tunafanya kazi zetu pamoja nao kwa weledi. Pia, nawapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Sheria Ndogo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleze pale ambapo amefikia mwenzangu, Mheshimiwa Hamida; na nitajielekeza kwenye utekelezwaji wa maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba katika Mkutano wa Kumi na Tatu, tulipitisha Maazimio ya Bunge ya Kamati ya Sheria Ndogo. Kati ya maazimio yaliyopita, ilikuwemo

Sheria ya Ada na Ushuru ya Wilaya ya Mafinga, Tangazo Na. 211, inayomhusu mpara samaki kutoa ushuru wa shilingi 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tulilisemea sana, na mwisho tukaazimia kwamba hii haikubaliki. Ule ulikuwa ni Mkutano wa Kumi na Tatu, leo tunazungumza ndani ya Mkutano wa Kumi na Nane. Tulizungumza na tukakubaliana vizuri na Mheshimiwa Waziri, lakini mpaka leo hii hii sheria bado ipo na inafanya kazi. Ni kumaanisha kwamba, Azimio la Bunge halikufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka niiambie Serikali, mara zote sheria mama zinakuja Bungeni zinafanyiwa kazi na zinakwenda kufanya kazi zikiwa ziko vizuri, lakini mara nyingi kanuni ndizo zinazowaumiza wananchi. Hii ni kwa sababu zinatoka mtaani, zinafanya kazi, na zinapokuja kwetu, tayari kule zinakuwa zimeshaanza kufanya kazi. Kwa nini Azimio la Bunge likishaelekeza, Wizara isichukue hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi huwa naumiza kichwa hapa. Siyo hilo tu, pia lilikuwepo Tangazo la Serikali, Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mafinga, inayoelekeza kwamba watakusanya ushuru kuanzia saa 12.00, na mwisho kukusanya ushuru ni saa 12.00 jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haina uhalisia, kwani wengi wanaweza kukwepa ushuru kwa kuona kwamba, mimi nimefika sehemu saa 11.30, ngoja ni-*delay* kidogo, nikiingia saa 12.01 siwezi kudaiwa tena ushuru. Tunapoteza mapato mengi ya Serikali hapa. Kwa nini Serikali msiwe pamoja na sisi? Hili ni tatizo. Hii sheria ilikuja kwenye azimio wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu, lakini leo hii tunavyozungumza, ni Mkutano wa Kumi na Nae, lakini bado sheria hii haijafanyiwa marekebisho na haijafanyiwa kazi. Hili jambo linatusikitisha sana kama Kamati. Ni vizuri tunapotoa maazimio ya Bunge Mawaziri wawe tayari, tuwe pamoja katika kuhakikisha yanafayiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamesemwa na wenzangu waliopita na hivyo hakuna haja ya kuyarudia. Naendelea kuwapongeza viongozi wetu, akiwemo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya, pia Rais wa Zanzibar kwa kazi nzuri anayoifanya. Nawaambia tu, CCM hawakukosea kuwaweka kama ni wagombea mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya machache hayo, naunga mkono hoja zote mbili zilizopo Mezani. Ahsante sana, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa ujasiri.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na ninazipongeza Wizara zote chini ya Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kamati pia tulifanikiwa kutembelea miradi mbalimbali, tumeona kwa asilimia kubwa imetekelezwa japokuwa ipo michache iliyotekelezwa chini ya kiwango. Hiyo ni kutokana na ucheleweshaji wa kulipwa wakandarasi kwa muda. Hivyo, tunaiomba Serikali kuwalipa wakandarasi kwa wakati ili miradi ikamilike kwa wakati na iweze kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa kutekeleza maazimio tuliyoyafikia kama Bunge. Kipekee naipongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwani imeboresha miundombinu ya watu wenye ulemavu katika mchakato wa usaili wa ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, e-Utendaji ni mfumo wa kuimarisha utendaji kazi wa watumishi wa taasisi za umma unaotegemewa

kuleta tija katika kufuatilia na kutoa mrejesho wa utendaji kazi na kuimarisha uwazi na uwajibikaji itakayohakikisha wananchi wanapata huduma bora na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishauri Serikali, ubunifu huu uendane na kupeleka mtandao ya vijijini ili watumishi waliopo huko pembezoni, wasawazwe kwa uwiano ili wasiwepo ambao wanakuwa na mzigo mkubwa wa majukumu hivyo kushindwa kujaza mifumo hiyo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira kuendelea kusaili kidigitali. Kwa sasa baada ya mfumo wa kupima uelewa na ufahamu ambao mpaka sasa umesaili zaidi ya wasailiwa 28,143 katika taasisi 19 na kada 60, na sasa wamekuja na mfumo wa kupima haiba na tabia, umefikia 60%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza Serikali iwekeze mifumo hii kwenye vituo vyote vya usaili katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Naibu Waziri, Wizara ya Makamu wa Rais, Muungano.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mungu, kwa kuwa ametujalia kukutana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue fursa hii kukushukuru wewe, Wajumbe wa Kamati hii ya Utawala, Katiba, na Sheria pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wametoa michango yao ambayo kwa kweli iko *very constructive*; na inaonesha wazi kwamba wametoa michango hii wakiwa wana mustakabali mwema wa kulijenga Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Dkt. Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi kubwa wanayoifanya, hasa katika kusimamia, kulinda, kuendeleza, na hatimaye Muungano huu keshokutwa unakwenda kutimiza miaka 61. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi sana duniani zilijaribu kutaka kuungana, lakini zilishindwa na ziliishia njiani. Leo nchi yetu inakwenda kutimiza miaka 61 ya Muungano huu. Ni kazi kubwa iliyofanywa na viongozi wetu kwa sababu ya busara ya viongozi wetu wa pande zote mbili; Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi wana busara ya hali ya juu katika kuulinda na kuuendeleza Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa Kamati ya pamoja inayoshughulikia mambo yote ya Muungano, na kuhakikisha kwamba panapotokezea jambo linaloleta mgongano, Kamati hii inakutana kwa kushirikiana pande zote mbili. Lengo ni kuhakikisha kwamba muungano huu unaendelea kubaka salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni dhamira ya viongozi tulionao. Watanzania bado wana nia na dhamira ya kuuendeleza Muungano huu. Maana yake ni kazi kubwa inayofanywa na viongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kumekuja hoja, ama moja miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa, ni jambo la uwepo wa Ofisi za Muungano. Kwanza uwepo wa Ofisi ya Makamu wa Rais inayosimamia Muungano kwa upande wa Zanzibar, na pia uwepo wa ofisi za kudumu kwa baadhi ya ofisi kupitia Wizara ambazo zina nasaba na Muungano kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, na Watanzania kwa ujumla kwamba, zipo taasisi 33.

Zote hizi ni taasisi ambazo zinagusa kwenye Muungano, na kati ya hizo, 21 tayari zimeshakuwa na majengo yao yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano tumeshaanza mchakato wa kutafuta ofisi itakayokuwa ndiyo ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa lingine nataka niwaambie tena Waheshimiwa, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa. Ndani ya kipindi chake, zaidi ya changamoto 15 zimepatiwa ufumbuzi kwa lengo la kuhakikisha kwamba Muungano huu unaendelea na unadumu. Nawaomba Watanzania watambue kuwa, Muungano wetu ndio Utaifa wetu. Tuendelee kuuenzi Muungano wetu kwa ajili ya maslahi mapana ya vizazi vinavyokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupokea taarifa hii, lakini tuwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, yote waliyoyaelekeza na waliyoyachangia pamoja na Kamati, tunakwenda kuyafanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, niwatangaze kwanza wageni waliopo Bungeni mchana huu. Hawa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay, ambaye ni Padri Swaga na Padri Novatus wa Kanisa Katoliki kutoka Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Sasa ninamwita Naibu Waziri Utumishi, jiandae Waziri wa Mipango.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru

sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mchango wangu wa kwenye hoja zilizowekwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kuwepo hapa leo. Kwa namna ya pekee nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, hasa katika eneo hili la utumishi wa umma na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mambo mengi makubwa yanafanyika, na kweli anastahili tuzo nyingi, na ninaamini atapata tuzo nyingi zaidi na zaidi, kwa sababu kazi kubwa anayoifanya inaleta hamasa kubwa kwa watu wengi kumpa tuzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba pia nijielekeze kwa mambo machache yaliyosemwa. Kwanza, naipongeza Kamati yetu ya Utawala, Katiba, na Sheria kwa namna ambavyo wanafanya kazi nzuri chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Mhagama pamoja na Makamu Mwenyekiti na Kamati yote kwa ujumla, wanafanya kazi nzuri. Tumekuwa tukishirikiana nao, na kwa kweli ushauri wao umekuwa ni msaada mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na ufanisi katika kazi yetu ambayo tumekabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo tumepewa ushauri na kwa kweli tumelifanyia kazi ambalo nitaanza nalo ni kuhusu upandishaji wa vyeo watumishi. Kweli nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, alipandisha vyeo watumishi 232,532, na mwaka huu wa fedha katika bajeti hii, fedha imetengwa kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi zaidi ya 219,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niihakikishie Kamati yako kwamba, ushauri wao waliotupa tutahakikisha tunawasimamia vizuri maafisa utumishi katika maeneo yote, kwamba wahakikishe wanaleta taarifa kwa wakati ili kupitia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge hili watumishi wale wanaostahili kupanda

vyeo, ambapo kumekuwa na malalamiko mengi, tuhakikishe kwamba tunapomaliza mwaka huu wa fedha tuwe tumetekeleza jukumu hili kadri mlivyotupitishia bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili lililoongelewa ni suala la kutangaza kazi ya Kituo cha Ubunifu *(Research and Innovation Centre)*, inayokuwa chini ya *e-GA*. Naomba jambo hili nilisemee angalau maneno machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kituo chetu hiki, kwa takribani kipindi cha miaka miwili *e-GA* imekuwa ikiandaa vijana takriban 400 hivi ambao wanafanya ubunifu katika teknolojia ya habari (TEHAMA). Mambo ambayo wanayafanya ni mambo ambayo ni makubwa kwa manufaa ya Taifa letu. Kwa mfano, wanafanya tafiti kwenye mambo ya *Blockchain Technology Crypto Currency* pamoja na mambo ya *Artificial Intelligence*. Wameweza kubuni vitu vingi ambavyo vimetupelekea kama nchi kupata sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi katika maonyesho yaliyofanyika kwenye *African Digital Platform* iliyofanyika nchini Zambia, tuliweza kupata nchi mbalimbali ambazo zimeweza ku-*develop interest* ya kuja Tanzania kujifunza namna vijana wetu wanavyofanya ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubunifu ule umeweza kufanya pia nchi yetu ipate tuzo mbalimbali. Kwa mfano, mwaka 2024 katika maonyoshe ya *UN*, kwenye *Digital Palatiform* iliyoandaliwa na *UN* nchini Korea Kusini tuliweza kupata tuzo ya kuanzisha mfumo wa e-Mrejesho ambapo nchi ya Tanzania iliibuka kinara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sifa zote hizi ni jitihada kubwa na uwekezaji mkubwa anaofanya Mheshimiwa Rais. Kama Kamati ilivyoshauri, tutaendelea kutangaza kazi hizi ili tuwavutie nchi nyingi zije kwenye kituo chetu zijifunze namna ambavyo vijana wetu wanafanya ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu hilo, baadhi ya vijana wetu wamepata ajira. Kwa mfano, kuna baadhi ya vijana wameajiriwa

*Singapore*, wengine wameajiriwa *UK*, na baadhi ya wengine wameleta maombi ya kuwachukua vijana wetu kutoka kwenye kituo hiki. Kwa hiyo, ni habari njema ambayo kama Wizara tutaendelea kushirikiana na Kamati, na maazimio yote haya manne waliyotushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kamati tumeyapokea chini ya usimamizi wa kiongozi wetu wa Wizara, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene. Tutahakimisha kwamba Kamati; na tumwombe sana Mwenyezi Mungu ili Bunge lijalo; na ninaamini kwa kazi kubwa tulifofanya Wabunge humu; Mwenyezi Mungu atanyoosha mkono wake, tutakutana tena Novemba ili tuone kazi kubwa ambayo tutakuwa tumetekeleza maazimio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mipango, jiandae Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na shukrani na pongezi kwa taarifa nzuri sana ya Kamati yenye kurasa 57, naomba nichangie mambo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, sisi kama Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji tumeyapokea na tunakubaliana na mapendekezo ya maazimio matatu yote yaliyopo katika ukurasa wa 44 mpaka ukurasa wa 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiambie tu Kamati kwamba kwenye Muswada mpya wa sheria ambao tumependekeza kuuleta hapa, Sheria ya Uwekezaji, baadhi ya mambo yatashughulikiwa kule pamoja na mapitio ya mpango mpya wa kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili katika mchango wangu nataka nichukue nafasi hii katika muktadha wa utawala

bora kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa tuzo ambayo ameipata jana, tarehe 4 Februari, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani watu wengi hawajaelewa vizuri ile tuzo, niieleze kidogo. Hii tuzo kwa Kiswahili inaitwa Tuzo ya Dunia ya Golikipa *(Global Goalkeeper Award)*. Unaweza ukaifananisha na wanamichezo hapa, na tuzo ambayo huwa inatolewa kwa golikipa bora katika mashindano ya *FIFA* ya *World Cup.* Kila mwaka huwa inatolewa kwa kila mashindano ya kipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwaka 2022 mtakumbuka Emmy Martinez wa Argentina ndiyo aliyeshinda hii tuzo. Huwa inatolewa kwa golikipa bora sana. Ndivyo hii *Foundation* ya *Gates* iliiga kutoka kwenye *FIFA* ikaanzisha tuzo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu ni wa saba kuipokea jana. Inatolewa tuzo kwa nani? Inatolewa tuzo kwa viongozi ambao wamechangia katika kufanikisha utekelezwaji wa malengo ya dunia endelevu *(Sustainable Development Goals 2030)*. Ukitaka kujua uzito wake, angalia waliopita ni akina nani? Wa kwanza aliyepata tuzo hii mwaka 2019 Narendra Modi, Waziri Mkuu wa India ndio wa kwanza kuipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisikutajie wa pili na wa tatu, nikutajie wa nne Ursula von der Leyen, Rais wa *European Commission* (Tume ya Ulaya). Yule mama mnamfahamu, lakini wa tano alikuwa nani? Mtu wa tano alikuwa Fumio Kishida, Waziri Mkuu wa zamani wa Japan, 2021 mpaka 2024. Mtu wa sita alikuwa ni Luiz Inácio Lula da Silva, Rais wa Brazil, mwaka jana hiyo; na wa saba aliyepata ndiye anaitwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kapewa tuzo hii? Kwa kutambua mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Sekta ya Afya Tanzania *specifically,* mchango wake katika kupunguza vifo vya akinamama wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulijiwekea lengo kwamba ifikapo mwaka huu, 2025 tuwe tumepunguza vifo kutoka 565 mpaka 225, lakini tume-*achieve* 104, mwaka 2022. Kwa hiyo, duniani hapa *indicator* kubwa ya kupima maendeleo ya afya na maendeleo ya watu ni afya ya akina mama na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ulikuwa unatilia shaka uthabiti na ubora wa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tafadhali bwana, waliotoa tuzo hii ni taasisi inayoheshimika duniani, lakini ligi yake waliyopata wengine ndio hawa akina Narendra Modi, Waziri Mkuu wa India. Tafadhali Bwana; Lula, Rais wa Brazili ambaye anasifiwa sana kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fumio Kishida, Waziri Mkuu mwenye mafanikio makubwa sana Japan. Amekaa miaka minne kule Japan, Waziri Mkuu anakaa miezi kadhaa, mwaka mmoja; huyu kakaa miaka minne, kapata tuzo, na huyu Mama Ursula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuwaomba Watanzania watembee kifua mbele, kwani tunaye kiongozi thabiti, Rais imara ambaye anasimamia ajenda zake. Mafanikio haya pia ni mafanikio ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi ambacho leo kinaazimisha miaka 48. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mafanikio haya ni ya Serikali. Mafanikio haya ni ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kuwapata wagombea watatu katika uchaguzi wa mwaka 2025. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Balozi Emmanuel

John Nchimbi ambaye anaenda kuwa mgombea mwenza, na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi anaenda kuwa mgombea Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa safu hii ambayo imepatikana wakati Chama cha Mapinduzi kinatimiza miaka 48, itawafanya watu wasiingize timu uwanjani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo chini ya uongozi wa Dkt. Wakili Msomi, ambao umetuwakilisha leo hapa na taarifa zetu mbili. Ni taarifa nzuri ambazo Serikali kwanza tunazipokea na kuziunga mkono, lakini pili tunachukua maelekezo yao yote na maazimio yote ili kwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niseme mambo machache ambayo yamesemwa kwenye Kamati na sisi tunayaunga mkono. Jambo la kwanza, Kamati imeongea kuhusiana na umuhimu wa uwepo na ufanisi wa Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inaunda Tume hii ilikuwa na makusudi kwamba kila sheria itakayotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano lazima ifanyiwe utafiti kwanza na Tume ya Kurekebisha Sheria. Kamati imetoa maazimio hayo, sisi tumeyapokea na tuahidi kwamba nikiwa Waziri mwenye dhamana ya haki nitakwenda kutekeleza jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu ambaye Mheshimiwa Prof. Kitila amemwaga sifa nyingi, lakini katika suala la haki tunafahamu ya kwamba aliunda Tume ya Haki Jinai ambayo imetoa mapendekezo ya kufumua mfumo mzima wa haki jinai, nasi Serikali tumeanza kuyafanyia kazi. Hata hivyo, juzi wakati wa Sherehe ya Siku ya Sheria ambapo yeye, Mheshimiwa Rais alikuwa Mgeni Rasmi, alisema sasa anapeleka nguvu katika haki madai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa haki jinai huku tayari gari limeshika mwendo, sasa tunakwenda kwenye hakimadai. Huku napo tayari tuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tusimamie vizuri eneo hilo ili wananchi pia wapate haki zao katika masuala ya madai. Katika kutekeleza hayo, Mheshimiwa Rais amekuja na mpango ambao umepewa jina lake, kwa heshima yake unaitwa *Mama Samia Legal Aid Campaign*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mpango huu ambao Kamati imeelezea vizuri na kuipongeza Serikali; mosi, ni kutoa elimu ya sheria kwa wananchi wote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na pili, kutoa msaada wa kisheria hususan kwa wananchi wanyonge waliopo vijijini ambao hawawezi kumudu gharama za juu za Mawakili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu umeshakwenda katika mikoa 17 mpaka sasa, na mpango ni kwamba tukifika Aprili, 2025 mikoa yote 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa imefikiwa na mpango huu. Mpaka hivi sasa mpango huu umeshatatua migogoro zaidi ya 7,000 na tunaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi, tarehe 01 - 08 mwezi Machi katika wiki ya wanawake duniani mpango huu unakwenda kuungana na sherehe za wiki ya wanawake duniani na tunahamia mkoa wa Arusha kuhakikisha tunaufanya vizuri kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, niseme naishukuru sana Kamati. Tumepokea maazimio yote na Serikali, tunakwenda kuyashughulikia na kuyatekeleza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa

Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuhitimisha hoja ya Kamati ambayo ililetwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote tisa na Mawaziri na Naibu Mawaziri wanne ambao wamepata fursa ya kuchangia hoja hizi za Kamati zetu zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa sehemu kubwa au kwa 100% wachangiaji wote waliopata fursa hii wameitumia hii fursa kukubaliana na hoja za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge na Waheshimiwa Naibu Mawaziri waliopata fursa ya kuchangia eneo linalohusu Utawala, Katiba na Sheria wamejielekeza kwenye hoja za Kamati moja kwa moja na wameweka mkazo kwa Waheshimiwa Wabunge. Pia, Waheshimiwa Mawaziri wameonesha namna bora ambayo wataenda kutekeleza maazimio haya ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nasoma, yapo maeneo mawili ambayo nilidhani ni muhimu sana hayakupata mkazo sana, mkazo ambao unastahili ukilinganisha na umuhimu wake. Kwa hiyo, tunapohitimisha hoja hii, nilitamani maazimio haya mawili yawe sehemu ya maazimio ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza, inahusu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Naamini unakubaliana nami kwamba tunayo sera nzuri sana ya uwekezaji nchini na sasa tunaboresha sheria kwa ajili ya kutengeneza sheria bora kabisa ya uwekezaji. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba hakujafanyika utafiti au kama utafiti umefanyika haujawekwa vizuri ili kubainisha kwanza, uwezo wetu wa ndani wa kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi na pili, uwezo wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini tukiwa na sera ya uwekezaji na sheria ambazo zitawasaidia Watanzania, kwanza kuelewa maeneo ya uwekezaji yanayoendana na uwezo wao wa kifedha, kimtaji na kiujuzi yakawekwa sambamba na maeneo

ya uwekezaji ambayo labda yanahitaji ujuzi na mitaji mikubwa ambayo inawataka wageni wawekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini yapo maeneo mengi sana kama Serikali yetu itaongeza nguvu ya kuwawezesha Watanzania, basi tutapata Watanzania wengi sana watakaowekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa natoa mfano eneo la Kilimo, eneo la Mifugo na maeneo mengine mengi ambayo kama nchi tutaamua kuwekeza nguvu, basi tutawasaidia Watanzania wengi na hatutahitaji wageni kuwekeza katika maeneo ambayo Watanzania wenyewe tunaweza kufanya. Kwa hiyo basi, kwa sababu hili lilijadiliwa sana kwenye Kamati, naomba liwe sehemu ya maazimio ya Bunge lako na azimio lisomeke kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa, imebainika kuwa uvutiaji wa wawekezaji nchini hauzingatii vipaumbele vya maeneo ya uwekezaji baina ya yale ambayo Watanzania wana uwezo nayo na yale ambayo hawana uwezo nayo kwa kuzingatia viwango vya mitaji, ujuzi na teknolojia;

Na kwa kuwa, kuacha hali ilivyo kunawaingiza Watanzania kwenye ushindani usio sawa wa kibiashara;

Na kwa kuwa, hali hii inaweza kuwaongezea Watanzania wengi umasikini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kuwa Serikali isimamie Sera ya Uwekezaji kwa kubainisha maeneo ya vipaumbele kwa wageni na kwa Watanzania na kuwajengea uwezo Watanzania kuwekeza kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naomba kuliwasilisha kama azimio la Kamati na ninaomba sasa ligeuke kuwa pia azimio la Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusu Wizara ya Katiba na Sheria. Utakubaliana nami kwamba tuna changamoto sana ya uendeshaji wa mashauri katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Tuna changamoto ya watumishi, lakini pia tuna changamoto ya kibajeti. Yapo mashauri mengine tunalazimika kutafuta *consultants* kutoka nje ya nchi ili kuyafikia kuyafanyia kazi. Ipo mikataba mbalimbali ambapo tunatumia fedha nyingi sana kupata watu toka nje kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili pia limejadiliwa kwenye Kamati na ninaomba liwe pia sehemu ya maazimio ya Bunge lako na maazimio haya yasomeke kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya bajeti na upungufu wa rasilimali watu kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

Na kwa kuwa, upungufu huu unakwamisha jitihada za Serikali na Ofisi hii kushughulikia mashauri muhimu yenye maslahi makubwa kwa Taifa letu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2025/2026 ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutekeleza wajibu wake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena kukushukuru wewe na wote waliochangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu shughuli za Kamati ya mwaka 2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu shughuli za Kamati ya mwaka 2024, ilipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa hii ni rasmi ni maazimio ya Bunge kwa Serikali. Nawapongeza Mwenyekiti na Kamati yako kwa kazi nzuri mliofanya.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu ambayo nimeitoa leo hapa muda mchache uliopita. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote, Mawaziri na Naibu Mawaziri waliochangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla tumepata wachangiaji 13, Wabunge tisa na Naibu Mawaziri na Mawaziri wanne. Wote kwa umoja wao wameunga mkono hoja na kukubali kwamba hoja ina mashiko na inatakiwa iwe ndiyo maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Kamati hii ya Sheria Ndogo ni kama jicho la Bunge au ni kama *watchdog.* Ndiyo chombo cha Bunge hili kuhakikisha kwamba kazi yake inafanyika vizuri. Ibara ya Nne ya Katiba kama nilivyoisema pale awali inaeleza bayana kwamba kazi za kutunga sheria ni ya Bunge, chombo pekee chenye uwezo wa kutunga sheria ni Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Ibara ya 97 (5) inatoa tena nafasi kwa Bunge hili kukasimu madaraka yake kwa watungaji wengine, ambao ni Wizara, Idara za Serikali au watu mbalimbali Serikalini kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kamati hii ya Sheria Ndogo inatazama kama hawa waliokasimiwa madaraka ya Bunge, je, wamefanya vizuri au kuna dosari na kasoro? Ndiyo kazi hiyo pekee kubwa tunayoifanya. Sasa baada ya kufanya kazi hiyo tunakaa, tunachambua sheria ndogo hizo na kutoa maelekezo ambayo yanakuja hapa, yanakuwa maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba maazimio hayo mengi yanatekelezwa kama yanavyotolewa. Nitataja hapa Wizara chache ambazo zimefanya maazimio hayo vizuri bila kupindisha kwa kufuata maelekezo na maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha imetimiza maazimio au kwa kurekebisha sheria ndogo mbili vizuri na kwa ufasaha mzuri. Wizara ya Viwanda na Biashara imetekeleza maazimio ya Bunge kwa kurekebisha kabisa sheria ndogo moja, na Wizara ya Uchukuzi imetekeleza kwa kurekebisha na kutangaza sheria ndogo tisa, na tayari zinafanya kazi vizuri kwani kasoro zimeondolewa na zipo sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pia, imetekeleza kwa kurekebisha sheria ndogo 24 vizuri bila mabaki yoyote na zinafanya kazi vizuri, lakini wapo wachache ambao hawakufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wa TAMISEMI katika Manispaa ya Mtwara kwa mfano kuna sheria ndogo nne hawajazifanyia kazi. TAMISEMI hiyo hiyo, Halmashauri ya Manispaa ya Singida sheria ndogo tatu hawajazifanyia kazi na bado zinabaki kuwa kero na zina dosari ambazo zinasumbua wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ile kazi ya Bunge ya kuhakikisha kwamba wananchi wasipate sheria ambazo zina kero na matatizo, haijafanyika kwenye maeneo hayo mawili au matatu ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kusisitiza kwamba hao ambao wamebainika wafanye kazi hiyo vizuri haraka na

tumeeleza kwenye taarifa kwamba kwenye vikao vya Kamati mwezi Machi, taarifa zije tuone kama wametekeleza au kama kuna upungufu. Hiyo ndiyo kazi ya Kamati ya Sheria Ndogo ambayo tunaifanya kwa niaba ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2024; wanaoafiki waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo. Wote mmeafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2024 ilipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**NAIBU SPIKA:** Nakupongeza na wewe Mwenyekiti kwa kazi nzuri na Wajumbe. Pia, nawapongeza Serikali kwa maneno mazuri na hasa haya ya pongezi kwa Mheshimiwa Rais, ambaye sasa anatambulika Kimataifa. Tuna jemedari, tuna kiongozi ambaye ni *results oriented President*. *(Makofi)*

Nina tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tarehe 6 Februari, 2025 siku ya Alhamisi utafanyika mhadhara kuhusu *Artificial Intelligence*. Mhadhara huo utatolewa na Profesa Raghunathan kutoka *Institute of Technology Madras India*, mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria mhadhara huo muhimu ili kuwajengea uelewa zaidi kuhusu *Artificial Intelligence*.

Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.01 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 6 Februari, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*